**17 JUNI, 2022**

# BUNGE LA TANZANIA

__________

## MAJADILIANO YA BUNGE

___________

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Arobaini na Sita – Tarehe 17 Juni, 2022

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU WA MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Francis Leornad Mtega.

Na. 401

**Mamlaka ya Mji Mdogo wa Rujewa kuwa Mamlaka kamili**

**MHE. ORAN M. NJEZA K.n.y. MHE. FRANCIS L. MTEGA** aliuliza:-

Je, ni lini Mamlaka ya Mji Mdogo wa Rujewa inaenda kuwa Mamlaka kamili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Jimbo la Mbarali kama ifuatavyo:-

Mhesimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura 288 pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa Mwaka 2014, vigezo na taratibu zinazopaswa kufuatwa ni pamoja na maombi rasmi kuwasilishwa Ofisi ya Rais TAMISEMI. Ofisi ya Rais TAMISEMI itakapopokea maombi rasmi ya Halmashauri ya Mji Mbarali itafanya uchambuzi na tathmini ya kukidhi vigezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kumekuwa na changamoto za uendeshaji na tija za kuwepo kwa baadhi ya Mamkaka za Miji Midogo. Ofisi ya Rais TAMISEMI inafanya uchambuzi na kubaini tija ya kuendelea kuwepo au la, kwa baadhi ya Mamlaka za Miji Midogo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, iliyoko Wilaya ya Mbeya

yenye watu zaidi ya laki moja iliishapita vigezo vyote vya vikao vyote vya *DCC, RCC* na hata kiuchumi iko vizuri. Je, ni lini Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi itapanda kuwa Halmashauri ya Mji?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano, aliagiza hata kubadili Jina la Jimbo la Mbeya Vijijini. Je, ni lini Serikali itabadili jina la Jimbo la Mbeya Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Njeza Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji Mdogo wa Mbalizi ni kweli kwamba ni mamlaka ya Mji ya muda mrefu lakini tayari imeshafikisha vigezo kwa maana ya idadi ya watu, uwezo wa kiuchumi, lakini wameshafuata taratibu na kuwasilisha ofisi ya Rais TAMISEMI. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Ofisi ya Rais – TAMISEMI sasa tunafanya tathmini lakini pia tunatambua vigezo hivyo na baadaye tutatawakilisha kwa mamlaka husika ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa kwa kadri itakavyokuwa inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na jina la Halmashauri ya Jimbo la Mbeya Vijijini kubadilishwa ni taratibu ambazo zinafanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kwa hivyo Ofisi ya Rais – TAMISEMI tumechkua hili tutashirikiana na Wizara husika kuona uwezekano wa

kutekeleza maelekezo hayo ya Mheshimiwa Rais.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Londo.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri, amezungumza kwamba moja ya vigezo vya kupata Halmashauri ni maombi ya Halmashauri husika kufika TAMISEMI. Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa imeshaomba kwa miaka mitano mfululizo kuanzisha Halmashauri katika Jimbo la Mikumi, tuna vigezo vyote ambavyo vingine vimepitiliza.

Je, ni nini kauli ya Serikali kwa wananchi wa Jimbo la Mikumi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dennis Londo, Mbunge wa Jimbo la Mikumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Halmashauri ya Kilosa ina Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mikumi, na ninafahamu kwamba vikao vya awali vya kuomba kupandishwa hadhi kuwa halmashauri ya Mji vimeanza, kwa ngazi ya *DCC*, lakini nafahamu kwamba *RCC* bado haijakaa kupitisha maombi hayo. Kwa hiyo, nimwelekeze Mkuu wa Mkoa wa Morogoro kufanya mapema suala hili ili tuweze kuona kama inakidhi vigezo hivyo baada ya

kuwasilishwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Ningependa kujua Halmashauri ya Bunda ina Majimbo mawili ambayo Halmashauri moja ipo Jimbo la Mwibara lakini Majimbo hayakutani, yamekatwa katikati na Jimbo la Bunda Mjini. Ni lini sasa Serikali itapeleka Halmashauri ya Nyamswa kwenye Jimbo la Bunda Vijijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu maombi ya kuanzisha mamlaka mpya kwa maana ya Halmashauri ya Nyamswa, nimuombe Mheshimiwa Mbunge lakini nimuelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, kuanza taratibu ambazo ziko kwa mujibu wa Sheria Sura 288 na kuwasilisha Ofisi ya Rais TAMISEMI ili tuweze kufanya tathmini ya vigezo hivyo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Songe Mbunge wa Busega.

Na. 402

**Kupandisha Hadhi Shule ya Sekondari Nassa Busega**

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE** aliuliza:-

Je ni lini ahadi ya Rais wa Awamu ya Tano ya kuipandisha hadhi Shule ya Sekondari Nassa itatekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile Mbunge wa Jimbo la Busega kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Mwongozo wa Uanzishaji na Usajili wa Shule wa Mwaka 2020 uliotolewa na Wizara ya Elimu unabainisha hatua za kuipandisha hadhi shule kuwaya Kidato cha Tano na Sita kama ifuatavyo:-

Mwombaji ambae ni Mkurugenzi ataandika barua kwa Kamishna wa Elimu kupitia Mdhibiti Mkuu wa Ubora wa Shule Kanda. Barua hiyo itaambatishwa na taarifa ya ukaguzi wa Mdhibiti wa Ubora wa Shule Kanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega kutenga fedha kupitia mapato ya ndani ili kukamilisha miundombinu

muhimu inayowezesha shule hii kukidhi vigezo vya kupandishwa hadhi ya kuwa na Kidato cha Tano na cha Sita.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Songe.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa majibu yake awali, lakini nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Busega ni moja ya Halmashauri mpya hapa nchini na makusanyo yake ni kidogo sana.

Je, Serikali haioni sababu ya msingi ya kutenga fedha kutoka Serikali Kuu ili kuanza ujenzi wa miundombinu hii ambayo Mheshimiwa Waziri ameitaja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Jimbo la Busega kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Mkurugenzi afanye tathmini kubaini gharama zinazohitajika kujenga madarasa hayo na miundombinu hiyo na awasilishe rasmi Ofisi ya Rais – TAMISEMI ili tuweze kuona kama Halmashauri inaweza kujenga sehemu ya miundombinu hiyo, lakini eneo lingine la miundombinu, Serikali Kuu iweze kuchukua. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sima.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Singida Mjini tumekarabati na kujenga shule ya Sekondari ya Mungumaji na kila kitu kiko tayari na tumeomba ili kuweze kupandishwa hadhi kuwa Kidato cha Tano na Sita lakini mpaka sasa kibali hicho hakijatoka.

Je, ni lini Serikali itatoa kibali cha kuhakikisha sasa tunaanza shule ya Kidato cha Tano na Sita pale Mungumaji Sekondari?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mussa Sima, Mbunge wa Jimbo la Singida Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Sima na Manispaa ya Singida Mjini kwa kufikia hatua hiyo kukamilisha vigezo vinavyohitajika na nimhakikishie Ofisi ya Rais TAMISEMI, tumelichukua hili na baada ya hapa nitafuatilia nione wapi tumekwama ili shule zianze huduma mapema. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Shule ya Sekondari Lemira ina hekta 20 lakini ina madarasa toshelevu kabisa ya kuweza kuanzisha Kidato cha Tano na cha Sita.

Je, ni lini Serikali itaipandisha hadhi shule hii ya Lemira kuwa Kidato cha Tano na cha Sita?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Jimbo la Hai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa kufuatilia kama Halmashauri ya Hai imekwishawasilisha maombi hayo kwa Kamishina wa Elimu lakini baada ya kupata ripoti ya Mdhibiti wa Kanda wa Elimu. Kama hiyo imekwishafanyika, nitawasiliana na yeye baada ya Kikao hiki ili tuweze kuona namna gani tunalisukuma hili liweze kukamilika mapema.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, tofauti na shule ya Changarawe ambayo Serikali mmekuwa mkitusaidia sana. Shule ya JJ Mungai ambayo ni ya Kidato cha Kwanza mpaka cha Sita kimekuwa na uhitaji wa mabweni na uboreshaji wa miundmbinu yake.

Je, Serikali mko tayari kutusaidia kama mlivyofanya shule ya sekondari Changarawe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cosato Chumi, Mbunge wa Jimbo la Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, majengo yetu au miundombinu yote katika shule zetu kwanza tunayo bajeti ya kumalizia majengo ambayo yameanzishwa na wananchi kwa maana ya maboma, kwa kutumia *EP4R* na tumeendelea kufanya katika miaka yote na mwaka huu pia. Pia kwa sekondari tunayo bajeti ya *SEQUIP* lakini tunakwenda kutekeleza mpango wa *BOOST*. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika eneo hilo kwanza tutakwenda kuona majengo yanayohitajika, lakini tuone gharama zake, kwa kushirikiana na mapato ya ndani ya Mji wa Mafinga na Ofisi ya Rais TAMISEMI itaona namna gani tunaweza tukatoa fedha kwa ajili ya kazi hiyo.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Jaqueline Kainja Andrew.

Na. 403

**Kuunga mkono juhudi za wananchi ujenzi wa shule – Urambo**

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA K.n.y MHE. JACQUELINE K. ANDREA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kukamilisha ujenziwa Shule katika Kijiji cha Izengabatogilwe, Kata ya Ugalla - Urambo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jaqueline Andrea Kainja, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19 imepeleka Shilingi Milioni 40 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika kitongoji cha Gimagi kwenye shule shikizi ya shule Mama ya Izengabatogile.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga Shilingi Milioni 220 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya madarasa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi katika Halmashauri ya Wilaya ya Urambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya madarasa ikiwemo ya shule katika Kijiji cha Izengabatogile, Kata ya Ugalla, Wilayani Urambo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwinjuma.

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwenye Jimbo la Muheza, Serikali iliahidi kupeleka Shilingi

Milioni 600 kwa ajili ya shule mbili za sekondari kwenye Kata mpya. Kata moja ya Makole haijapata hata shilingi moja mpaka hivi tunavyoongea na mwaka wa fedha unakaribia kuisha.

Je, Serikali ina mpango wowote wa kupeleka fedha hizi kama ilivyoahidi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, Mbunge wa Jimbo la Muheza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa sekondari mpya katika Kata ambazo hazina sekondari unaendelea na kwa awamu ya kwanza Serikali ilipeleka Shilingi Milioni 470 katika Kata hizo, na itakwenda kumalizia Shilingi Milioni 130 kukamilisha Milioni 600. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kama Kata hii ya Makole haipo kwenye orodha ya kupata Milioni 600 na haijapata, tutafuatilia tuone ni kwanini haijapata ili iweze kupata kama ipo kwenye orodha ya kupata shule hizo.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri zetu

mbalimbali hapa nchini kuna nguvu za wananchi zimetumika kujenga shule kwenye *level* ya shule za msingi na shule za sekondari, zimebaki kama maboma kwa muda mrefu bila ukamilishaji.

Je, Serikali sasa kwanini isizitake Halmashauri, izitambue na kuwapa *timeframe* wa ukamilishaji wa majengo hayo ambayo ni nguvu za wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali kwa nia njema ya kuhakikisha kwamba maeneo yetu yote yanakuwa na shule za msingi kwa maana ya vijiji lakini na shule za sekondari kwenye Kata, ilihamasisha nguvu kazi za wananchi lakini Serikali inachangia nguvu zile kukamilisha maboma ya madarasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya kazi kubwa sana, sote ni mashahidi kwamba fedha nyingi sana zimetolewa kwa ajili ya kukamilisha madarasa hayo katika miaka yote ya fedha ukiwepo mwaka huu, kupitia *EP4R*, kupitia *SEQUIP* lakini tunakwenda na mpango wa *BOOST*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunafahamu kwamba tungependa kuweka *deadline* kukamilisha maboma hayo kwa Halmashauri, lakini pia bado kuna changamoto za

uwezo wa mapato ya ndani kukamilisha kwa pamoja kutoka na wingi wa majengo ambayo yamejengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba safari ni hatua, tumekwenda kwa kiasi kikubwa sana na tutakwenda kukamilisha maboma yaliyokamilika, kwa sababu mpango umewekwa vizuri kwa ajili ya shughuli hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete.

Na. 404

**Hitaji la maji Mchinga**

**MHE. SALMA R. KIKWETE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka maji katika Jimbo la Mchinga kutoka kwenye chanzo cha maji cha Ng'apa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mbunge wa Jimbo la Mchinga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imeendelea kuboresha huduma ya maji katika Manispaa ya Lindi kwa kujenga miradi ya maji inayotumia chanzo cha visima vya Ng'apa. Maji yamefika

eneo la Mitwero na kazi inayoendelea ni kuyafikisha maji Mchinga ambapo Kata za Mchinga, Mvuleni, Kilolambwani na Kilangala zenye jumla ya vijiji 18 zitanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, wananchi katika vijiji nane katika Kata ya Mbanja inayopitiwa na bomba kuu kwenda Mchinga watanufaika. Kwa sasa, Mkandarasi anaendelea na kazi. Kazi zinazoendelea ni ulazaji wa bomba kuu umbali wa kilometa 42, ulazaji wa mabomba ya usambazaji kilometa 12.9 na ujenzi wa matanki manne yenye ujazo wa lita 100,000, mawili yenye ujanzo wa lita 200,000 na moja la lita 680,000. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2022/2023.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salma.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza ninaishukuru Serikali kwa majibu yake mazuri na yenye matumaini makubwa kwa jengo la Mchinga na kwa Manispaa yetu ya Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali la nyongeza, sambamba na hili tuna suala zima la ukarabati kwenye Kata yangu ya Milola na chanzo kiko kule Chipwapwa, fedha tulizozipata ni shilingi milioni 50 na jana wamesaini mkataba, lakini mahitaji ni shilingi milioni 490.

Je, fedha zilizobaki zitapatikana lini na hii ikiwa na maana kwamba huu ndiyo mwisho wa bajeti wa 2021/2022?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mbunge wa Jimbo la Mchinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kata aliyoitaja ni kweli fedha zimekwenda kwa utangulizi, lakini kama ilivyo kawaida kila mgao unapokuwepo tunaendelea kuleta fedha. Kwa wiki hizi mbili zilizobaki za kumaliza mwaka huu wa fedha tutajitahidi kuona uwezekano wa kuongeza fedha kadri ya mahitaji. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mradi wa Maji wa Bunda kutoka Nyabeu tayari Serikali imeshafikisha Bunda Mjini, lakini changamoto kubwa iliyokuwepo ni miundombinu ya usambazaji maji, ni ya zamani, ndiyo maana mpaka leo wananchi wameshindwa kupata maji safi na salama. Je, ni lini sasa Serikali watahakikisha wanaweka miundombinu mipya ili kata zote 14 za Bunda Mjini ziweze kupata maji safi na salama? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyokiri maji yameshafika mjini; lengo la Wizara ni kuhakikisha maji

yakishafika katika maeneo ya mwanzoni, basi sasa usambaji utafuata na miundombinu ya zamani yote tunakwenda kuendelea na ukarabati kuhakikisha tunaleta mabomba na miundombinu ambayo itaendana na idadi ya watu waliopo kwa sasa. Hivyo, nipende kukwambia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mwaka ujao wa fedha tutaendelea na ukarabati wa mradi huu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwenye Kata ya Nyakatuntu kuna chanzo cha maji Kitoboka, na kwenye Kata ya Songambele kuna chanzo cha maji Kitega ambacho wananchi wanapata adha kuhusu maji safi na salama. Je, ni lini Serikali itaboresha chanzo hiki lakini pia kukamilisha visima ambavyo tumetengewa kwenye bajeti? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bilakwate, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, visima hivi ambavyo amevitaja Mheshimiwa Mbunge tunaendelea kuvifanyia kazi kuona kwamba pamoja na hivi vyanzo vya maji alivyovitaja vyote tuweze kuvitumia, lengo ni kuona tunapata maji mengi yatakayoweza kuwafikia wananchi wengi. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge avute Subira, kazi ambayo tumeianza kwa pamoja tutakwenda kuikamilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Mohamed Jumah Soud.

Na. 405

**Vigezo vinavyotumika kuanzisha Vituo vya Polisi**

**MHE. MOHAMED JUMAH SOUD** aliuliza:-

Je, ni vigezo gani hutumika kuanzisha Vituo vya Polisi maeneo yenye idadi kubwa ya watu pamoja na vitendo vya uhalifu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Jumah Soud, Mbunge wa Donge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo vinavyotumika kuanzisha Vituo vya Polisi ni ongezeko la watu, ongezeko la matukio ya uhalifu, umbali kati ya Kituo kimoja cha Polisi na kingine, uwepo wa miundombinu ya Serikali, shughuli za kibiashara pamoja na maeneo ya kimkakati kwa ajili ya ulinzi na usalama wa nchi, uwezo wa kibajeti na utayari wa wananchi na Mamlaka zao za Serikali za Mitaa ni vigezo vingine tunavyovitumia. Hatua inayofuata ni mapendekezo ya uanzishwaji wa kituo husika kuwasilishwa kwenye Kamati ya Usalama ya Wilaya, Kamati ya Usalama ya Mkoa na

kisha ushauri wao huwasilishwa kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi kwa ajili ya utekelezaji. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Soud.

**MHE. MOHAMED JUMAH SOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali la nyongeza. Kwa kuwa Jimbo la Donge limepanuka sana na hivyo vigezo ambavyo amevizungumza Mheshimiwa Naibu Waziri vingi vyake vinakidhi kuanzishwa Kituo cha Polisi katika Jimbo la Donge na halikadhalika uharamia umeongezeka sana kiasi kwamba mazao sasa hivi kulima kumekuwa ni shida, mifugo kufuga imekuwa ni tabu. Swali hili niliwahi kuuliza hapa na Mheshimiwa Naibu Waziri aliniahidi kwamba atafanya tathmini ili kuangalia uwezekano wa utekelezaji. Sasa je, ananiahidi vipi ile tathmini imeshafanyika na kama haijafanyika basi lini itakamilika ili utekelezaji uanze. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la moja la nyongeza la Mheshimiwa Soud, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kama nilivyosema ameeleza hapa Jimbo la Donge linakidhi vigezo hivyo, kupitia Bunge lako Tukufu nimwelekeze Kamishna wa Polisi wa Zanzibar na Wasaidizi wake waweze kufanya tathmini ya eneo hilo. Wakibaini kwamba linakidhi vigezo, basi hatua za kujenga Kituo cha Polisi liweze

kufanyika. Mheshimiwa Mbunge tutapeana ushirikiano ili kuona kwamba jambo hilo linafanyika. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile.

Na. 406

**Makusanyo ya fedha katika Daraja la Nyerere lililopo Kigamboni**

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUNGULILE** aliuliza:-

Je, ni kiasi gani cha fedha kimekusanywa tangu Daraja la Nyerere lianze kutumika na ni lini huduma ya daraja hili itatolewa bila malipo?

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndungulile, Mbunge wa Kigamboni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Mfuko wa *NSSF* ulianza kupokea fedha zitokanazo na tozo kwa watumiaji wa Daraja la Nyerere mnamo tarehe 14 Mei, 2016 baada ya kuzinduliwa. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Mei, 2022, Mfuko ulikuwa umekusanya jumla ya shilingi bilioni 66.86.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kupunguza tozo kwa watumiaji wa daraja hilo tangu kuzinduliwa kwake kwa kuzingatia tathmini ya uwezo wa wananchi kumudu tozo hizi. Kwa mara ya mwisho, Serikali imepunguza tozo husika tarehe 21 Mei, 2022. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUNGULILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; nataka kujua kwamba kwa sasa kimebaki kiasi gani cha deni la gharama za ujenzi ambacho kimebaki?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kwa mujibu wa majibu ambayo amenipa kwamba tarehe 21 Mei, 2022 walifanya mapitio ya tozo za daraja na kuanzisha utaratibu wa tozo za siku, wiki na mwezi. Je, ni lini utaratibu huu wa tozo za siku, wiki na mwezi utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri swali la kwanza lina takwimu unaweza ukaliacha, jibu swali la pili.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakamilisha mfumo wa kuanza tozo kwa siku, wiki na mwezi; nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunategemea kwamba kuanzia tarehe 1 Julai, 2022, mfumo huu utaanza kutumika. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Tunaendelea, Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

Na. 407

**Ujenzi wa Barabara ya Old Shinyanga – Solwa hadi Salawe**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya kutoka *Old* Shinyanga kupitia Iselamagazi, Solwa hadi Salawe kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa sehemu ya Solwa - Salawe yenye urefu wa kilometa 15.35. Kwa sehemu iliyobaki kutoka Solwa kwenda Iselamagazi hadi *Old* Shinyanga yenye urefu wa kilometa 64.66 kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inaendelea. Baada ya kazi ya usanifu kukamilika na gharama ya ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha ili kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Swali la kwanza; kwa kuwa Serikali imeshakamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa kipande cha kutoka Solwa kwenda Salawe kilomita 15, je, ni lini ujenzi utaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa sehemu ya Solwa – Iselamagazi yenye kilomita 64.66, upembuzi unaendelea. Je, ni lini huo upembuzi utakamilika ili ujenzi uanze? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu uliopo ni kwamba, kwa kuwa barabara hii ni moja itakuwa na *lot* moja kwa hiyo tunataka tupate tathmini ya gharama ya barabara nzima ili tuweze kupata gharama ya barabara nzima na kuianza kuijenga kwa kiwango cha lami kwa jinsi itakavyokwenda. Kwa barabara hii ambayo imebaki kilomita 64.66 kama tulivyosema, usanifu na upembuzi yakinifu unaendelea, tunategemea utakwenda kadri ya mkataba ulivyopanga na tunaamini kwamba kabla ya mwisho wa mwaka huu 2022, usanifu utakuwa umekamilika. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Kabula Ennock Shitobela.

Na. 408

**Kupunguza Tozo Zinazotozwa na *TPA***

**MHE. KABULA E. SHITOBELA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapunguza tozo zinazotozwa na *TPA* kwani imekuwa ikitoza tozo kubwa kwenye mizigo kuliko Makampuni binafsi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE FREDY MWAKIBETE)** alijibu**:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabula Enock Shitobela, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuhakikisha Bandari zote za Tanzania zinatoa huduma bora na kwa gharama nafuu ili kuendana na hali halisi ya ushindani katika bandari za ukanda wa Afrika Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika. Katika kufikia azma hiyo, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ipo katika hatua za mwisho za kufanya mapitio ya gharama za huduma za bandari. Hivi sasa, uchambuzi wa maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali yanafanyiwa kazi na zoezi hili linatarajiwa kukamilika Julai, 2022.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabula.

**MHE. KABULA E. SHITOBELA** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, nili Serikali sasa itakamkilisha ujenzi wa bandari zote zilizosalia kwa Mkoa wa Mwanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni sheria gani inayotumika kwenye tozo za bandari hapa nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabula maswali yako yote mawili yamekwenda nje kabisa ya swali lako la msingi. Kwa hiyo, tunakuomba baadaye Mheshimiwa Waziri ukipata takwimu sahihi kaa na Mheshimiwa Kabula umwelezee, sawa.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge.

Na. 409

**Marekebisho ya Kanuni za Uvuvi**

**MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafanya marekebisho ya Kanuni za Uvuvi za mwaka 2020 ambazo zinalalamikiwa na wadau wa Sekta ya Uvuvi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inaendelea kufanya marekebisho ya Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2020 ili kuboresha shughuli za uvuvi nchini na biashara ya mazao ya uvuvi ndani na nje ya nchi kwa kuzingatia maoni ya wadau wa sekta ya uvuvi na maoni yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwenye Vikao kati ya Wizara na Kamati hiyo vilivyofanyika tarehe 30 Machi, 2020 na tarehe 25 Agosti, 2021. Aidha, Marekebisho ya Kanuni husika yanatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2022.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Niipongeze na niishukuru Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi kwa hatua ambayo imefikia, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; wakati Wizara inaendelea kurekebisha Kanuni hizi au inakwenda kufanya marekebisho ya Kanuni hizi, ilituma timu ya wataalam kwa ajili ya kufanya utafiti katika maeneo ambamo shughuli za uvuvi zinafanywa na wataalam hawa waliwasilisha ripoti ambayo nadhani Wizara ndiyo inafanyia kazi ikiwa ni kama msingi wa kutengeneza kanuni hizi. Swali la kwanza; je, maoni ya wataalam yatazingatiwa katika marekebisho ya kanuni hizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Wizara imeshirikisha wadau mbalimbali katika kufanya marekebisho ya kanuni hizi ikiwa ni pamoja na Kamati ya Bunge inayohusiana na Sekta ya Mifugo. Je, Wizara ipo tayari wakati inaendelea kufanya marekebisho kanuni hizi kuwashirikisha pia Wabunge wanaotoka kanda za uvuvi ili kuongeza maoni? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, maoni ya wataalam yatazingatiwa nataka nimhakikishie yeye na Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla, wataalam maoni yao tutayazingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, je, Wabunge ambao walishiriki katika kuibua hoja hii wale wanaotoka katika maeneo ya uvuvi watashirikishwa? Hili pia tutahakikisha tunawashirikisha ili kusudi kuweza kutoka na Kanuni za pamoja. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Miongoni mwa kanuni ambazo zinalalamikiwa na wadau wa uvuvi ni pamoja na utitiri wa tozo unaotaka mmiliki alipe Dola 55, lakini chombo alipie Dola 55 na mvuvi alipe Dola 10. Ni lini watafanya

marekebisho ya kanuni hiyo ambayo inakwenda kuwatesa hao wavuvi ambao ni Watanzania wanalipa kwa dola? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lini tutarekebisha kanuni inayoonesha kwamba mmiliki wa chombo analipa leseni, mvuvi analipa leseni na chombo kinalipiwa leseni. Ni kweli kwamba, tunao utaratibu wa chombo cha chini ya mita 11 kinalipiwa leseni katika Halmashauri zetu za Wilaya kama ni sehemu ya mapato ya ndani. Kwa upande wa mmliki wa chombo na yeye analipishwa leseni na yule mvuvi analipishwa leseni ili tuweze kupata namba kwa maana ya takwimu ya wavuvi wangapi wanaoshiriki katika shughuli za uvuvi kila siku kwa kuwa na ile leseni. Hata hivyo, kwa maoni tuliyoyapokea kutoka kwa Wabunge tupo katika mchakato wa kuitafakari kanuni hii ili tuweze kuona namna iliyo bora ya kile cha kupata takwimu lakini vilevile ya kuweza kurahisisha shughuli zetu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Miongoni mwa kanuni ambazo zinalalamikwa na wavuvi ni ile kanuni ambayo inamlazimisha mvuvi kutokuvua chini ya mita 50 kwenda chini.

Je, wakati Serikali inaendelea na mikakati ya kurekebisha kanuni haioni haja ya kupeleka mitungi ya *oxygen* kwa wavuvi wadogo wadogo ili kuweza kuwaokoa na athari ya kuzama maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Njau, kumradhi Mheshimiwa Felista Njau, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wavuvi wapo wanaofanya shughuli za uzamiaji kwa ajili ya kuweza kupata rasilimali na hii ni katika zile kanuni tunazokwenda kuzifanyia kazi ya maboresho; na baadhi yao wanataka watumie zaidi ya mitungi 10, sisi tunadhani tunao uwezo wa kuruhusu lakini kwa uchache kwa sababu tunaamini matumizi ya mitungi mingi ni kinyume cha uhalisia wa kwenda kile anachokikusudia isipokuwa tu kama ana lengo lingine ambalo kinyume na uvuvi. Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa Wabunge, wawe na subira ni katika kama jibu la msingi la mwanzo kwamba ni sehemu ya majibu tukakayoyatoa kwenye marekebisho ya Kanuni zetu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itakuja na mpango wa kujenga vizimba vya kufugia Samaki katika Ziwa Duluti lilopo Arumeru Mashariki kwa lengo la ku…

**NAIBU SPIKA:** Hebu rudia tena hilo swali.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itakuja na mpango wa kujenga vizimba vya kufugia samaki katika Ziwa Duluti kule Arumeru Mashariki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pallangyo, swali lako ni tofauti kabisa na swali la msingi.

Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Katiba na Sheria. Mheshimiwa Nashon Bidyanguze.

Na. 410

**Hitaji la Mahakama ya Wilaya – Uvinza**

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya Uvinza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Uvinza ni moja ya miradi ya Mahakama inayotekelezwa katika kipingi mwaka wa fedha 2021/2022

kupitia programu ya maboresho ya Mahakama. Mkandarasi wa ujenzi wa Mahakama hii amepatikana ambaye ni *Lucas Construction* na kukabidhiwa eneo la ujenzi mwezi Oktoba, 2021. Kazi za ujenzi zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika ifikapo Julai, 2022.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nashon.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naipongeza Serikali kwa majibu mazuri, lakini ninalo swali moja la nyongeza. Ni lini Serikali itapeleka Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Kalya na ni lini itapeleka Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo pale Buhingu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nashon, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tutawaepeleka hawa watendaji ambako kuna upungufu katika maeneo yao kwenye kipindi cha bajeti hii ambayo kimsingi ndiyo tunayoijadili sasa. Kwa sababu tuna eneo ambalo tutapata watumishi wapya ambap tutazingatia maeneo ambayo hayana watumishi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mwaka 2021 niliomba Mahakama kwenye

Tarafa ya Ikuwo, Tarafa ambayo wananchi wake wanatembea zaidi ya kilomita 120 kwenda kufuata huduma Mahakama ya Mwanzo. Niliahidiwa kwamba nitapewa Mahakama, lakini tunaenda mwisho wa mwaka, hadi leo hatujajengewa Mahakama. Ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Mwanzo kwenye Tarafa ya Ikuwo ili iweze kuhudumia Kata ya Kigala na Mfumbi ili wananchi wao wasipoteze haki zao za Kimahakama ambazo wamekuwa wakizikosa kwa muda mrefu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kumjibu Mheshimiwa Sanga swali lake la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba ujenzi haujaanza na kama nilivyojibu jana swali la msingi, niliwaeleza juu ya mkakati wa mwaka mpya huu wa fedha ambao tunakwenda kuanza ujenzi wa sehemu kubwa sana wa zile Mahakama za Tarafa. Namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira kidogo katika kipindi hiki kinachofuata ambapo bajeti yake imeshaidhinishwa, tunaenda kuanzisha ujenzi ambao utakwenda kutibu kiu ya wananchi wetu hawa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Zaytun.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa sisi Mahakama ilijenga Mahakama ya Wilaya na imekamilika na Naibu Waziri wewe ndio ulikuja kuhimiza ukamilishwaji wa ujenzi huo: Je,

utakuwa tayari kushawishi Mahakama waje sasa kuifungua kwa mbwembwe zote? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge atararijie kwamba tunakwenda kuizindua, mbwembwe aziandae huko huko kwa wananchi wake wakati wa kufungua hii Mahakama, kwa sababu ni huduma ambayo kimsingi ni ya muhimu katika maeneo yale. Kwa hiyo, naomba watu wa Mahakama waweze kuweka utaratibu wa kwenda huko na ikiwapendeza zaidi wamwalike Mheshimiwa Waziri akaungane nao katika uzinduzi huo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mahakama ya Wilaya ya Meru ina majengo chakavu sana na hivyo kuzorotesha huduma za Kimahakama: Je, Serikali ina mkakati gani wa kukarabati wa majengo haya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zaytun, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokuwa nikijibu jana maswali yale ambayo yalihusisha masuala ya ukarabati, naomba niwaahidi Waheshimiwa Wabunge wote, majengo yote ya Mahakama ambayo yamechakaa, yametengewa fungu maalum na kwa kipindi hiki ambacho tunakwenda kuanza kuitumia bajeti ambayo mmeiidhinisha nyie wenyewe, kimsingi tunaenda kuanza ukarabati kwenye maeneo yote yale ambayo mpango kazi wake umeshakamilika. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Wilaya ya Kishapu haina Mahakama yenye hadhi na kwa bahati nzuri jitihada zimefanyika za kupata eneo kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama hiyo: Je, Serikali inaahidi nini kumaliza tatizo hili la Mahakama yenye hadhi katika Wilaya ya Kishapu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Butondo swali lake la lini Mahakama itakwenda kujengwa kwenye eneo lake?

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi tumeshaweka programu ya Mahakama zote za Wilaya ambazo katika mazingira ya kawaida mpaka kufikia 2025 tutakuwa tumekamilisha nchi nzima ujenzi wa Mahakama zetu. Sasa ni lini? Ninaomba tu Mheshimiwa baada ya majibu haya, kwa sababu programu hii ninayo, tuweze kumpitisha

kwenye eneo lini tunakwenda kuanza ujenzi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kwenye Mkoa wa Dar es Salaam eneo lililobakia kuwa na Mahakama ya Wilaya ni Jimbo la Kibamba ndani ya Wilaya ya Ubungo na eneo tayari tunalo: Je, Serikali mko tayari kujenga Mahakama pale ya Wilaya katika mwaka huu 2022/2023?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kumjibu Mheshimiwa Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari mpango wa kuanza ujenzi katika eneo alilolitaja umeshakamilika. Nami naomba baada ya hapa tuweze kuwasiliana ili tuone ni lini tunaanza mpango huu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, maswali yetu yamekwisha. Orodha ya wageni bado haijafika, lakini nina matangazo hapa.

Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge, kutakuwa na semina kwa ajili ya Wabunge Wanawake leo Ijumaa tarehe 17 Juni, saa 7.30 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Semina hiyo imeandaliwa na Mradi wa Kulijengea Uwezo Bunge *(LSP II)* ambapo mtoa

mada ataeleza masuala mbalimbali ya uongozi kwa wanawake na hasa kwenye kuingia kwenye Majimbo.

Waheshimiwa Wabunge, mnasisitizwa kuhudhuria semina hiyo muhimu. Mzee Mkuchika, mbona umeshtuka! *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania *(TIRA)* wapo katika viwanja vya Bunge nyuma ya jengo la Msekwa kuanzia tarehe 17 - 24 Juni, kwa ajili ya kutoa elimu ya Bima. Hivyo Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa kutembelea banda hilo ili kujifunza masuala mbalimbali yanayohusu bima. Pindi orodha ya wageni itakapokuja tutawatambulisha wageni wetu ambao wametembelea Bunge.

Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2022
### *(The Finance Bill, 2022)*

*(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa majadiliano yanaendelea. Tunaanza na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, jiandae Mheshimiwa Dkt. Chamuriho na Mheshimiwa Daniel Sillo. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla hayupo, Mheshimiwa Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho.

**MHE. ENG. DKT. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hoja hii ya Bajeti Kuu ya Taifa. Kwanza napenda kuunga mkono hoja ya bajeti hii ambayo ni bajeti ya wananchi iliyowasilishwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kutoa pongezi kwa Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea bajeti ya wananchi ambayo kwa kweli imekidhi mambo mengi. Kwanza imeongezeka kwa asilimia 8.1 ambayo inaashiria kwamba vitu vingi vimeongezeka, huduma nyingi zimeongezeka. Pili, amefuta ada na mambo mengine mazuri. Pia ni bajeti ambayo ina mambo mengi mazuri ambayo hata muda wa kuyaelezea unakuwa ni kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nitoe pongezi kwa Mawaziri wote, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na Manaibu Katibu Wakuu kwa kazi nzuri wanayofanya ya kumsaidia Mama kutuletea maendeleo katika nchi hii. Ukingaalia bajeti hii kama ilivyowasilishwa…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tumsikilize mtu anayechangia, kuna mada maalum. Naomba utulivu ndani ya Bunge.

**MHE. ENG. DKT. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia bajeti yetu ilivyopangwa na kuletwa, utekelezaji wake utahitaji mambo mawili makubwa, ambayo kwanza ni kuongeza mapato; na pili, ni kubana matumizi. Tunanipongeza bajeti hii kwani hayo yote mawili yamejitokeza mabaya na katika uwasilishaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026 ni kujenga uchumi shindani wa viwanda kwa maendeleo ya Taifa. Sasa mimi nitaelekeza mchango wangu katika viwanda vya vifaa vya ujenzi, wajenzi wenyewe yaani Wakandarasi na tatu, ni uhai wa matokeo yao ya ujenzi huo kwamba ni nini ambacho kinaendelea?

Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa vya ujenzi kutoka nje au vyenye kutumia bidhaa nyingi kutoka nje vimepanda sana. Kwa mfano, tukichukua mabati ya kuezekea, bei yake imepanda kidogo. Kwa hiyo, hapa katika bajeti hii, ushauri ambao tunaoutoa ni kwamba tutumie vifaa vingi vyenye asili ya hapa nyumbani ili tuweze kupunguza utegemezi mkubwa kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano ambao nitautoa hapa ni huo huo wa mabati kwamba kwa miaka ya nyuma tumekuwa tukiona majengo mengi ya Serikali yalikuwa yakiezekwa kwa vigae na kwa kweli yamekuwa yakidumu kwa muda mrefu; na huko nyuma tulikuwa vilevile na viwanda vya vigae. Ukiangalia vigae hivi vinahitaji vitu viwili tu, udongo ambao ni mwingi sana tunao hapa nchini, na vilevile kama ni malighafi ya kuchomea, tukiokoa misitu yetu tunaweza tukatumia hata gesi ili tuweze kuchoma vigae tuvipate kwa bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tukipunguza utegemezi wa vifaa ambavyo vinatengenezwa nje na tukaongeza vifaa ambavyo vinatengenezwa ndani ya nchi tutakuwa tumemsaidia sana Mama katika bajeti yake hii ya wananchi kwani tutakuwa tumepunguza utegemezi kutoka nje na vilevile tutakuwa tumepunguza utegemezi wa dhana ya *imported inflation* kwani bidhaa nyingi kutoka nje zinakuwa na mfumuko wa bei ambao hauko ndani ya uwezo wetu katika udhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili nitajielekeza kwa Wakandarasi. Tumekuwa na miradi mingi ambayo tunaitekeleza hapa nchini, lakini miradi hiyo mingi inatekelezwa na Wakandarasi kutoka nje. Hii inatokana na vigezo ambavyo vinawekwa katika tathmini kwamba uwezo, uzoefu na kadhalika; na katika hilo nashauri tuendelee kujenga uwezo wa makandarasi wetu wa ndani ili waweze kujenga hii miradi mikubwa. Tufanye juhudi za makusudi za kuwawezesha watendaji wa ndani hawa Wakandarasi ili waweze kutekeleza hii miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri ambao tunaipongeza Serikali kwa kuwa imefanya hilo, imeweza kuwakusanya Wakandarasi katika miradi minne ya majaribio ambayo imewajengea uwezo. Kuna daraja la Mbutu ambalo limejengwa na Wakandarasi wa ndani, wameungana Wakandarasi 10 ambao imewasaidia kujenga uwezo wa kutekeleza mradi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna barabara ya Dumila - Kilosa ambayo hadi sasa hivi inajengwa na ina mkusanyiko wa Makandarasi 10 ambao nao vilevile tunawajengea uwezo wa kujenga barabara hizo. Barabara ya Urambo - Kaliuwa nayo imejengwa na Wakandarasi wa ndani lakini kwa mkusanyiko huo huo wa kuwajengea uwezo; na vilevile kuna barabara ya Makutano - Sanzate.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa utaona kwamba tukiziendelea juhudi hizi ambazo tunawapa uwezo Wakandarasi wa ndani kuweza kujenga miradi mikubwa, tutapunguza sana gharama za matumizi au utegemezi wa makapuni ya nje ambayo yana bei kubwa, na hiyo itatusaidia kabisa katika kutekeleza bajeti hii ya wananchi ambayo Mama yetu mpendwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ametuletea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kumshauri Waziri wa Fedha na Mipango kwamba Sheria ya Ununuzi iko Wizarani kwake. Kwa hiyo, anaweza kabisa kufanya juhudi za makusudi za kuweza kulirekebisha hili au kujenga uwezo wa Makandarasi wetu kwa kuwatengea miradi ya mifano au miradi ya kuweza kuwajengea uwezo ili waweze kuendelea na kuhakikisha kwamba katika miradi mikubwa inayofuata au inayokuja tuwe na ushiriki mkubwa

zaidi wa Wakandarasi wetu wa ndani ili bei iweze kupungua na vilevile na fedha nyingi zaidi iweze kubaki hapa kwetu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa tatu, napenda kuelekeza katika matokeo ya ujenzi huu ambao unafanywa. Mama yetu ametoa fedha nyingi sana kwa ajili ya ujenzi wa miradi mingi; zahanati, hospitali, barabara, na kadhalika. Sasa tunajiuliza; je, katika fedha hizo ambazo zimetengwa, miradi hiyo uhai wake utakuwaje? Kwa hiyo, hapo tunatoa tena ushauri kwamba ili tuweze kuwa na matumizi mazuri zaidi ya fedha zetu na kuhakikisha kwamba fedha hii ambayo inatolewa na Mama inatupa *value for money,* basi tutumie vifaa bora ambavyo vitaakisi matokeo ya kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa ndiyo kuna changamoto kwa sababu vifaa bora vinakuwa na bei kubwa kidogo kuliko vifaa duni, lakini ukiangalia uhai wa vile vifaa unakuta kwamba ni tofauti sana. Sasa katika bajeti yako tumeona kwamba Mkaguzi Mkuu wa Serikali *(CAG)* ameongezewa bajeti na hii inampa uwezo wa kukagua zaidi, basi huyu *CAG* naye ajengewe uwezo wa kuhakikisha kwamba anapata uwezo wa kutathmini *life cycle cost* ya mradi mzima. Tusipotoshwe na bei ndogo ya mwanzo ambayo unakuta kwamba mradi huo ukikamilika unaweza kuwa una maisha mafupi zaidi kuliko kutumia vifaa bora zaidi ambavyo vitakuwa na maisha marefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ukikamilisha jengo lako ambalo litakaa miaka miwili halafu linakuwa limekwisha kwa gharama nafuu, lakini ukitumia vifaa bora

ambavyo utaweza kupata jengo hilohilo kwa gharama kubwa kidogo lakini likakaa miaka mingi zaidi, utakuta kwamba ukifanya tathmini kwa *life cycle cost* utakuta ni kwamba ni bora utumie vifaa bora lakini upate kitu kizuri kitakachodumu miaka mingi kuliko kuwa unafanya marekebisho na matengenezo kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili linahitaji tujengeane uwezo kidogo kwani inatia hamasa sana kuchukua vifaa vya bei nafuu ambavyo vina uhai mfupi, badala ya vifaa vya kudumu muda mrefu. Wote ni mashahidi kwamba katika majumba yetu huko unaweza ukanunua bomba la bei nafuu la Shilingi Elfu Tano, lakini kila baada ya miezi miwili au mitatu unalibadilisha, ukinunua bomba la 15,000 ungekuta bomba linakaa miaka mitatu, ukijumlilsha utaona kwamba ni heri ununue kile ambacho kinadumu kuliko kununua kile kitu ambacho ni rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa Wizara hii kuleta bajeti ambayo imeakisi hayo matakwa na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sillo Mwenyekiti wetu wa bajeti na Mheshimiwa Mafuwe ajiandae.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye Bajeti hii Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, bajeti hii ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Shilingi Trilioni 41.48 kwa mwaka

huu wa fedha 2022/2023 inaleta matumaini makubwa sana, italeta mapinduzi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa maono haya makubwa ya kuwaletea Watanzania bajeti inayoleta matumaini makubwa. Nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri wetu wa Fedha na Mipango, Naibu Waziri na timu nzima kwa kazi nzuri wanayofanya pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara hii kwa kusimamia sana sera za kifedha na za kiuchumi, pamoja na changamoto ya mfumuko mkubwa wa bei hapa duniani, kwa kweli kwa nchi yetu mfumuko wa bei upo katika wigo wa Afrika Mashariki, kwa hiyo wanafanya kazi kubwa wenzetu hawa tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii ukiangalia imejielekeza sana kwenye sera za uzalishaji. Kwa mfano, Wizara ya Kilimo tumetenga bajeti kuanzia Bilioni 294 mwaka 2021/2022 hadi Bilioni 954 kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ni hatua kubwa sana tuwapongeze sana wenzetu upande wa Serikali. Wizara ya Uvuvi na Mifugo bajeti imetoka Bilioni 168 kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 hadi Bilioni 268 ongezeko la Bilioni 100 ni hatua kubwa sana na hii sekta muhimu sana katika nchi yetu. Hatua mbalimbali za kikodi zilizopendekezwa pia zinaonekana kabisa kupanua wigo wa walipa kodi na kupunguza mzigo kwa walipa kodi wachache hapa nchini. Ili kufikia makusanyo haya tunayotarajia Bilioni 41.48 naomba nishauri katika maeneo yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ni mifumo ya ukusanyaji mapato iliyoko chini ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*, eneo la pili nielekeza kwenye *coordination*

ndani ya Serikali katika utekelezaji wa miradi mbalimbali. Dunia ya leo ni dunia ya TEHAMA na Tanzania siyo kisiwa lazima tukubaliane uhalisia kwamba sasa mawasiliano na biashara zote ziko kwenye TEHAMA. TEHEMA imerahisisha maeneo mbalimbali kwenye ulipaji na ukadiliaji wa kodi ni lazima tuelekeze kwa kutumia mifumo, ili kutokupoteza makusanyo katika nchi yetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika*, TRA* ina mifumo ya *high tax* ambayo iko ndani ya kodi za ndani, kuna mfumo wa *TANCIS* ambao upo Idara ya Forodha na Ushuru wa Bidhaa, lakini kuna *e-filing* ambayo inatumika kwenye kodi la ongezeko la thamani *(VAT)*. Changamoto iliyopo kwenye mifumo hii yote ni kwamba haisomani, ndani ya taasisi moja muhimu ya kukusanya mapato ya nchi mifumo haisomani, kwa hiyo niombe sana Wizara ya Fedha na Mipango kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania ili mifumo yote iweze kusomana kusiwe na mwanya wa kupoteza mapato ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mifumo ni muhimu sana ikasomana ili endane na wakati, lakini manufaa ya mifumo bora inayosomana ni kama ifuatayo:-

Moja ni kupunguza muingiliano baina ya Maafisa wa Kodi, na Wafanyabiashara na hivyo kupunguza mianya ya rushwa katika nchi yetu. Faida ya pili ni kupunguza mapingamizi ya kodi yanayotokana na ukadiliaji tukiwa na mifumo bora hata *assessment* zinatoka kwa ubora kwa hiyo utapunguza mapingamizi ya kodi kwenye Bodi za Rufaa pamoja na Mahakama za Rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni kurahisisha ulipaji wa kodi, kwa hiyo tukiwa na mifumo bora inayosomana itarahisisha ulipaji wa kodi na kupunguza usumbufu wa Watanzania na Wafanyabiashara, wetu kwa hiyo kuna haja kubwa sana ya mifumo hii kuwezeshwa ili makusanyo yetu yakusanywe kwa manufaa makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunganishe hili na Idara ya Forodha na Ushuru, Idara ya Forodha na Ushuru wa Bidhaa inachangia zaidi asilimia 40 ya mapato yote ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*, lakini changamoto kubwa iliyoko kwenye idara hii sasa ni kukosekana kwa *Cargo Scanners.* Kamati ya Bajeti ilifanya na ziara katika mpaka wa Namanga tumekuta hakuna *Cargo Scanners* lakini ukienda Tunduma, Holili, Sirari kwenye eneo hili tumepoteza mapato makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipata hii bila kuwa na *Cargo Scanners* ni vigumu kutambua bidhaa gani zinaingia nchini kwa hivyo kutokupata makadirio sahihi ya kodi katika maeneo haya. Kwa hiyo niombe sana upande wa Serikali wawekeze kununua *Cargo Scanners* kwa mikakati mikubwa ili tuweze kuboresha makusanyo ya kodi katika Taifa letu. Tunalenga kupata hiyo bilioni 41 bila kuwa na mifumo sahihi itakuwa ni ngumu sana kufikia malengo haya. Kwa hiyo niombe sana wizara iweze kufanya nguvu kubwa ili tuweze kukusanya makusanyo makubwa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni uratibu wa bajeti za Wizara, tunapanga mipango mizuri sana na bajeti nzuri sana, lakini bila kuwa na Wizara zetu kusomana itakuwa ni vigumu sana katika kuteleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika Taifa yetu. Kwa mfano, Wizara ya

Kilimo kwa mfano inapoandaa miradi mbalimbali ya umwagiliaji na kadhalika je inahusisha Wizara ya Ujenzi ambayo itahusika na ujenzi wa barabara kufikia maeneo haya ya uzalishaji, je, inahusisha Wizara ya Nishati, inayohusika na miundombinu ya umeme? Kwa hiyo, tunapoandaa mipango na bajeti yetu ni muhimu sana kukawa na *coordination* baina ya Wizara zetu ili kuweza kuweka tija na kuweza kutekeleza miradi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili bila *coordination* ama tunachelewa au tunakwamisha kutekeleza miradi mbalimbali ya wananchi wetu kwa hiyo niombe sana wenzetu upande wa Serikali kuwe na *coordination* ili tuweze kutekeleza bajeti zetu kwa pamoja. Tunapokosa *coordination* baina ya Wizara idara na Taasisi inacheleweshа miradi lakini tungekuwa tunawasiliana tungepunguza gharama na pia tungerahisisha utekekelezaji wa miradi mbalimbali na kuwa na tija katika Taifa letu, kuna umuhimu mkubwa sana wa *coordination* ndani ya Serikali ili mambo haya yaweze kufanyika kwa wakati na kwa manufaa makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya nashukuru sana kwa fursa, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, orodha ya wageni imekuja, kwa vile tuna wageni wengi inabidi tuwatambulishe hawa ili nafasi ipatikane na wengine waingie. Wageni walioko kwenye jukwaa la Spika, wageni 17 wa Bunge ambao ni wanachama wa kikundi cha akina mama kiitwacho upendo kinachotoka Wilaya ya Ubungo - Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Violet Mlimbila

Mwenyekiti wa kikundi, Ndugu Selela Mwangwale Mwenyekiti Msaidizi, Elima Luhende Mhazini Monica Sebo Mhazini Msaidizi, Stela Swai Katibu na Neema Swela Katibu Msaidizi, Ndugu Angel Nsubi Bukuku mbunifu wa mitindo na mshonaji wa nguo za watoto na akina mama, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Bunge ambao ni Mheshimiwa Omari Mgumba Mkuu wa Mkoa wa Songwe karibu sana, ahsanteni. Mheshimiwa Anna Gidarya Mkuu wa Wilaya ya Ileje,na Mheshimiwa Cosmas Nshenye Mkuu wa Wilaya ya Mbozi. *(Makofi)*

Wapo pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge waliotembelea Bunge wasimame kwa Pamoja, wageni wote wa Waheshimiwa Wabunge simameni kwa pamoja tafadhali, ahsanteni karibuni sana. Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo wanafunzi 59 na Walimu toka Shule ya Msingi Nalopa iliyoko Jijini Arusha karibuni. Pia wapo wanafunzi 136 na Walimu Saba kutoka Shule ya Sekondari ya Kiislam Ihsan ya Jiji Dar es Salaam, karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Nilishamuita Mheshimiwa Mafuwe jiandae Mheshimiwa Kandege, jiandae Mheshimiwa Neema.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba ya bajeti iliyoko mbele yetu. Kwanza, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya na uzima, lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anazozifanya ndani ya nchi yetu, pamoja na viongozi wote

wanaomsaidia Mheshimiwa Rais, kuanzia Makamu wa Rais mpaka Mwenyekiti wa Kitongoji kwa sababu wote wanafanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana wananchi wa Tanzania ambao ndiyo walipakodi niwaombe waendelee na moyo huohuo. Ninampongeza pia Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na hasa wananchi wa Hai wamenituma niwashukuru kwa jambo zuri walililoratibu la kuweza kupata Milioni 400 pale kwenye Kituo chetu cha Afya Kisiki wanasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nipongeze hotuba hii kwa kweli imekuja na mambo ambayo yanagusa wananchi, moja ya eneo ambalo linagusa mwananchi moja kwa moja ni kuondoa ada kwa Kidato cha Tano na cha Sita tunashukuru sana. Pia kubadilisha utaratibu ule wa manunuzi ambao mfuko wa simenti ukiitwa wa Serikali bei yake inapanda saa hiyohiyo, kwa hiyo jambo hili linaenda kunusuru fedha nyingi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ule utaratibu wa magari mliouleta na lenyewe ni jambo lenye tija sana ninawapongeza. Mimi nitangulie kutanguliza maombi kadhaa kabla ya kuingia kwenye mchango wangu, mimi niombe Mheshimiwa Waziri mkatazame namna ya kupata fedha kwenye *remittance* wale Watanzania wanaofanya kazi na wanaishi nje ya nchi ya Tanzania, ni namna gani tunaweza kupata pesa kwao. Wenzetu wa Bangladesh asilimia 12 ya Pato lao la Taifa wanapata kutoka kwenye *remittance,* mimi niombe mkakae na wataalam muone namna ambavyo tunaweza tukapata fedha hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la pili mmeweka fedha kwenye mazao mengine ya ruzuku, zao la kahawa mkaacha! Zao la kahawa hili linatuletea fedha nyingi za kigeni niombe Mheshimiwa Waziri utakapokuja kuhitimisha hapa nenda kaa na wataalam wako uone namna ya kuongeza zao la kahawa na lenyewe liweze kupata ruzuku. Pia niombe nimekuwa nikisema mara kadhaa, sasa hivi huku mbele nitachangia kuhusu Wizara ya Kilimo. Tumeweka fedha nyingi pale na tunataka kuongeza thamani mazao yetu lakini mazao haya wateja wetu wako nje ya nchi na mazao ya mbogamboga usafiri wake mzuri ni usafiri wa ndege, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri unikubalie kwamba kiwanja cha ndege cha Kilimanjaro, ndege zile za mizigo tu zitue maegesho yawe bure na kutua ndenge kuwe bure ili tuweze kuvutia ndege nyingi za mizigo zije pale zichukuwe mazao yetu haya ambayo tumeweka fedha nyingi yaweze kupata wateja nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ni ombi ofisi ya *ombudsman* tuliosema ambao ni msuluhisho wa masuala ya kikodi, tuombe Tarehe Moja ianze na siyo lazima ianze na watumishi wote, mnaweza kuanza na watumishi wachache ili mradi tu waweze kuanza na mkisema muanze kuhangaika ofisi hapo Chuo Kikuu cha *UDOM* kuna maofisi wapelekeni hapo waanze kazi mara moja ili kuondoa adha kwa wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kuhusu Wizara ya Kilimo, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kusikia maoni yetu Wabunge, kutoka kwenye Bilioni 294 hadi Milioni 954 haya ni mapinduzi makubwa sana kwenye Bajeti ya Kilimo. Tafsiri yake ni kwamba tunaenda kuongeza pato la

Taifa, kwa sababu *formula* ni kwamba unapoongeza uzalishaji maana yake Pato la Taifa letu linaenda kukua. Ninamuomba Mheshimiwa Waziri fanya ufanyavyo fedha hizi zije kama zilivyo, kwa sababu kama tutapanga hapa halafu hazitakuja tutakuja kualaumu Wizara ya Kilimo kumbe hakupeleka fedha. Ili kusudi tuhakikishe kwamba tunaenda kupata mbegu ya Kitanzania, wataalam wetu hapa Tanzania kwenye taasisi inayoshughulika na mbegu wafanye utafiti tupate mbegu za kwetu ambazo ni rafiki na ikumbukwe Mheshimiwa Waziri hii ni biashara shindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unapoenda kuchukuwa mbegu huko hatukatai ni vizuri ni majirani zetu lakini tuko kwenye ushindani wa kibiashara, tuhakikishe fedha inayotengwa kwa ajili ya utafiti wa mbegu inakwenda kwa wakati, kwa sababu mbegu ndio kitu cha kwanza kinachotangulia. Fedha zilizopangwa kwa ajili ya skimu ziende ili mwisho wa siku tuweze kufanya kilimo biashara lakini chenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine zuri Wizara ya Kilimo imetenga fedha kwa ajili ya kutengeneza vile viwanda vya kuongeza thamani ya mazao *common use facility*, niombe hizi fedha ziende mara moja ili zikajengwe bahati nzuri na sisi Hai ni wanufaika kitajengwa pale Hai. Tuweze kujenga wakulima wetu waende wafungashe mazao yao, wauze yakiwa yameongezwa thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine tumekuwa tukipewa taarifa hapa kwamba nchi yetu ina dalili ya kupata mafuta lakini tayari tumekwisha kupata gesi, nimezungumza na wataalam wakasema tunahitaji Bilioni 40

kufanya utafiti kisima kimoja, hivi kwa nini tusifunge mkanda tukaamua sasa tutenge fedha za kutosha tufanya utafiti tuangaike na haya mafuta kwa sababu tuna uhakika tukiyapata tutainua uchumi wetu na tutaondokana na matatizo makubwa kama ambayo yametukumba hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mungu ametujalia na dalili zinaonekana mimi niombe sana Mheshimiwa Waziri inawezekana sio bajeti hii pale utakapopata pesa nyingine, nje ya bajeti tunayoipitisha hapa, kipaumbele kiwe ni namna gani tunaweza kufanya utafiti, tuwe na mafuta yetu, tuwe na gesi yakujitosheleza ya kwetu itatusaidia sana. Pia sambamba na hilo nchi hii imejaliwa madini mengi, mimi niombe namna ambavyo tunaendesha biashara hii ya madini bado haijawa yenye tija ya kutosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tuna shida gani ya kuchagua Mikoa Mitatu au Minne tukasema Mkoa wa Mbeya, Geita, Mikoa inayofanana na hiyo yenye madini mengi, tukaenda kufanya tathmini *geological survey* tukapata ripoti ya madini tuliyonalo tukauza leseni ambazo zimefanyiwa utafiti kuliko hivi sasa hivi tunauza leseni ambazo hazijafanyiwa utafiti ninajua ni gharama kubwa lakini sisi tu-*invest* pale hela ile itarudi ukizua leseni ambayo imefanyiwa utafiti utapata fedha ya haraka halafu ambayo haina *risk* yeyote lakini tuwe tumefanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niombe nimekuwa nikisema Mheshimiwa Waziri wewe ni mtaalam wa uchumi nchi hii tuna shida gani ya kutengeneza *National agenda* za kwetu tuwe na mipango ya miaka 100? nchi hii imejaa

wachumi wengi wako Vyuo Vikuu, na nitumie nafasi hii kuwaomba Wachumi nchi hii waje na andiko la kutusaidia ni namna gani tunaweza tukawa na mipango yetu ya miaka 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunayo maono nakubali ya miaka 20, lakini tunayo maono ya miaka mitano, mwaka mmoja mmoja lakini tutoke hapo ili kuweka nguzo ya uhakika tunaposema Serikali yetu tunataka tuimarishe kilimo basi tuweke mipango ya muda mrefu ambayo itafungwa kisheria, yeyote atakayekuwa Kiongozi wetu atasimamia mipango hii bila kuipindisha. Mheshimiwa Waziri naomba kipindi chako wewe ni Mchumi hebu anzisha jambo hili ili tuone litafikia wapi, watakuja wengine watakuja wataendelea ulipoishia wewe lakini usikubali kuondoka kwenye Wizara hii sasa hivi bila kuacha mpango huu umekaa vizuri. Nchi hii iwe na mipango ya muda mrefu miaka 100 na tufanye mabadiliko ya sheria jambo hili linawezekana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niseme kuhusu watumishi ambao tumesema hapa, kwamba watumishi wale ambao wako kwenye uteuzi, wakitoka kwenye teuzi zao warudi kwenye utumishi wa umma wa kawaida. Nashauri kwa kuwa mtumishi huyu atakuwa ameondoka kwenye utumishi wake wa umma wa kawaida akaenda kwenye uteuzi kuna miaka ambayo hakupanda madaraja, anaporudi basi apewe kwanza promosheni zake kwa kipindi kile ambacho alikuwa nje ya utumishi halafu ndiyo abaki pale, kuliko kumrudisha huku amefanya kazi labda alikuwa Afisa Utumishi akateuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya amekuwa Mkuu wa Wilaya kwa miaka ishirini au miaka kumi akirudi akaanzie tena daraja la pili, hii siyo

sawa. Apandishwe promosheni zake kwanza, halafu ndiyo ambapo anaweza kubaki kwenye cheo chake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine niombe sana, kule Hai walifanya tathmini muda mrefu sana ya Daraja lile la Kikafu ambalo ni Barabara ya Moshi – Arusha, wananchi wamesimama muda mrefu hawajalipwa fidia zao na nimepita kwenye hotuba ya Waziri, sijaona mahali ameweka. Nimwombe Mheshimiwa Waziri atafute fedha hii na bahati nzuri mradi ule ni wa wadau, atafute fedha hii alipe wananchi wale fidia na lile Daraja la Kikafu liweze kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe jambo lingine, Chuo chetu cha *SUA* tafadhalini sana. wamezungumza Wabunge hapa, ifike mahali Mheshimiwa Waziri apokee maoni yetu, Chuo cha SUA kiwe Chuo cha Kilimo kweli kweli, wawapelekee fedha wafanye kazi yao…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mafuwe, kengele ya pili hiyo

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naomba kuunga hoja mkono. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kandege ana dharura, Mheshimiwa Neema, ajiandae Mheshimiwa Cherehani. Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa hii ya kuchangia kwenye Bajeti Kuu ya Serikali. Napenda kuanza kwa kuipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea bajeti ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti Kuu ya Serikali napenda kuchangia katika maeneo manne ambayo yaligusiwa katika hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali. Eneo la kwanza ni matumizi ya TEHAMA na *internet*. Naipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa matumizi ya TEHAMA na *internet* katika utekelezaji wa kazi zake na uamuzi huu utapelekea kuongeza chachu katika kufikisha huduma ya TEHAMA na *internet* katika maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tufanikishe hilo kwa uharaka, napenda kurejea ushauri niliotoa wakati nachangia kwenye bajeti ya Wizara inayosimamia masuala ya TEHAMA kwamba wakati umefika sasa Serikali itambue *community networks* kama njia mbadala ya kufikisha huduma ya *internet* kwenye maeneo ambayo bado hayajaunganishwa. Katika hili nina habari njema, wiki iliyopita katika Mkutano Mkuu wa Maendeleo ya Mawasiliano Duniani uliofanyika Kigali na nashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri Nape Nnauye alikuwepo kwenye mkutano ule, Nchi zote Wanachama wamepitisha Azimio namba 37 ambalo limetambua *community networks* kama njia mbadala ya kufikisha haraka huduma ya TEHAMA na *internet* kwenye maeneo ambayo bado hayajaunganishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kusisitiza kwa Serikali, ili tutimize dhamira hii ya Serikali ya kutumia

TEHAMA na teknolojia katika maeneo yote ikiwemo maeneo ya pembezoni, basi wakati umefika pia na Tanzania tutambue rasmi *community networks* kama njia mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo langu la pili, napenda kuishukuru Serikali kwa kuamua kuanzisha dirisha maalum la kuhudumia watoto wanaotoka kwenye kaya maskini katika Mfuko wa Maendeleo wa *TASAF*. Hapa narejea wakati nachangia katika bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, nilipendekeza kwamba Serikali ione namna gani ya kutumia Mfuko huu wa TASAF kuwezesha watoto wa kike wanaotoka kwenye kaya maskini wapate msaada wa taulo za kike ili wasiendelee kukosa shule kwa sababu ya kuwa kwenye hedhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu Nchemba wakati akihutubia, alisema kwamba dirisha hili jipya kwa ajili ya watoto wanaotoka kwenye kaya maskini litatumika kuwawezesha watoto wanaotoka kwenye kaya maskini kupata mahitaji maalum. Hivyo ningeomba kwa unyenyekevu mkubwa wakati Mheshimiwa Waziri anakuja kuhitimisha hoja yake atuainishie bayana haya mahitaji maalum ni yapi na naendelea kusisitiza katika hayo mahitaji maalum ni muhimu sana suala la msaada wa taulo za kike kwa watoto wa kike wanaotoka kwenye kaya maskini lijumuishe ili mtoto wa kike asiendelee kukosa shule kwa sababu ya kuwa kwenye hedhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo langu la tatu, naishukuru sana Serikali kwa kupendekeza maboresho kwenye Sheria ya 148 ili kuwezesha Serikali kukusanya kodi za biashara za mtandao (*online businesses*) pamoja na

*digital services.* Suala hili nilishauri hapa Bungeni mwaka jana na hii inadhihirisha kabisa kwamba kwa hakika Serikali ya Chama Cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ni Serikali iliyo sikivu na inaendelea kutupa moyo sisi Wabunge kuendelea kuishauri Serikali kwa ari na nguvu ili kuhakikisha kwamba tunachangia maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Serikali iweze kukusanya kodi ipasavyo, lazima pia tufanye maboresho kwenye Sheria ya *VAT* ili *TRA* waweze kutoza kodi makampuni ambayo yamesajiliwa nje ya nchi. Nitatoa mfano mdogo, *DSTV* wanatoa huduma hapa Tanzania, lakini hapa Nhini Tanzania kuna *agent,* pesa zote tunazolipa katika kuangalia DSTV zinalipwa Afrika Kusini na kanzidata ya wateja wa *DSTV* ipo Afrika Kusin. Kwa mantiki hiyo ni ngumu kwa Serikali yetu kupitia *TRA* kupata uhakika *DSTV* ina wateja wangapi hivyo kujua inatakiwa ilipwe *VAT* ya kiasi gani. Kwa hiyo pamoja na kwamba tunaenda kufanya maboresho ya hii Sheria 148 ni lazima Serikali ifanye haraka kuleta ile sheria ya *data protection* ili ndani ya ile sheria iwe ni lazima kwa kampuni hizi za kibiashara kutoa taarifa zao za wateja (*sharing of debtor*), kati ya hizi biashara na Serikali ili tuweze kupata uhakika maana zile data ni data za Watanzania iweje ziwe nje ya nchi na sisi ndani ya nchi tusiwe na *access* nazo. Kwa hiyo Sheria ya *Data Protection* ije ili tuweze kuhakikisha kwamba, kunakuwa hakuna mianya yoyote ya ukwepaji wa kodi katika biashara ambazo aidha zinafanywa *online business* ama zinatoa *digital services* au zinatoa huduma kwa kutumia *satellite*.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo langu la nne, naipongeza sana Serikali kwa uamuzi wa kwamba kila mtu

kuanzia umri wa miaka 18 apate usajili wa *TIN,* kwa sababu usajili huu wa *TIN* utawawezesha vijana wetu kujiajiri ikiwemo na kupata leseni za udereva. Hata hivyo, natambua pia moja ya lengo la kufanya hivi ni kuongeza wigo wa walipakodi kwa maana ya kwamba kuanzia vijana wa miaka 18 watakapofikisha kipato kile ambacho kinaweza kutozwa kodi, basi wataweza kulipia kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwa unyenyekevu kabisa na kwa kutambua kwamba tunayo changamoto ya ajira kwa vijana, naomba kupendekeza kwa Serikali itoe msamaha wa kodi kwa biashara mpya zitakazoanzishwa au biashara zitakazorasimishwa za vijana kati labda umri wa miaka 18 mpaka 30 ili vijana ambao wamemaliza shule wanahitimu vyuo vya kati, wanahitimu Vyuo Vikuu waweze kujiajiri. Jambo hili linawezekana, Serikali inaweza ikatoa msamaha wa kodi kwa vijana walau kwa miaka mitatu ili itoe hamasa kwa vijana hawa kuanzisha biashara zao na kurasimisha. Naamini jambo hili linawezekana kwa sababu ikiwa Serikali inatoa misamaha ya kodi kwa wawekezaji kwa nini ishindwe kutoa misamaha ya kodi kwa vijana wetu wa Kitanzania ambayo itakuwa ni chachu ya wao kujiajiri, lakini vivyo hivyo itakuwa ni njia ya kupelekea kuongeza wigo wa walipakodi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha, naomba kwa unyenyekevu mkubwa sana nirejee suala la umuhimu wa Serikali kuweka msamaha wa kodi ya *VAT* kwenye *pump* za maji zinazotumia nishati ya jua (*solar water pumps*). Wakati Serikali inaendelea kupeleka jitihada ya kufikisha maji vijijini, inaendelea kufanya jitihada ya kufikisha umeme vijijini, ni muhimu sana kwa Serikali kuweka mazingira ambayo yatarahisisha upatikanaji wa maji, hivyo

kufanikisha dhamira ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ya kuwatua akinamama ndoo kichwani. Vivyo hivyo suala hili la *solar water pump* pia lina mchango mkubwa sana katika sekta ya kilimo kwa maana ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku ya tarehe 9 mwezi Juni mwaka huu 2022 katika ziara ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan mkoani Kagera katika mkutano wa kati yake na wananchi wa Bukoba mjini na Mkoa wa Kagera kwa ujumla niliwasilisha ombi kwake Mheshimiwa Rais la kuona namna gani ambavyo Serikali itaweka msamaha wa kodi kwenye hizi *solar water pumps.* Wakati anahutubia Mheshimiwa Rais alifanya rejea kwenye suala hili la *VAT* kwenye *solar pumps.* Mimi binafsi naamini kitendo cha Mheshimiwa Rais kufanya rejea kwenye suala la *VAT* kwenye *solar pumps* ni kiashiria tosha kwamba Serikali lazima iangalie jambo hili kwa jicho la kipekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri Dkt Mwigulu Nchemba atakapokuja kuhitimisha hoja yake, lakini pia katika Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2022/2023, jambo hili la msamaha wa kodi kwenye *solar pumps* ni jambo ambalo linahitaji liwekewe uzito. Natarajia kwamba ni jambo ambalo litakuwemo na Serikali italichukua kwa uzito wake ili kuhakikisha kwamba tunawatua akinamama ndoo kichwani, lakini pia tunahamasisha kilimo cha umwagiliaji ambacho ndiyo sera ya Serikali hii ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Cherehani, jiandae Mheshimiwa Edward Ole Keita Kisau.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai na kuweza kuendelea kutusimamia na kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais. Pia nikushukuru sana wewe binafsi kwa jinsi ambavyo unaendesha Bunge kwa hekima kwa busara. Nimshukuru sana vile vile Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa bajeti kubwa ambayo amevunja rekodi kati ya Marais wote waliowahi kuitawala nchi yetu, bajeti yake imejikita sana kuwasaidia wananchi wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kusamehe kodi kwa wafanyabiashara ambao sasa wamepewa wigo mpana wa kuendelea kufanya shughuli zao na kuwahudumia wananchi wetu. Kipekee sana nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Naibu wake, niseme kwamba amevunja rekodi hasa kwenye suala la kubana matumizi ya magari na amevunja rekodi kusimamia haya magari. Kwenye hotuba yake kama alivyosema ni kweli unakuta gari nyingi zinazunguka barabarani wakati mabosi wao wamepanda ndege kwenda Dar es Salaam, wamepanda ndege kutoka Dar es Salaam kwenda Bukoba, wamepanda ndege kutoka Bukoba kuja Dodoma, halafu magari sasa yanawafuata kule gharama zake zinakuwa kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hili, ningeomba sasa fedha hizi

ambazo wanaenda kuziokoa, Mheshimiwa Waziri zielekezwe mahospitalini, zielekezwe kuwahudumia akinamama hospitalini. Fedha hizi zikienda hospitalini zitawasaidia sana akinamama wanaoenda kujifungua. Bado akinamama wanaambiwa kwenda na *gloves* hospitalini, bado akinamama wanaambiwa kwenda kununua dawa zingine, hatujajua na naomba hili niweze kulisema hapa hadharani, akinamama wanapoenda hospitalini wanaandikiwa vitu vingi vya kwenda navyo, sasa tunataka tujue ni vitu gani akinamama wanatakiwa aende navyo, akinamama hao hospitalini wanahangaika sana, akinamama hao hospitalini wanateseka sana.  Pia watoto wadogo hopitalini wanapoenda wanateseka sana na kunakuwa na changamoto moja ambayo tunakutana nayo sisi hasa kwenye majimbo ya vijijini ni gharama gani ambapo mama anatakiwa afanye *operation* ni kiasi gani anatakiwa alipe.  Kwa sababu katika maeneo mengi unakuta akinamama wanapofanyiwa *operation* gharama zinakuwa kubwa, wengine wanafanyiwa *operation* mpaka kwa 150,000, wengine *operation* mpaka kwa 400,000, wengine anafanyiwa *operation* mpaka kwa 500,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *issue* ambayo naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha aiangalie vizuri, anafika mama hospitalini anaambiwa apumzike mpaka mfumo ukae sawa, mfumo umegoma, daktari ana-*chat* na simu, *nurse* ana-*chat* na simu, eti kwanza mfumo umegoma, sasa tujiulize ndugu zangu Wabunge tuko hapa, hivi uchungu unasubiri mfumo? Tuambizane hivi mtoto anapotaka kuzaliwa anasubiri mfumo? Ningeomba suala hili Mheshimiwa Waziri aliangalie, akinamama wanateseka, akinamama wanapewa rufaa kwenye hospitali zetu, kwenye zahanati zetu, wanaenda kwenye hospitali za

rufaa, kwenye vituo vya afya, mtu anapopewa rufaa hali yake siyo nzuri, anafika pale anaambiwa mfumo haujakaa vizuri. Niombe, akinamama wanapoteza maisha katika hili suala la mfumo, tunaomba tuliangalie, anapofika mama kwa udharura wake ashughulikiwe kwanza wakati mfumo wao wanauandaa badala ya kuambiwa kaa hapo mfumo haujakaa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waziri wa Fedha, Dkt. Gwajima alitangaza suala hili kwamba vifo vinavyotokana na akinamama wajawazito na watoto lazima wajiridhishe Wizara ya Afya, lakini cha ajabu maneno haya yanaishia kwenye mtandao tu, hakuna anayeshuka chini kwenda kulifuatilia hili. Naomba hili suala lifanyiwe kazi hasa katika majimbo ya vijijini, ni changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia juzi kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ameondoa tozo kwenye vifungashio vya pamba, akaondoa tozo kwenye vifungashio vya korosho, lakini hajaondoa tozo kabisa kwenye vifungashio vya zao la tumbaku, zao ambalo linaingiza fedha nyingi za kigeni hapa nchini. Mwaka huu tu zao la tumbaku pekee fedha ambazo zinakopwa benki ni zaidi ya dola milioni 86 ambazo zinaenda kuwahudumia wakulima na Mheshimiwa Rais ameweka ruzuku, lakini kuna tozo ambazo ziko kwenye vifungashio hasa magunia, kuna asilimia 35 ambayo ni ya *import duty,* ni gharama kubwa sana kwenye magunia haya ambayo wakulima wanaenda kutumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna *VAT* 18%, ukiipiga kwa magunia tu kwa bei ya dola 720 kwa pensheni *cross* inaingia kwenye dola 1146.96 kabla ya gharama za

usafirishaji bado gharama za bandarini ukijumlisha gharama yake na gunia inakuwa na bei kubwa sana, lakini magunia haya yanaenda kutumiwa na wakulima wetu, magunia haya wanaenda kufungia tumbaku wakulima wetu na ndiyo wanazitumia wakulima wetu kuvunia tumbaku na mwisho wa siku tumbaku hii ndiyo inayoingiza fedha nyingi za kigeni.

Mimi ningeomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha hili suala la upande wa *import duty* kwenye magunia yetu vifungashio vya tumbaku viweze kupunguzwa viweze kuondolewa ili wakulima sasa tuwape *favour* ya kuongeza bei waweze kuona faida kwenye zao la tumbaku. Vile vile kuna tozo ya mionzi, tozo ya mionzi ni 0.2 kwa kilo kwa kila tumbaku inayosafirishwa nje ya nchi, lakini hawa watu mbaya zaidi hawako bandarini ofisi yao iko Arusha, ina maana mtu anaposafirisha tumbaku mpaka wapigiwe simu kutoka Arusha waende Dar es Salaam kutoa kibali, sasa inachelewesha usafirishaji na gharama yake inakuwa kubwa kinachofanyika sasa wanunuzi wanapunguza bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimwombe na nimshauri Mheshimiwa Waziri, tuangalie cha kufanya, tukiondoa hii kodi ya mionzi, tukaamua kuwekeza kwenye mjengeko wa bei, kwanza tukiondoa wanunuzi wataongeza bei, tumbaku yetu inanunuliwa wastani wa dola moja mpaka dola 1.6, lakini wenzetu Nchi za Malawi, Zimbabwe na washindani wetu Zambia, bei yao sasa iko kwenye dola tatu, dola tano mpaka dola nane kwa sababu kodi hizi nyingi wameziondoa. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kodi hizi aziondoe, halafu aziweke kwenye mjengeko wa bei. Mfano tu kama uzalishaji tukaenda tani 60 mpaka tani 200, tukiweka dola mbili tu kwenye kila kilo, tuna uwezo wa

kukusanya zaidi ya dola 800,000 kwa mwaka. Ukibadilisha kwa fedha kwa *rate* ya leo, tuko kwenye zaidi ya trilioni moja. Sasa hebu tuangalie asilimia 0.2, hatukusanyi fedha nyingi usumbufu kwa wanunuzi, matokeo yake wanunuzi wetu wanaendelea kupunguza uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo linanisikitisha sana, zao la tumbaku linaingiza fedha nyingi sana, lakini juzi Waziri wa Afya amesema anaendelea kupiga marufuku matumizi ya tumbaku Tanzania na ni zao la kimkakati kwenye Serikali yetu. Hata kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ukurasa wa 41 linasema Serikali inahakikisha kufikia mwaka 2025, tutatoka kwenye tani 60,000 tutaenda kwenye tani 200,000, sasa tutafikaje kama wakulima tunaendelea kuwachanganya hivi? Waziri anasema anapiga marufuku matumizi ya tumbaku, kwenye ilani inasema inahitaji kuongeza uzalishaji, tuondoke na lipi? Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ambayo sasa ndiyo msahafu wetu wa Chama Cha Mapinduzi unasema tuongeze uzalishaji, lakini wengine tunasema tunapiga marufuku matumizi ya zao la tumbaku, wakulima hawa tunawachanganya na wanunuzi ambao wanaingia kutoka nchi za nje. Hivyo, ningeomba sasa tuangalie wapi ambao tunaweza tukasimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni riba za benki. Bado riba ya benki kwenye sekta ya tumbaku ni kubwa sana, bado ni asilimia saba kwa dola, ukizibadilisha leo ni zaidi ya asilimia 18 ya riba. Ningeomba mabenki yaendelee kupunguza riba, ni kweli juzi wametangaza ni asilimia tisa lakini asilimia tisa haiwafaidishi wakulima wadogo wadogo bado ni changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine masharti bado hawajayapunguza, unapunguza riba lakini masharti yanakuwa makubwa kwa wakulima wetu. Tungeomba sasa mabenki pamoja na kupunguza riba, wanaendelea kupunguza riba, lakini masharti yaendelee kupunguzwa ili wakulima wadogo wadogo waweze kukopa, wakulima wetu vijijini waweze kukopa, wafanyabiashara wadogo wadogo waweze kukopa na waendelee kufaidika, lakini tunaposema riba imepunguzwa lakini masharti yanaendelea kuwa magumu, haisaidii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kukushukuru sana, kwa kweli suala la riba ya benki ni changamoto kubwa sana. Naomba sana sekta ya pamba inaingiza fedha nyingi pia na yenyewe naomba kodi zake ziendelee kuondolewa ili wakulima wetu wanaolima pamba waweze kufaidika na pamba. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuunga mkono hoja, nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri, wanaupiga mwingi na wanamshauri vizuri Mheshimiwa Rais, Ahsanteni sana, hongereni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edward Kisau, halafu Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma na Mheshimiwa Mchungahela wajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kwa bajeti yake ya kwanza ambayo ni nzuri sana. Nampongeza pia Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, mwananchi; Mheshimiwa Naibu Waziri, Bwana Shemeji; na timu yote ya Wizara hii ikiongozwa na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wataalam wote kwa kazi nzuri ambayo mmefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii tunaipongeza kwa sababu ifuatayo: Moja, kuhusu kilimo. Kilimo fedha imeongezeka sana, shilingi bilioni 954. Ni ongezeko la Shilingi bilioni 660 ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2021. Pia bajeti hii imezungumza kuajiri vijana 3,000,000 wa kilimo na itatenga karibu hekta 8,500,000 kwa ajili ya umwagiliaji. Vile vile wanazungumza habari ya kuanzisha viwanda vya saa 24. *Twenty-four hours a day* na *seven days in a week,* hii itaongeza kasi ya ajira. Kwa hiyo, kwa kweli ni nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuhusu mifugo, mmezungumka habari ya kuongeza bajeti ya mifuko kwa shilingi bilioni 40 zaidi. Pia kuhusu *TASAF,* kuanzisha dirisha maalum kwa ajili ya vijana wanaotokana na familia ambazo zimejiandikisha kwenye *TASAF,* itaongeza sana sana sana ari ya wananchi. Kwa kweli vijana hawa wamekuwa wanateseka sana, hawawezi ku-*compete*. Usipowawekea dirisha maalum la kwao kwa kweli hasingeweza ku-*compete* kupata mikopo ile. Kwa hiyo, *big up*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sekta ya mifugo mmezungumza habari ya kuanzisha *incubation centers* na

kuajiri vijana 1,000 wawe na miradi ya kunenepesha, *very nice*. Ila nina angalizo vilevile baada ya pongezi zote hizo. Kuhusu tani za vyakula vya mifugo; Ilani ya Chama cha Mapinduzi Mheshimiwa Waziri wa fedha *I hope* unanisikiliza. Tulisema hivi ukurasa wa 52, tani za vyakula vya mifugo ni 8,000,000 kwa miaka mitano, lakini kwa *trend* sasa tumetoka 900,000 tukaenda milioni moja, na tani laki mbili, na sasa tunazungumza habari ya milioni mojam tani laki tatu na themanini. Kwa hiyo, tukiendelea kwenda na *trend* ya laki mbili, laki tatu hatutaweza kufikia tani milioni nane. Kwa hiyo, *in average actually* ilitakiwa kwa miaka mitano kuwe na *average* kila mwaka tuongeze tani 1,420,000. Kwa hiyo *we are not doing so well*. Kwa hiyo, tujaribu kuongeza bidii ili tufanye vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nimefurahi sana kuona *VETA* kuna fedha zimetafutwa kwa ajili ya *VETA* na Mheshimiwa Waziri mimi niliuliza swali la kwanza Bungeni hapa, namba 13 kuhusu Kiteto kutokuwa na *VETA*. Majibu niliyopata kutoka Wizara husika wanasema wanatambua Kiteto haina *VETA,* lakini itakuwa kwenye *priority list*. Wakileta zile *lists* zao la *VETA* 36, Kiteto isipokuwepo usi-*approve* huo mradi, kwa sababu majibu tuliyowapa wananchi ni kwamba lazima Kiteto iwepo, lakini kwa sababu mmesema mtajenga kwenye Wilaya zote ambazo hazina, Kiteto *I am sure* itakuwepo tena inatakiwa iwe namba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba sasa nizungumzie kitu kinachoitwa *carbon credits* ambayo ndiyo msingi wa hotuba yangu leo. *Carbon credit* ni *new source* ya *finance* ambayo itaiongoezea nchi mapato zaidi. Kwa Afrika nzima, Tanzania ni nchi ya tatu kwa kuwa na

eneo kubwa lenye mapori, baada ya *DRC* na Angola. Kwa hiyo, *potential* ya *carbon credit* kwa Tanzania ni kubwa zaidi, na kuna *study* zimefanyika na *natural conservancy* zinaonesha kwamba tangu Tanzania mmeanzisha mradi wa *Red Plus Project* na Tanzania imekuwa *pioneers,* tumeanza kufanya vizuri na tumeanza kuvuna fedha zinazotokana na *carbon credit. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimwuliza Mheshimiwa Kakoso kule kwao, Mbunge wa Mbulu kule kwao na Kiteto vile vile, sisi tumeanza miradi ya *carbon credit* na kwa kweli inasaidia sana wananchi. Nilitoa mfano siku moja hapa kwamba Kiteto, *internal revenue* ni *2.2 billion,* lakini sisi baada tu ya kuanzisha mradi wa *carbon,* vijiji vitano tu vinatengeneza *one billion a year*. Kwa hiyo, sasa tunge-*utilize* vile vijiji vyote, maana yake *carbon credit* ni *new financing area* ambayo ni lazima Wizara ya Fedha, Wizara ya Makamu wa Rais, Mazingira, na Wizara ya Viwanda na *TRA* lazima sasa mje *strongly* mtengeneze *policy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, alipokwenda Rais wetu kwenye baadhi ya safari za Kimataifa alisema hivi, baadhi ya wawekezaji, yaani wawekezaji wanaokuja kwa wingi sana ni watu wanaokuja na miradi ya *carbon credit*. Kwa hiyo, mtegemee kupata watu wengi sana wa *carbon credit. But it is a shame, we don't have a law and we don't have a policy*. Hakuna mtu atakuja hapa bila kuwa na *framework* na *legislation for certainty purposes.* Kwa hiyo, ni lazima sasa muanze ku-*speed.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Bunge hili, Mheshimiwa Mbunge wa Vunjo Dkt. Kimei aliuliza swali hapa la *cardon credit,* Mheshimiwa Mbunge wa Kilolo

aliuliza vile vile, lakini majibu tunayoyapata hapa, tunaambiwa bado Serikali inatengeneza *policy*. *Honestly! Six years, ten years down the line?* Mheshimiwa Rais anawaleta watu sasa waje kwa ajili ya wawekezaji...

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina nia ya kumvurugia mtitiriko Wakili Msomi, lakini naomba kumpatia taarifa kwamba kupitia mifuko mbalimbali ya mabadiliko ya tabianchi kama *Adaptation Fund*, *Climate Fund* na kadhalika, tungeweza kunufaika sana, lakini nchi yetu ina taasisi mbili tu ambazo zimekuwa *accredited* ambayo ni *NEMC* na *CRDB* na hizi fedha nyingi na *grants,* wala siyo mikopo. Kwa hiyo, naomba kumpa hiyo taarifa. Nchi kama Kenya ina taasisi 18, sisi tunazo mbili tu wakati hii ni fursa kubwa sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kisau.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na nakubaliana na mchango mzuri sana huo, sana! Kwamba hii biashara ya *carbon credit* siyo tu kwamba ni biashara *as business per-se,* lakini pia inaongezea nchi fursa za kupata *climate change financing*. Kwa hiyo, ni lazima tujikite zaidi kutokana na biashara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *in fact,* tunaambiwa tuna mapori *between 48 to 50 million hectors* nchi hii zipo *protected. How much we get it for this forest?* Ni rasilimali iliyopo, *in fact* watu wengine wanasema ni *business for doing nothing.* Yaani mapori yapo tu, *which is good for climate* na itakuletea mvua, acha kukatakata mapori, halafu utapata *cardon financing. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zinazoongoza sasa duniani *on cardon financing* na wanao-*produce carbon,* ya kwanza ni India; ya pili, Marekani; ya tatu, ni China; ya nne, Indonesia, Peru, Kenya, Brazil, Guatemala, Uganda *and Zimbambwe.* Zinazoongoza kununua, *market* ni *United States, France, United Kingdom, German and Switzerland.* Kwa hiyo, najua hii *carbon financing* ni *new area* hata Wabunge wengi hawafahamu. Naomba hata Bunge litafute mjadala wa siku moja ili Wabunge wafundishe Habari ya *carbon financing. It is a new sources of funding* ili tuje tupate mjadala, wataalam waitwe, waje watufundishe ili nchi sasa ianze kukimbia mbele zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Afrika kwa mfano, *projects* ambazo zimekuwa *registered on carbon financing* ni miradi karibu 234. *Asia and Pacific* 6,580; *Europe and Central Asia 89*; *Latin America* 1,139; *Middle East* ni 87 ambazo ni *worth 190 billion USD,* ni fedha nyingi sana. Tusiache Mheshimiwa Waziri hii ni *gold* ambayo imekaa ili tuweze kui-*utilize.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, halafu wajiandae Mheshimiwa Mwinjuma na Mheshimiwa Mchungahela.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa fursa hii ya kuchangia kwenye mpango na Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka 2022/2023. Awali ya yote nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan na Serikali yake kwa kuja na bajeti nzuri ya kimkakati, na mikakati iliyopo ndani ya bajeti hiyo inaendana na nyakati tulizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiisoma bajeti Kuu ya Serikali, ukatazama namna ambavyo Serikali inaenda kupunguza kodi, namna ambavyo Serikali inaenda kuwekeza kwenye miradi ya kimkakati, utaona moja kwa moja kwamba taswira na umbile la bajeti hii ni taswira ya kwenda kufanya *economic recovering* kufuatia kuanguka kwa uchumi wa Kitaifa na Kimataifa kulikosababishwa na mambo makubwa mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza likiwa, kuanguka na kudorora kwa uchumi kulikosababishwa na mlipo wa ugonjwa wa *Covid-19* mwaka 2019 ambapo madhara yake tunayapata mpaka leo. Jambo la pili, mdororo wa uchumi na changamoto tunazopitia leo hii zinafanana na zile za mwaka 1979 na 1980 ambao ulisababishwa na mapinduzi ya kule Iran ya wale Ma-shaah wa Iran ambapo mafuta kutoka Iran hayakuweza kuingia kwenye Soko la Kimataifa kirahisi na hivyo gharama za mafuta kwa maana ya *force refuels* zika-*double*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sasa hivi pia kumetokea mgogoro baina ya nchi ya Ukraine na Urusi ambapo hususan Urusi ni nchi ya pili kwa uzalishaji mkubwa wa mafuta na ni nchi ya kwanza kwa uzalishaji wa gesi. Kwa maana hiyo, kudorora kule kwa uchumi tunakokupata sasa hivi na kupanda kwa bei za mafuta kumesababishwa na mgogoro huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya changamoto za kiuchumi zilizotokea mwaka 1980 ama ukitazama changamoto za kiuchumi zilizotokea mwaka 1930 na miaka iliyofuatia kufuatia *the great depression,* utaona sera za kiuchumi ambazo Serikali za nchi mbalimbali zilichukua zilikuwa ni za *supply side economics,* kwa maana ya sera ambazo *proponents* wake ni wachumi kama akina John Bernard King ambao walikuwa wanazungumzia kwanza kuhusu Serikali kuongoza uchumi kwa maana ya kufanya *Government intervention* na kuachana na sera za kwamba Serikali haitoshikilia chochote kwenye uchumi, itauacha uchumi wenyewe ujiendeshe na mwisho wa siku kimbunga kikipita basi bahari itatulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sera hizi ninaziona moja kwa moja kwenye bajeti hii ya mwaka 2022, na pia naziona sera hizi kwenye mchakato mzima wa kuendesha uchumi wa Taifa letu katika kipindi cha mwaka mmoja cha uongozi wa Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, ambapo mambo yanayofanyika ni pamoja na kwanza kupunguza viwango vya kodi. Tumeona kodi zimepunguzwa maeneo mengi, na la pili ambalo tunaliona ni kuendelea kutekeleza miradi ya kimkakati kwa maana ya kwamba Serikali inaachia fedha ilizonazo, inazipeleka kwenye jamii kwa kutekeleza miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, tunaona Serikali ikichukua mikopo kutoka sehemu mbalimbali na hata sasa hivi ukisoma hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Fedha na mipango, unaona tayari wako katika *negotiation* ya mkopo wa zaidi ya Shilingi trilioni moja kutoka Benki ya Dunia. Wapo katika *negotiation* ya mkopo wa zaidi ya Shilingi trilioni mbili kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF),* lakini na pia unaona zile fedha za shilingi trilioni 1.3 za UVIKO ambazo zote zinakuja kuingia katika uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kuishauri Serikali iendelee katika *trajectory* hiyo hiyo, wasisikilize kelele za watu wanaosema tunakopa sana kwa sababu hao hawawatakii mema wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwanini nalisema hili, anasema, John Bernard King kwamba katika zama kama hizi ambapo unataka kuchochea ukuaji wa uchumi kufuatia mdororo, ni lazima Serikali iingilie, ni lazima Serikali ichukue hatua za muda mfupi, hatua za dharura za kuwakomboa wananchi wa kipato cha chini dhidi ya ukali wa maisha unaosababishwa na mdororo wa kiuchumi. Hatua zenyewe ni pamoja na kuhakikisha tunaongeza ajira kwa kuongeza uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila Rais wetu na Serikali yake kutoka nje, kuboresha mahusiano ya Kimataifa, kurudi ndani kuboresha mifumo na misingi ya utawala bora, hatuwezi kukopesheka, hatuwezi kuvutia wawekezaji kutoka nje kuja kuwekeza katika uchumi wetu, na hatimaye kuzalisha ajira, kuzungusha fedha katika mzunguko wa uchumi wetu, na mwisho wa siku tutaanguka vibaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kuwaambia Serikali kama ambavyo alifanya Ronald Regan miaka ya mwanzo ya 1980 na sera zake zikajulikana maarufu sana kama Reganomix na ambazo mimi pia nimezifuatilia kwa ukaribu na nimeandika katika kitabu changu cha Kigwanomix, napenda pia kuendelea kuwaomba watu wa Serikali wakae katika mtiririko huo huo wa kutanua uchumi wetu kwa kufanya uwekezaji lakini pia kuboresha mahusino ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi hatua zote ambazo zinachukuliwa na Mheshimiwa Rais nimeziweka katika makundi 10. Ukizitazama kwa undani wake unaweza ukaziita *Samianomix* kama ambavyo kule Marekani mwaka 1980 waliziita sera za Rais wa wakati huo Bwana Ronald Regan, Reganomix. Kwa hiyo, nami napenda kuzitaja hatua ambazo zinachukuliwa ni pamoja kupunguza viwango vya kodi, kufuta baadhi ya mipango isiyo na tija kama hii ambayo ameisema Waziri wa Fedha wakati anasoma bajeti yake; kupunguza magari, lakini pia gharama za kusimamia magari ya watumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ya tatu, kupunguza matumizi ya Serikali kama ambavyo tunaona Waziri wa Fedha alipohutubia, kupunguza riba kwenye benki zetu kama ambavyo tunaona kwenye benki katika kipindi cha Mheshimiwa Mama Samia, baadhi ya benki zimeshusha viwango vya riba mpaka asilimia tisa. Pia kuendelea kukopa mitaji kutoka nje ili kuleta katika uchumi wetu; sita, kuboresha utawala bora na uhusiano wa Kimataifa kama ambavyo tunaona, Rais ana-*reach out* kwenye Mataifa mbalimbali, kama ambavyo tunaona Rais ameweza kuitangaza Tanzania vizuri sana kupitia *Royal Tour*.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hapa napenda nitoe mapendekezo kwamba Waziri wa Maliasili na Utalii akatazame mkakati ambao tulianza kuufanya kipindi mimi nikiwa pale Wizarani wa kutangaza vivutio vya Utalii kwenye michezo hususan Soka la Ulaya. Hii ni katika mikakati ambayo itaungana na *Royal Tour* katika kuvutia wawekezaji na wageni kuja kutembelea Tanzania. Ni mkakati ambao utaendana na Samianomix.

Mheshimwia Naibu Spika, la saba ni kutekeleza miradi ya kimkakati kwa kutumia fedha za nje badala ya kutumia fedha za ndani. Kwa hiyo, ni katika ile ambayo ameisema Waziri wa Fedha hapa *EPC+F*.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba nane ni kuendelea kuwekeza kwenye sekta ambazo zinagusa watu wengi ikiwemo sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi kama ambavyo bajeti inasema; tisa, ni kuboresha huduma za jamii kama ambavyo tumekuwa tukifanya; na kumi, kuwekeza zaidi kwenye miradi ya kimkakati kwa mfano miradi ya gesi, aliongea vizuri sana Mheshimiwa Prof. Muhongo, sina haja ya kurudia. Siyo tu kwenye gesi wameanza na *LNG plant*, waende kwenye miradi ya mbolea ambayo inatokana na gesi, waende kwenye miradi ya madawa ambayo inatokana na gesi, na tukifika hapo, tutakuwa tumeweza kuchomoka katika mtanziko tulioingia kutokana na changamoto nilizozisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muda umeniishia, ningeweza kuongea mengi zaidi. Nashukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Dkt. Kigwangalla. Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, tunao Wanafunzi 150, Walimu Watano wa Shule ya Sekondari Pallotti kutoka Mkoani Singida. Karibuni sana. Wanafunzi 80 na Walimu Wanne kutoka Shule ya Sekondari Mvumi ya Wilayani Chamwino, Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana kwa mafunzo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Mwinjuma, Mheshimiwa Mchungahela, Mheshimiwa Makoa, atafuatiwa na Mheshimiwa Njau.

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ya Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu na nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake nzima kwa hotuba nzuri iliyobeba dira, dhamira, maono na mwelekeo na huruma ya Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa Watanzania, inatia moyo na tunachoweza kufanya ni kuendelea kumuombea Mheshimiwa Rais Mungu amuweke kwasababu kuna mahali tunapoelekea na kuna mwanga mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nimpongeze kwa kuyatafsiri yote haya malengo ya Mheshimiwa Rais kwa matendo katika kipindi cha mwaka mmoja huu, kusema kweli ile kauli ya unaupiga mwingi na

wewe inakuhusu moja kwa moja. Mara nyingi mimi nasema Kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu unakuwa huna baya isipokuwa inapokuja mambo yako ya 'Utopolo' tu lakini huko kwingine upo safi kabisa. Hongera! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ni nzuri hata hivyo kuna maeneo kadhaa ambayo mimi nahisi naweza kuweka senti hamsini zangu. Kwanza kabisa ni katika ukurasa wa 69 ambapo Mheshimiwa Waziri anapendekeza kuhusiana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri zetu kwamba tuikate kwa asilimia 50. Asilimia Tano iende kwenye kutengeneza miundombinu ya masoko ya Wamachinga. Kwanza, mimi niseme msingi wa sera ile, msingi wa ule mwongozo ilikuwa ni kuwawezesha wananchi kiuchumi, kuwakwamua kwenye umaskini, kuwaunganisha na Serikali yao moja kwa moja kwa kuwahakikishia kwamba hali zao za kiuchumi binafsi zinaimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ile imekuwa inafanya shughuli nzuri ina changamoto za hapa na pale lakini naamini suluhisho la changamoto zile si kuikata kwa asilimia 50 na kuirudisha kwenye Halmashauri, hili jukumu la kujenga miundombinu ya masoko ya wamachinga ni jukumu la Serikali, Serikali isilikimbie inabidi ilifanye kwa namna yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuchukua asilimia Tano kati ya asilimia 10 zile na kuirudisha Serikalini ni kuwapora akina Mama, Vijana na Watu Wenye Ulemavu fedha ambazo tulikuwa tumeshawaahidi na zinawasaidia kwelikweli. Mimi kwa mfano, Muheza pale mapato yetu ya ndani ya Halmashauri ni takribani shilingi bilioni 2.1 kwa hiyo, kiutaratibu tunatakiwa kutoa shilingi milioni 210 kila mwaka

kwa ajili ya kuyawezesha makundi haya. Sasa pamoja na mzunguko na marejesho tunakaribia kutoa shilingi milioni 500. Makundi ambayo yananifuata mimi binafsi, makundi ambayo yanamfuata Mkurugenzi, yanamfuata Mkuu wa Wilaya kumuomba awasaidie kupata mikopo hii kwa ajili ya kujisaidia kwenye shughuli zao za kiuchumi ni mengi mno hata hiyo hela yote ambayo tunayo haiwezi kufika nusu ya haja tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, kusema ukweli Mheshimiwa Waziri wa Fedha ninakuomba hii asilimia Tano tusiiguse huku, tusipite njia hii haitoki na Serikali isikwepe kama kuna lolote ambalo lingeweza kufanyika kwanza, ningehisi kwamba ungetoka mwongozo mwingine wa hii fedha iongezwe kwa sababu inawasaidia moja kwa moja inamsemea vizuri Mheshimiwa Rais, inaisema vizuri Serikali, inasema vizuri Wabunge, Madiwani na Halmashauri zetu. Kwa hiyo, badala ya asilimia 10 pengine ingeenda kuwa asilimia 15. Serikali ifanye jukumu lake la kujenga miundombinu kwenye masoko ya wamachinga kwa fedha ambazo yenyewe itazipata wapi hatujui, lakini ihakikishe kwamba fedha hii haiguswi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kuna uwekezano tena Serikali itoe ruzuku kwa Halmashauri zetu ambazo zinaingiza mapato kwa kiwango ambacho kimekusudiwa, kimekadiriwa basi zipewe ruzuku kwa ajili ya kufanya miundombinu hii ya wamachinga na siyo kutoa kwenye fedha hizi ambazo tulishaahidi makundi haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, pendekezo hili Mheshimiwa Waziri mimi niseme kwamba sikubaliani nalo na

ninapendekeza tuachane nalo moja kwa moja lisirudi wakati wa majumuisho yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nimemsikia pia akisema kwamba Pato la Wastani la Mtanzania kwa sasa ni Shilingi Milioni 2.8 na hii inamaanisha ni kama 233,000 kwa mwezi, hatupo vibaya kusema kweli dola elfu moja mia moja na kitu, lakini tunaweza kuimarisha kwa kulainisha zaidi mazingira wezeshi yanayomfanya Mtanzania wa kawaida kujiongezea kipato chake, kwenye hili bado hatujafanya vizuri sana kuna maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mfano; kule kwetu Muheza kuna Tarafa inaitwa Amani katika vijiji vya Fanusi, Magoda, Kisiwani na Kavaa kule Amani tulikuwa tunafanya miradi ya ufugaji wa vipepeo kabla ya mwaka 2016, halafu likatoka zuio 2016 la kuzuia miradi ile isifanyike, najua ukisema miradi ya vipepeo watu wanajua kama mnachukua vichujio vile mnaenda kukamata kwenye maua haipo hivyo ni miradi mikubwa ambayo ilikuwa inawasaidia sana wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kaka yangu Mheshimiwa January Makamba alipokuwa Waziri wa Mazingira alishatembelea miradi ile, somo yangu Mheshimiwa Hamisi Kigwangalla alipokuwa Waziri wa Maliasili alishajionea na juzi Mzee wangu Mheshimiwa Jerry Silaa akiongoza Kamati yake ya Uwekezaji walipita pia kule, na wote wamekuja na *positive feedback* kwamba miradi ile kwanza haina athari za kimazingira, vipato vya wananchi vinaongezeka, shughuli za kijamii kama maji na madarasa yamejengwa na miradi ile pia vilevile na inatusaidia kulinda misitu kwa

sababu wananchi wanapata shughuli nyingine za kiuchumi za kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016 mpaka sasa hivi ni miaka takribani Sita, pengine mwongozo ulitoka haraka haraka kwa sababu ulikuwa unataka kulinda swala, pundamilia na twiga wetu wasitoroshwe na ukawa haukupata muda wa kutofautisha kati ya pundamilia na vipepeo, lakini mimi ninachosema ni kwamba imechukua miaka sita sasa kwamba wataalam wetu wameshindwa kufanya kazi yao ya kuweza kutofautisha kati ya wanyama ambao wanatakiwa kulindwa wasitoroshwe kwenye nchi hii na hawa Vipepeo wanaoishi kwa siku 14. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mzigua mmoja hapa nyuma yangu anasema kwamba tunakaa kwa miaka Sita tunabishania kuhusiana na wadudu ambao wanaishi kwa siku 14. Miradi ile ilikuwa inawasaidia wananchi wa maeneo husika wanapata mpaka kiasi cha shilingi milioni moja kwa mwezi, sasa katika nchi ambayo pato la Mtanzania ni shilingi milioni 2.8 kwa mwaka mtu mmoja anapata milioni 12 kwa mwaka na bado tunamzuia, tunamfanyia roho mbaya tu ili mradi asifanye biashara hii kwa sababu ya uvivu tu wakushindwa kutenganisha kati ya swala na vipepeo hii siyo sawa! Hili eneo hatujafanya vizuri Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine unaona kama kuna masihara yanafanyika mpaka juzi Kamati ya Bunge ya Uwekezaji inayoongozwa na Mzee wangu Jerry Silaa ilitoa maagizo ya kwamba suala hili lifanyiwe kazi na miradi ile ifunguliwe, vipepeo waendelee kusafirishwa lakini mpaka sasa hivi hamna hata mtu mmoja aliyetingisha hata

unywele! Sasa hii maana yake ni kama ni dharau kwa Bunge vilevile kwasababu kutenganisha kati ya vipepeo na Swala kusema kweli ….

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa mchangiaji kwamba siyo tu miradi ya kufuga vipepeo ina faida na tija kubwa kwenye maisha ya wafugaji ambao ni wananchi wa vijiji alivyovitaja, bali pia miradi hiyo inafaida kubwa sana kiuhifadhi na kimazingira. Pia miradi ya vipepeo haihusiani kabisa na sababu zilizopelekea kuzuiliwa kwa wanyama kusafirishwa nje ya nchi ambazo nyingi zilikuwa ni kelele na vilio vya wananchi baada ya kusikia kwamba Twiga na Pundamilia wanasafirishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa apokee taarifa hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwinjuma taarifa hiyo.

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kigwangalla *will always come to my rescue,* ahsante sana naipokea taarifa hii kwa mikono miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichokuwa najaribu kusema ni kwamba hata watoto wa Darasa la Nne wangeweza

kutofautisha kati ya Swala, Pundamilia na Vipepeo bila wasiwasi wowote, sasa sisi tuna watalaam ambao kabisa wamesomeshwa na hela za kodi za wananchi wa nchi hii, wameshindwa kufanya shughuli hii wakaandika madokezo na kupendekeza kwamba miradi ile iruhusiwe kwa miaka Sita, haya ni masihara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Bunge lako Tukufu miongoni mwa mambo ambayo tunatakiwa kuyafanya ni kuhakikisha tunawalegezea mazingira wananchi ya kujiingizia vipato vyao binafsi, hili likiwa mojawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela, Mheshimiwa Makoa, ajiandae Mheshimiwa Njau.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na afya kuweza kutekeleza majukumu yangu ya kila siku, pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii kulihutubia Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru mzalendo Namba Moja Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa uzalendo wake aliouonyesha ni uzalendo mkubwa sana, siku tulipoingia mkataba wa *LNG* ule hodhi, Mheshimiwa Rais alifanya kitu kikubwa sana ambacho aliitangazia Dunia kwamba yeye anafahamu sana diplomasia ya uchumi. Mheshimiwa Rais alisimama na kuwaambia wawekezaji kwamba wanapokuja Tanzania

wahakikishe kwamba wanayo dhamira ya dhati ya kufanya biashara nasi na kwamba mkataba ule usije ukawa ni shere ya kutufanya sisi tuendelee na jitihada zetu zakutafuta mtu wa kutusaidia kushughulika na biashara ile. Ikawa wao wanaishikilia kwa maana waendelee kufanya biashara ile kwenye maeneo mengine walikowekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli hii imetoka mdomoni mwa Mheshimiwa Rais ni kauli nzito sana ile ni *message* ambayo inatakiwa watu wote tuzingatie kwa sababu ni *message* inayoonyesha uzalendo wa hali ya juu na kuonesha ni kwa jinsi gani yuko *serious* hasa katika suala hili la uwekezaji. *Message* kwa mtindo upi? Kwamba Tanzania kama nchi ni nchi tajiri sana na ina madini mengi lakini ina vitu vingi sana vitakavyoweza kutusaidia tukiamua kuvitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, l*message* ile ilikuja kwa Watendaji pia kuwa wakati wanatengeneza mikataba wawe makini sana kwa sababu *failure* inaleta hasara kubwa sana katika nchi, lakini *message* kwa dunia na wawekezaji kwamba wanapokuja Tanzania wajue kwamba biashara ya uwekezaji Tanzania ni *very serious* siyo kitu cha mchezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli ile ilinitia nguvu kama nilivyosema kuhutubia Taifa, dhana hii ya kuhutubia Taifa kuna baadhi hawaielewi lakini siwezi kuwalaumu kwa sababu ni dhana yenye maana pana sana pia ni mtambuka. Kwa kifupi tu ni kwamba ni dhana inayoendana na falsafa ya kuchunga fedha, falsafa ambayo inafanya kazi vizuri sana katika mazingira ya jamii yenye itikadi ya kizalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema ni itikadi maana yake siyo wimbo wa kizalendo kwa maana itikadi ni dini na dini ni kuamini na kuabudu. Kwa hiyo, Watanzania lazima tuamini na kuabudu kwenye itikadi hii, tukifanya hivyo itatusaidia sisi kufanya yale tunayokusudia kuyafanya kwa maslahi ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumepungukiwa sana na hii dhana ya uzalendo, tumekuwa hatuwezi kuweka maslahi ya Taifa mbele na hii imetokana na jinsi tulivyopita katika mapito mbalimbali kuelekea kutengeneza uchumi wa nchi hii, mapito ambayo yameleta athari mbalimbali ambazo hasi pamoja na athari chanya, sitazungumzia athari chanya kwa sababu zimegusa watu wachache lakini athari hasi zimegusa watu wengi kwa maana jamii nzima. Athari hasi zimetengeneza mitazamo hasi pia kwa jinsi tunavyoangalia mambo mbalimbali ya muhimu sana yanayohusu maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, tukiangalia dhana ya elimu, jamii ya nchi hii kutokana na athari zilizojitokeza inaiangalia elimu kuwa ni chombo cha kutengeneza fursa ya ajira ambayo itatengeneza fedha, kwamba mtu anayetafuta ajira ni lazima aje kuajiriwa baadaye lakini ajira hiyo impe fedha. Sasa mtizamo huu ukiuangalia umeleta msukumo ambao unaleta changamoto sana katika utendaji wa masuala mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, unakuta kwamba kila mtu anayetaka kusoma, anataka kusoma masomo ambayo anasema ni yenye mlengo wa *deal,* masomo yatakayo mpa ulaji na hata wazazi wamekuwa wakiwasukuma watoto wao kusomea masomo ya namna

hiyo na kuacha masomo mengine, pia msukumo wa kikazi uko katika kutafuta fedha kwa maana mtu anahangaika kutafuta kwa njia yoyote ile, bila kujali hata kama fedha hiyo inapatikana kwa taratibu unaostahili au lah. Kwa hiyo, kumekuja na mtazamo kuwa mwajiriwa akimuibia mwajiri wake hata kama wizi huo utasababisha kufilisi kampuni au kama utasababisha kuyumbisha uchumi wa nchi, mtu huyo anaonekana kuwa ni mtu mjanja. Sasa suala hili ni baya sana ndugu zangu watanzania, tunatakiwa kwa makusudi kabisa tuwe na jitihada za kuepukana nalo jambo hili, tufanye jitihada kubwa sana kuwasomesha watoto wetu kuwaelimisha lakini kuwaelimisha kizazi chetu na jamii nyingine kwamba tunatakiwa tuifikirie nchi kwamba ndiyo pekee yenye maslahi, wewe usifikirie kwamba nchi itakufanyia nini lakini fikiria kwamba wewe utaifanyia nini nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba kumekuwa na mtizamo wa masuala tofauti tofauti, pia kumekuwa na changamoto sana katika usimamizi wa bajeti kwa mfano, Serikali kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi imelazimika kwa namna moja ama au nyingine kutekeleza miradi mkakati. Miradi hii kama tutaangalia mapato yetu ya ndani hatuwezi kuitekeleza au itachukua muda mrefu sana kuitekeleza, lakini kutokana na hiyo Serikali inalazimika kwenda kukopa. Mheshimiwa Rais kwa mfano, ameenda nje akajitahidi kukopa zile fedha zikija hapa ni fedha zinatakiwa ziende moja kwa moja katika miradi mkakati, kwa sababu kama hazitaenda huko zitatupa madeni makubwa ambayo itakuwa ni mzigo mkubwa kwa Serikali, nataka jambo hili lieleweke tukiangalia kwa mfano kwenye bajeti tunaweza tukalielewa jambo hili vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Mwaka 2019 kwenda 2020 tulikuwa na bajeti ya kulipa Deni la Taifa takribani Trilioni 9.3 lakini bajeti ya Mwaka 2020 kwenda 2021tulikuwa na *amount* ya kulipa Deni la Taifa trilioni 10.4 bajeti ya mwaka 2021/2022 tulikuwa na bajeti ya kulipa Deni la Taifa shilingi trilioni 10.6 lakini kwenye bajeti ya mwaka huu kuna mapendekezo *estimation* ya kulipa Deni la Taifa takribani trilioni 9.093 ukijumlisha hii yote kwa miaka minne utakuta ni zaidi ya trilioni 39 fedha ambayo ni nyingi sana yaani ni bajeti nzima ya mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unaweza ukaona kwa jinsi gani hapa fedha nyingi sana kama hii ingeweza ikatumika katika masuala mengine kwa mfano, tungekuwa tunatumia ile trilioni kumi ya kila mwaka kuchanganya na fedha nyingine ya maendeleo utaweza ukaona kwa jinsi gani fedha hii ingeleta tija kubwa sana, lakini kwa sasa hivi fedha hiyo tunalipa deni, hapo ndipo linapokuja umuhimu wa sisi kusimamia hii fedha ya madeni tunayoikopa kutoka nje ili kusudi ifanye kazi inayostahili pia kusimamia ni pamoja na kuhakikisha tunapunguza changamoto zozote zile za kuongeza riba katika madeni hayo, kama hatuwezi kufanya hivyo maana yake tunaingizia hasara nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye usimamizi, kuna suala la kwamba, Wabunge wanatakiwa kusimamia. Tukiangalia hapo kuna changamoto, changamoto ipo kwamba je, Mbunge anasimamiaje? Mipaka yake ya kusimamia ni nini, nini anatakiwa asimamie, nini hatakiwi kusimamia. Akienda kuangalia akakuta kuna changamoto anaziripoti kwa nani?

Je, Mbunge kama kazi hii ya kusimamia anatakiwa kuisimamia, anawezeshwa, ana uwezo wa ku-*move* kutoka eneo moja kwenda lingine kusudi kuangalia miradi hii jinsi inavyofanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia pia usimamizi unapwaya kwa wenzetu Madiwani ambao ni muhimu sana. Tukiangalia Madiwani wao ndiyo wana nafasi kubwa ya kusimamia kwa sababu miradi hii inafanyika katika maeneo yao. Lakini Diwani ndugu zangu yuko hohehahe. Tukiangalia kimshahara, Diwani ni kama hana mshahara. Hata posho anayopewa Diwani haitoshi kabisa, kiasi kwamba suala la usimamizi kwake yeye linakuwa ni suala nyeti kabisa kwa sababu kuna wakati anaweza akatishiwa hata na Mtendaji kwa sababu tu hana kipato kizuri kiasi cha kumfanya Mtendaji amshawishi Diwani kufanya kitendo kibaya cha kuweza kubadili fedha ambayo inatakiwa kusimamiwa ikatumika vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye hili, ninalo la kuishauri Serikali. Tujaribu kufumba macho tuweze kumwezesha Diwani, kwa sababu Madiwani katika halmashauri 185 za nchi hii, kuna Madiwani 5,774 kiasi kwamba tukiamua tukatoa shilingi milioni moja kama mshahara wa Diwani kwa mwezi, tuna uwezo wa kumpa... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante, kengele ya pili hiyo. Mheshimiwa Kengele ya pili hiyo, ahsante.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sekunde mbili, tatu nimalizie, kwamba tukiweza kumlipa Milioni moja kila Diwani, tuna uwezo wa kulipa…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, mengine utaandika. Unaruhusiwa kuandika. *(Makofi)*

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Makoa, jiandae Mheshimiwa Njau.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango pamoja na Bajeti hii ya 2022/2023. Kwanza niipongeze Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutekeleza vilivyo Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kutuletea mpango ambao kwa kweli umekwenda kuwagusa wananchi wa maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuanzia mwanzo mpaka mwisho sijaona mahali pameelezea japo kwa ufupi Sekta ya Ardhi. Kwa hiyo, naomba angalau wakati Mheshimiwa Waziri anakuja ku-*windup* japo atuletee maelezo mafupi kuhusiana na Sekta ya Ardhi kwa sababu shughuli zote za kiuchumi zinafanywa kwenye ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ardhi hii inaipa nchi kipato kikubwa sana, kwa sababu ardhi iliyopimwa ina uwezo wa kuchangia kipato kikubwa sana kwenye Taifa hili.

Moja, wakati wa mauzo ya ardhi Serikali inapata fedha, pia wakati wa kodi ya viwanja na wakati wa malipo ya kodi ya majengo. Kwa maana hiyo, tupate japo maelezo kidogo tuone namna gani Wizara hii inakwenda kuweka umuhimu wa sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya vizuri sana kwenye Sekta ya Ardhi. Leo Serikali imetoa mikopo kwa ajili ya halmashauri kwenda kupima ardhi zao. Halmashauri nyingi zimenufaika kwa mikopo ya Serikali. Mwezi huu tu Wizara ya Ardhi imeweza kukopesha halmashauri mkopo usio na riba wenye thamani ya shilingi bilioni nne kwa halmashauri nne. Kwa maana hiyo, sekta hii ni muhimu sana na Wizara inafanya vizuri sana kuhakikisha maeneo haya yanapimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la Sekta ya Utalii tumeona namna gani watalii wameongezeka kutokana na filamu ya *royal tour* na tuna habari kwamba Zanzibar imejaa wageni, lakini hata Bara wamejaa wageni kutokana na *royal tour.* Sasa sisi kama Taifa tunatakiwa sasa katika mipango yetu ya ndani tuhakikishe ujio huu wa wageni wengi usikome na uendelee muda wote. Utaendelea vipi? Ni kwa sisi wenyewe kupanga mikakati yetu ya ndani kuanzia tunapoweza kumpokea mgeni anapoingia mpaka wakati anaondoka, kiasi kwamba wakati anaondoka atamani tena kurudi ama atamani kwenda kushawishi wageni wengine waje kuitembelea nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunapaswa kutoa vikwazo vyote ambavyo vitakuwa ni kero kwa wageni wetu. Kwa hili naamini Wizara itafanya vizuri na itahakikisha kazi

kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Rais itaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoongelea Sekta ya Utalii katika nchi hii, ni sekta ambayo inachangia katika pato la Taifa zaidi ya asilimia 17. Ni sekta ambayo imetoa ajira zaidi ya wananchi wa Tanzania 1,600,000. Kwa hiyo, ni sekta muhimu sana. Kwa hiyo, sisi tunapoiongelea Wizara ya Maliasili, tunatakiwa tuongelee Wizara kwa umakini sana kwa kujua kwamba Wizara hii imebeba uchumi mkubwa wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mawazo yoyote ya mtu yoyote ambayo yanaenda kwenda kuudumaza utalii wetu tuyakatae kwa nguvu kubwa sana. Ukishateuliwa na Mheshimiwa Rais kwenye sekta hii, katika Wizara hii usitegemee utasifiwa kwa sababu Wizara zote zinawatetea wanadamu, wewe peke yako utakuwa unatetea wanyama. Kwa maana hiyo, hakuna nafasi ya kusifiwa, unachotakiwa kufanya ni kusimamia sheria kwa ajili ya kulinda urithi wetu ambao sisi tumerithishwa na Watanzania, watoto wetu na wajukuu zetu watatamani kwenda kuona hivyo ambavyo tumevitunza tukarithishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda Sekta ya Ujenzi. Kuna jambo moja hapa ambalo nataka Bunge lako liweke sawa. Tuna Ilani ya CCM ambayo imeandaliwa vizuri sana na viongozi wetu makini na nina uhakika Ilani ile ni Ilani bora sana na ikitekelezwa tunakwenda kumuinua mwananchi mmoja mmoja. Sasa katika ujenzi lengo la CCM ni kuhakikisha wanaendelea kujenga barabara ili kuwawezesha wananchi waweze kujijengea kipato chao na maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hii barabara ya Handeni inayokwenda mpaka Singida. Barabara hii nimepata mashaka kidogo, kwanza kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameitaja vizuri barabara hii. Amesema kwamba barabara hii ya kilomita 460 itaanzia Handeni – Kibrashi – Kibaya na kwenda mpaka kwa Mtoro, lakini katika Mpango wa Serikali pia umetaja kama alivyotaja Waziri wa Fedha, hii haina mashaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro unakuja kwenye taarifa ya Wizara ya Ujenzi, wao waliitaja kwamba inatokea Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Ugoloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha halafu inarudi tena Chambalo inakwenda tena Chemba ndiyo iende kwa Mtoro halafu Singida, jambo hili ambalo haliwezekani. Ni kwamba barabara imezungushwa eneo moja lilelile ambalo nadhani Ilani ya CCM ambayo ndiyo ilitaka Serikali ijenge ile barabara, imeeleza vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Ilani ya CCM ukurasa wa 73 imetaja kwamba barabara hii itajengwa kuanzia Handeni - Kibirashi – Kondoa kwenda Singida wakifahamu kwamba, barabara hii ni barabara ya *TANROAD* ambayo ilikuwepo miaka mingi na ndiyo inafahamika. Barabara hii inatakiwa ijengwe kuanzia Handeni – Kibirashi – Mrijo Chini iende Dalai, iende Mondo, iende Bicha, iende Selya ikatokee kwa Mtoro ndizo hizo kilomita 440 zitatimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mpango huu na nilikwenda kuonana na Naibu Waziri wa Ujenzi, yeye pia ana mpango wake, ambao mpango wake niliona unakata

vijiji na mitaa mingi sana inaishia nyuma ya kijiji ambacho kinaitwa Dalai, halafu inakwenda Chemba halafu ndiyo inakwenda kwa Mtoro, Ilani ya CCM haijasema hivyo. Ilani ya CCM imesema barabara hii inakwenda Kondoa halafu ndiyo kwa Mtoro, halafu ndiyo ufupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitokea Kondoa kwenda Singida kwa njia ya Kwa Mtoro haizidi saa moja na robo, lakini kwa namna Wizara ilivyosema, ukitokea Kondoa kwenda Singida kwa barabara hii wanayoisema ni zaidi ya masaa manne. Kwa hiyo, utaona kwamba barabara hii inatakiwa Mheshimiwa Waziri akija, atamke ili wananchi wa Dalai, Mondo, Bicha na Selya wajue kwamba mpango wa CCM kwenye Ilani yake utatekelezwa kama namna Ilani ilivyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu wakati vikao vya chama vinapendekeza barabara hiyo ni kama vilijua. Barabara hii ndipo Mradi ule wa Bomba la Mafuta unapopita. Sasa ukiikwepesha barabara hii maana yake shughuli nyingi za uchumi zitakwama. Kwa maana hiyo, barabara hii ni muhimu kwa sababu kuna bomba la mafuta na kuna kituo kikubwa ambacho kitajengwa katika Kata ya Selya. Kwa maana hiyo, kutokuitendea haki barabara hii kutasababisha kwamba mengi kutoenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu barabara hii ya *TANROADS* ndiyo barabara ambayo itapokomea hapo Selya itakuwa inaelekea Usandawe ambako ndiko huko kwa Mtoro. Hapa inapokomea ni barabara ya *TANROADS* ambayo inakwenda kuunganisha na Hanang'. Tunafahamu Hanang' ni wakulima wazuri wa zao la ngano. Sasa kuzunguka kwenda Moshi mpaka Tanga kwenda Dar es

Salaam au Singida kuja Dodoma – Morogoro watakuwa wanatembea kilomita zaidi ya 600, lakini kwa kupitia Kondoa ni hizi hizi kilomita 460.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naunga mkono hoja, lakini Mheshimiwa Waziri akija atuelezee kwamba CCM ilivyopanga kwenye Ilani ndicho kitakachofanyika kwenye barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau. Wajiandae Mheshimiwa Sima, Mheshimiwa Songe na Mheshimiwa Gambo.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye hotuba hii ya Bajeti. Nikianza na hotuba hii ya bajeti, nimeiona imejikita kwenye mambo mengi ikiwemo utalii, uvuvi na mambo mengine. Si mbaya kwa sababu tayari tunatafuta keki pana zaidi kwa ajili ya kugawanya mgawanyo wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi sijaona kipengele muhimu sana cha diplomasia ya uchumi. Kinachofanyika katika Taifa letu, Mama Samia Suluhu Hassan amekuwa kama *assist* kwenye ulingo wa mpira. Sasa wanatakiwa ma-*striker* wa kufunga magoli, hivyo, kila mtu acheze kwenye nafasi yake. Wakati tukiimba *royal tour* inaleta matokeo ni lazima sasa twende kwenye diplomasia ya uchumi tuangalie tutapataje watu kupitia *royal tour,* wawekezaji pamoja na fursa mbalimbali katika Taifa letu.

Yeye amecheza nafasi yake na sisi tunatakiwa kucheza kwenye nafasi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikisema hayo, naenda moja kwa moja katika balozi zetu. Huwezi kuongelea diplomasia ya uchumi kama usipogusa balozi zetu nje ya nchi. Sasa hivi kuna shida kubwa katika balozi zetu nje ya nchi ambapo kuna uhaba mkubwa wa watumishi. Wale watu wanatakiwa wawe ndiyo *reception* yetu ya kupokea watalii, wawekezaji na watu wanaokuja kutafuta fursa na kutafuta sisi fursa kwenda nje, lakini kuna uhaba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukaguzi wa *CAG* wa Machi, 2022, inaonekana katika balozi sita kuna upungufu wa watumishi 26. Kiwango hiki ni kikubwa kwa sababu walitakiwa wawe watumishi 62 lakini wapo watumishi 38 tu. Hawa ndiyo tunaowategemea wawe *reception* yetu ya kupokea watalii na kupokea wawekezaji, hili ni janga. Wakati tunakwenda katika nchi ya Kongo, pia tulikutana na hii kesi ya upungufu wa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishauri, nikasema katika balozi zetu huwezi kuuza bidhaa zako ukazifungia chumbani, ni lazima uzitangaze. Katika balozi zetu hakuna kitengo ambacho ni cha habari. Ukiangalia *blog* mbalimbali za Wizara, ukiangalia kwenye *social media* huoni utangazaji wa fursa za kiuchumi za Tanzania kama ilivyo, huoni watu wamejipambanua. Tunahitajika kujipambanua zaidi kama Tanzania, tusisubiri mtu mmoja atangulie mbele halafu sisi tukarudi nyuma. Tutakuwa tunaharibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia katika suala zima la watumishi. Kama watumishi hawapo wa kutosha, ule mzigo unakuwa ni mkubwa, ufanisi unakuwa duni. Kwa hiyo, naomba wakati Waziri anakuja aweze kutuwekea mkakati bayana ni namna gani tunaenda kujaza hizi nafasi za watumishi katika balozi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, athari hii imekwenda moja kwa moja kwenye utekelezaji wa dhana ya kidiplomasia katika balozi zetu. Mwaka 2020/2021, balozi sita nje ya nchi zilishindwa kutekeleza dhana hii kwa kukosa bajeti. Siyo kwamba zilikosa hakuna, hazikupelekwa, zilitengwa na Bunge lako Tukufu lakini hazikupelekwa nje ya nchi. Nikifika hapa naunga mkono kile kipengele cha ufuatiliaji kwa ajili ya kuangalia bajeti tunazotenga, je, zinafika kwa wakati na zinafika kama tulivyozitenga? *Otherwise* tutakuwa tunakaa hapa na tunachokisema kinapotelea hewani, bila kipengele hicho hatuwezi kuvuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niainishe balozi ambazo zilishindwa kutekeleza hii dhana ya diplomasia ya uchumi nje ya nchi kwa vitendo kwa kukosa bajeti. Bunge lako tukufu 2020/2021, lilitenga shilingi 116,200,000 kwenda Ubalozi wa Kinshasa Congo, lakini fedha zilizopelekwa ni Sh.13,000,000, sawa na asilimia 11, tunatokaje hapa? Balozi ya Lilongwe ilitengewa shilingi 57,000,000, zilipelekwa shilingi 12,000,000 sawa na asilimia 21. Tunaondokaje hapa kwenda mbele? Ubalozi wa Doha ulitengewa shilingi 75,600,000, tulipeleka shilingi 10,000,000 tu, sawa na asilimia 14. Tuna *move* vipi kwenda kufunga magoli, vita iliyopo sasa hivi kwenye Taifa ni vita ya kiuchumi siyo vita ya mtu kwa mtu. Tunaingiaje kwenye ushindani wa kiuchumi kama

*reception* yetu imefungwa na hakuna pakupita? *(Makofi/Kicheko)*

*Mheshimiwa Naibu Spika, Addis Ababa tulitenga shilingi 138,000,000 zimepelekwa shilingi 2,000,000 tu, shame.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni sawa na asilimia 1.8. tunakwenda wapi? Ubalozi wa *Washington DC* tulitenga shilingi 144,000,000,000 lakini zilizopelekwa ni shilingi 8,000,000, sawa na asilimia saba. *How can we move* kama nchi kama tunakwenda kufanya mambo kama hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye kipengele cha pili. Hawa watu Mabalozi wetu, watumishi wetu wa ubalozi ambao ni pungufu wamebeba mzigo mkubwa lakini wawakilishi hawa wanadai Serikali, kuna nini hapa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau kuna neno umelitamka ambalo si neno la Kibunge ni neno la kuudhi. Huwezi kusema Serikali imefanya kitu halafu ukatamka neno hilo la *shame*. Kwa hiyo, naomba ulifute.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nalifuta.

**NAIBU SPIKA:** Hapana, tamka kwa maneno yako kwamba hilo jambo unalifuta.

***MHE. FELISTA D. NJAU:*** *Mheshimiwa Naibu Spika, niseme ni aibu.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**NAIBU SPIKA:** Futa neno lako hilo. Futa neno lako hilo. Si umeshafuta?

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimefuta.

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsante. Tuendelee. *(Makofi)*

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, badala yake niseme inasikitisha sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea. Madai ya watumishi katika balozi zetu ambayo ni sebule *(reception)* ambayo tunawapokea wawekezaji na watalii, tuwaangalie kwa jicho la huruma. Kwenye ripoti ya CAG imeainisha balozi nne ambazo zinadai Shilingi milioni 684.17, ni fedha nyingi. Labda niziainishe kwa haraka haraka; ni Ubalozi wa Paris, Ufaransa ambao unadai Shilingi milioni 83.2; Ubalozi wa Kuala Lumper, Malaysia unadai Shilingi milioni 67.3; Ubalozi wa Kinshasa, Congo unadai Shilingi milioni 243; Ubalozi wa *Pritoria, South Africa* unadai Shilingi milioni 290. Jumla yake ni Shilingi milioni 684.17. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu wenye mzigo mkubwa ambao hawatoshi, lakini bado wanadai marupurupu, wanadai posho zao na malimbikizo yao ya mshahara, na bado wanatakiwa waende mbele kupambana; nafikiri kama sijakosea, kwenye Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 zinaelekeza,

kama kuna watumishi wanadai malimbikizo, marupurupu, posho, kupanda vyeo, walipwe mara moja. Kanuni hii imekiukwa kupitia balozi hizi. Tunaendaje kuwabana wakafanye kazi kubwa namna hiyo wakati hata fedha zao hawajapewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anapokuja hapa aeleze ni mkakati gani madhubuti wa kwenda kulipa madeni haya ili balozi zetu ziweze kufunguka na Tanzania iweze kupata neema?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunaongelea haya, ni kwa maslahi mapana ya Taifa letu, ni kwa maslahi ya nchi yetu ambapo tumeona Kiongozi Mkuu Jemedari ametangulia mbele na wengine wapo nyuma wanarudi nyuma, tukamshike mkono twende wote pamoja. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililila kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunakwenda kwa Mheshimiwa Mussa Sima, jiandae Mheshimiwa Songe na Mheshimiwa Gambo.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema. Pia nachukua fursa hii kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya. Pia nakipongeza Chama changu cha Mapinduzi kwa maelekezo yote ambayo

Katibu Mkuu anatupatia, tunamshukuru sana. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na timu nzima ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na elimu. Naipongeza Serikali, kwani kama kuna eneo ambalo wametutua mzigo sisi wazazi ni ili eneo la elimu bila malipo kwa Watoto. Ila elimu imegawanyika sehemu mbili; tuna elimu nyoofu na *alternative education.* Elimu nyoofu kutoka Darasa la Kwanza mpaka Kidato cha Sita, watoto hao watasoma bila kulipa ada, na akienda Chuo Kikuu maana yake anapata mkopo. Hao *alternative education,* ni wa vyuo vya kati na wote tunawahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nataka niiombe Serikali, tunajenga sana *VETA,* lakini pia tuna vyuo vya kati vya kutosha na vijana wengi wanakwenda hata akipata *Division One* anataka kwenda chuo cha kati akasome *Nursing*, Maabara, Ufundi wowote ili aweze kupata ujuzi. Nchi yetu leo inawahitaji vijana wenye ujuzi ili tuweze kutoka hapa tulipo, lakini tukimsubiri kijana amalize aje na maarifa, hilo ni jambo moja, lakini jambo la pili, amkute kijana mwingine mwenye ujuzi yuko tayari anaendelea na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niiombe Serikali, Mheshimiwa Waziri amesema vizuri, tutawasaidia pale itakapopatikana fedha, lakini tunaweza kutumia utaratibu mzuri tu, kwa sasa tukapunguza ada ambayo inatolewa kwenye vyuo vyetu vya kati ili wazazi waweze kuwasomesha watoto wao walio wengi na sisi tunawahitaji. Nataka niombe eneo hili tulifanyie kazi, nami nimekuwa *pioneer* sana wa kuhakikisha vyuo hivi vya kati

tunavithamini sana, na ili uchumi wetu uendelee, unahitaji vijana wenye ujuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine hapa ni la *MSD,* upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Serikali imetenga Shilingi bilioni 200, ni jambo jema sana, na niipongeze sana. Mwaka 2021 walitenga Shilingi bilioni 218, wametoa zaidi ya Shilingi bilioni 160, hili ni jambo kubwa sana, nimpongeze sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni imani yangu fedha iliyobaki wataimalizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunazungumzia maisha yetu, tunazungumzia afya ya Watanzania, upatikanaji wa dawa umekuwa bado ni changamoto. Hii Shilingi bilioni 200 inayowekwa, inawekwa kwa *projection* ipi? Nataka hapa Serikali tujaribu kuangalia, maoteo ya dawa yanatoka wapi? Ukiangalia katika zahanati tulizonazo, zaidi ya zahanati 7,000 za Serikali hakuna mfamasia wala *pharmaceutical technically* hakuna, unawezaje kupata maoteo ya dawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama huna wafamasia; nchi nzima una wafamasia asilimia 22 tu, na wanafanya kazi kubwa, lakini tuna *deficit* ya wafamasia asilimia 78 zaidi ya wafamasia 35 wanatakiwa kuwepo nchini. Nataka kuishauri Serikali katika eneo hili, wanaofanya kazi ya *dispensing* kule kwenye zahanati zetu kutoa dawa, ni *medical attendant*. *Medical attendant* wameajiriwa kama wahudumu wa afya, siyo kama manesi, siyo kama watoa dawa, lakini wanafanya kazi zote kwenye zahanati zetu. Leo tunapozungumza hivi, sasa Serikali inapaswa kuwekeza hapa; ukiona dawa nyingi zime-*expire* ni kwa sababu yule *medical attendant* hatujamfanyia *training,* awezi kujua

*inventory* ya kuingiza na kutoa dawa. Hata dawa zile tunazozileta leo, maana yake anapaswa afanyiwe *training*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo nataka Serikali ilitazame vizuri jambo hili. *Medica attendant* kama hujamfanyia *capacity building,* wewe unawezaje kupata maoteo ya dawa? Unawezaje kujua dawa leo Watanzania wanataka dawa, unatenga Shilingi bilioni 200? La hasha! Lazima tuwe na *projection* inayotokana na hao watu. Tukawafanyie *capacity building,* tutenge fedha, tuwape uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja kubwa, wengi wanasoma mwaka mmoja na *certificate* ili tu-*cover* hili, lakini Serikali imefuta *NTL Level IV*. *NTL Level IV* ilikuwa inawawezesha vijana wetu kuweza kusoma *certificate* kwa mwaka mmoja na wakaenda ku-*cover* haya ma-*gap*. Unampeleka *NTL Level V* ambayo inamtaka kwenye somo la sayansi awe amepata C, sasa kwa mazingira gani ya shule zetu tulizozianzisha na maabara zetu hazina vifaa, mtoto anaweza akapata C halafu akarudi kwenda kusoma *alternative education?* Hili jambo bado ni gumu sana. Bado huyu atakayepata C, kwa nini asiendelee na elimu ambayo ni ya bure ya kidato cha tano na sita na huko atapata mkopo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali tuje na mpango na Wizara ya Afya waje watuambie wanapata wapi maoteo ya dawa? Inawezekana mahitaji yetu ya dawa ni karibu shilingi bilioni 500, tunatenga shilingi bilioni 200, ndiyo maana tatizo hili linaendelea kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine muhimu sana ni suala la utalii. Hakuna ubishi baada ya janga la *Corona* utalii wetu ambao ulikuwa unachangia *GDP* ya asilimia 27 umeshuka mpaka asilimia 17. Hili jambo limekuwa ni kubwa mno, ambapo sasa mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu ameamua kuingia *field* na kuja *Royal Tour* kwa ajili ya kuonesha kwamba utalii wetu ndiyo sehemu kubwa ambayo sisi tunaitegemea ili iweze kuongeza kipato kwenye uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa tumeshuka, nini sasa kinafanyika? Watalii wanataka mambo mawili tu. La kwanza, *political stability,* wanataka hali ya usalama na amani. Jambo la pili, wanataka ukarimu. Sasa leo tunapokwenda kuimarisha utalii wetu ambao tunajua kabisa ndiyo msingi wa pato letu, ndiyo unachangia kwa kiasi kikubwa ili tufike kwenye *GDP* ya asilimia 30. Lazima sisi Watanzania tuwe pamoja. Utalii hapa huwezi kuzungumza Ngorongoro na Loliondo peke yake, utalii hapa kama tunatokea sehemu ambayo inaonesha hakuna usalama, maana yake watu hawawezi kwenda Moshi, hawawezi kwenda Manyara, hawawezi kwenda Mara, hawawezi kwenda popote. Tayari Tanzania itakuwa inaonekana, huku kuna tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri maeneo machache. Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa maelekezo mazuri, nami nampongeza sana kwamba wale ambao wako tayari kuondoka, wanaondoka na mazingira yameandaliwa. Hili ni jambo jema sana. Hili la kwanza; la pili, ni lazima tuajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii ili ku-*improve relationship* ya wakazi wa eneo hilo. Watu wanapotoka kwenda eneo lingine, bado tunaweza

kuzalisha eneo lingine kule kama hatujaweka mkakati kuwa na Maafisa Maendeleo ya Jamii; na wale wanaobaki kama hatuweka mkakati kuwa na Maafisa Maendeleo ya Jamii, tusitarajie kwamba tutakuwa na mahusiano mazuri. Bado hapa hali ya usalama itakuwa hatarishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la utalii; utalii ni biashara, lazima tuajiri ma-*CEOs*. Sasa kama mtu anabaki na *game reverse,* yeye abaki kwenye *conservation,* lakini tuajiri ma-*CEOs* ili waweze kutusaidia kufanya biashara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, hili eneo ni muhimu sana. Nasi Watanzania tuungane kwa pamoja bila kujali tofauti zetu, lakini tunataka kuinua uchumi wetu. Uchumi huu kwenye utalii ndiyo eneo kubwa sana tunatakiwa tulisimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ulikuwa Waziri wangu, ulinituma kwenda kwenye ile timu ya Mawaziri nane. Kama kuna eneo la uhifadhi tulilisimamia lilikuwa la *Lake Natron. Lake Natron* tumelitenga kama eneo tengefu. Eneo tengefu linakuwa na pande mbili; upande wa kwanza litahifadhiwa, lakini upande wa pili matumizi ya binadamu yanaendelea, kama tunavyofanya kwenye Ziwa Rukwa. Kwa hiyo, sasa ile ripoti ambayo ilikuwa ya Mawaziri nane wakati ule, ndiyo ripoti pekee inayoweza kutoa suluhu ya haya matatizo ambayo yanaendelea sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niguse eneo lingine la *CAG*. *CAG* ametengewa fedha kwa ajili ya kuongeza kazi yake anayoifanya na anafanya kazi nzuri sana, lakini *CAG* anafanya *compliance*. Sasa tunamwongezea fedha kwa

ajili ya kwenda kufanya *postmortem*. Nadhani mnanielewa ninavyozungumza *postmortem*. Tayari *postmortem* unaenda kuangalia huyu marehemu amekufa kwa sababu ya nini? Unaenda kuangalia chanzo cha kifo cha marehemu, badala ya kwenda kumsaidia huyu asiweze kufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa fedha tuliyotenga imwezeshe *CAG* kuwa *pro-active*. *CAG* hawezi kubaki kuwa *reactive*. Tumefanya vizuri kwa *Internal Auditor* tumefanya vizuri sana wawe wanafanya kazi kwa wakati wote, lakini *CAG* anapoenda kufanya kazi, sisi mzunguko utoke kwenye Kamati, ije Bungeni, tufanye maazimio; *too late to catch the bus.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali hii, fedha tuliyotenga tumsaidie *CAG* aende awe *pro-active* ili atusaidie matatizo yasitokee, tusije tukawa tunasubiri matatizo yanatokea, tunakuja kujadili matatizo yameshatokea. Mtu unayeenda kumhukumu, hayupo; ameshahama, ameacha kazi, amestaafu. Huko hatuwezi kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie eneo muhimu sana. Mwaka 2021 Mheshimiwa Waziri alieleza juu ya Madiwani, kaeleza vizuri sana. Hawa wanafanya kazi nzuri na uzalishaji ni mkubwa na ndio wanaosababisha mapato ya ndani yanakuwa makubwa. Akatumia neno zuri sana, Wabunge wakaazi wa kata, na akasaidia, lakini ukiacha Halmashauri 16, nyingine zote Serikali iliamua kulipa posho yao na mpaka leo hatuna mgogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niiombe Serikali eneo jepesi sana. *Own source* zetu tunazozalisha kwa kiwango kikubwa kwenye mapato yetu ya ndani hatuwezi kushindwa kuweka *responsibility allowance* kwenye *own source*. Tunataka Serikali itoe tu maelekezo ya fedha ya madaraka kama tunavyotoa kwa Maafisa Elimu wa Kata, kwa Watendaji wa Kata, kote Serikali inatoa. Ila Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Kata, yeye hana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiweka *responsibility allowance* kwenye *own source* zetu ambayo ianze tu kuanzia Shilingi 200,000/= na kuendelea kulingana na mapato yao; ukiweka Shilingi 200,000/= kwa Singida Mjini, maana yake utakuwa unatenga Shilingi 4,600,000/=, haiwezi kushindikana. Naiomba Serikali iweze kuliangalia eneo hili ili liweze ku-*promote,* ili liweze kuwasaidia hawa wafanye kazi kwa ufanisi. Hapa tunazungumza uwajibikaji wa pamoja na uwajibikaji huu lazima twende kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda kwa haraka ili tufike mahali tukubaliane. Sisi ni wazalishaji wa alizeti, Serikali leo imeamua kuwekeza kwenye eneo hili. Tuna kiwanda kikubwa sana cha *Mount Meru* ambacho tangu kimeanza kazi hakijawahi kutosheleza mahitaji. Kwa nini? Ni kwa sababu viwanda vyetu vingi vinavyoanzishwa, hawa wawekezaji wanaokuja kuanzisha hawafanyi *contract farming*. Wewe unaacha mimi nizalishe, leo mimi naenda kwenye njaa, siwezi kulima alizeti kwa wingi kwa sababu ni zao la kibiashara, nitalima zao la chakula ili niweze ku-*survive*. Sasa nini kinatakiwa kifanyike?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itoe malekezo kwa wawekezaji wote hawa wanaoanzisha viwanda wawe na *contract farming*. Nenda umsaidie mwananchi mwenye eneo, mpe pembejeo, hakikisha unamsaidia, unawapa na watalaam na kila kitu, uzalishaji utaongezeka, na soko hili la mafuta litakuwa ndiyo soko kubwa ambalo litawasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna ubishi kwamba asilimia 10 imewasaidia sana Watanzania. Leo tunapoenda kuigawanya; tano inaenda kwenye eneo ambalo ni wajibu wa Serikali, suala la kujenga masoko ya Wamachinga, hii ni kazi ya Serikali, lakini asilimia 10 ni fedha ambayo tumeiandaa sisi. Tumekusanya kwenye vyanzo vyetu, tumeamua sasa asilimia 10 iwasaidie akina mama, vijana na pia watu wenye ulemavu. Mpaka sasa hamjatuambia, tumefanikiwa kwa kiwango gani? Tumefeli wapi? Hatuwezi kukimbia tatizo. Ila kama ndivyo, mtuambie tumeamua kwenda huku kwa sababu hawa watu wamewezesha. Sasa kama tunaamua kuweka *TIN,* umeweka *TIN* halafu unaenda kuwapata watu gani wanaoweza kufanya *productivity* kama sio hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali, hii asilimia 10 tena sisi tulikuwa tunawaza iongozwe, kwa sababu mapato tunakusanya wenyewe, sasa tunaitoa 5% inaenda kufanya kazi ya Serikali ambapo kazi hii ni wajibu wake Serikali kujenga masoko, kufanya nini, kutenga na kila kitu. Naiomba Serikali kwenye eneo hili tuachieni sisi tuka-*improve* maisha ya watu wetu, kwa sababu ndiyo eneo kubwa ambalo linatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Serikali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa nampa nafasi Mheshimiwa Songe, jiandae Mheshimiwa Gambo na Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami kuchangia hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa bajeti nzuri sana ambayo ametuletea mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wakati anatoa hotuba yake kuna sehemu nyingi sana alizoelekeza na alizosema za kupunguza matumizi, lakini kuna sehemu moja ambayo hakuitaja ambayo naona ni ya muhimu sana ya kupunguza matumizi katika nchi yetu. Eneo hili ni kupunguza matumizi ya Serikali ya eneo la riba na faini ambazo inatozwa Serikali kutokana na ucheleweshwaji wa malipo kwa wakandarasi na wazabuni. Eneo hili ni eneo muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakandarasi wana *charge interest* kwa Serikali kwa sababu tumechelewesha kuwalipa. Kama hatutabana hii sehemu, maana yake tutaendelea kuiingizia Serikali hasara, tunaendelea kupandisha miradi thamani yake, lakini pamoja na hayo, Serikali inazidi kupata hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mifano. Ukisoma ripoti ya *CAG* ya mwaka wa fedha 2020/2021 iliyotolewa Machi 22, inaeleza; ukisoma ukurasa wa 52 na 53 wa Hesabu za Mashirika ya Umma, utaona tulichajiwa *interest* na faini ya

Shilingi bilioni 95.2 ambapo *TANESCO* ilikuwa shilingi bilioni 10.4, *ATCL* ilikuwa shilingi bilioni 16.8 na Bodi ya Mikopo ilikuwa shilingi bilioni 68. Fedha hizi ni nyingi kwa Serikali. Ukienda kwenye Hesabu ya Serikali Kuu, utakuta *TANROADS* walichajiwa shilingi bilioni 68.7 na *TARURA* walichajiwa shilingi bilioni 0.88 sawa na shilingi milioni 880. Fedha hizi ni nyingi, lazima twende tukaziokoe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sasa Wizara kutazama kwa kina Hazina ili kuweza kutoa mlolongo uliopo mkubwa katika namna kubwa sana ya ku-*approval* malipo kwa Wakandarasi wetu. Tuki-*solve* hili eneo tutaokoa fedha nyingi sana kwa Taifa letu, tutaokoa fedha nyingi sana kwa nchi yetu. Namaanisha nini? Ukienda kwa mfano, Kamati yetu ilienda pale *TPA* tukakuta wamepigwa faini ya kuchelewa kulipa, ya shilingi milioni 980. Fedha hizi ni nyingi, lakini ukiuliza sababu utaambiwa kwamba Hazina ilichelewesha malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia, tunapata mikopo ya watu wa Benki ya Dunia, tunaposaini mikataba, yaani *financial agreement*, Benki ya Dunia huwa inaleta fedha zote inazipeleka Hazina. Sasa kigugumizi cha kulipa Wakandarasi kinatoka wapi? Kwa nini hatuwezi kulipa wakandarasi kwa wakati ili kuondoa hii gharama ya kulipa *interest? Implication* yake ni nini katika hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, implication yake ni kwamba inawezekana kuna viongozi kwenye ofisi wanachelewesha kwa makusudi ili watakapotoa fedha hizi waweze kupata mgawo. Hii ndiyo *implication* ya tatizo hili. *Implication* ya pili, Wakandarasi wameshatugundua sasa kwamba Watanzania wao hawalipi kwa wakati, tutachaji interest.

Kinachofanyika sasa wanapofanya *quotation* ya kazi wana-quote kidogo wakijua kwamba watakuja wafidie pale kwenye *interest.*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni muhimu sana Wizara ya Fedha kuliangalia. Nendeni pale Hazina, kama kuna issue zinasumbua, fumueni utaratibu, leteni tuwapitishie hapa, tuokoe fedha nyingi ambazo tunaingia gharama bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la pili ambalo nataka kuchangia, ni kuimarisha mashirika ya Serikali yanayozalisha na kupata kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuchukulie mfano Shirika letu la *TPDC,* katika uagizaji wa mafuta mwezi Mei, 2022 mafuta yaliyoingia nchini ya *diesel* yalikuwa *metric ton* 346,631. Katika hii Shirika letu la *TPDC* lilipewa *metric ton* 111,000 sawa na asilimia 32, ukiuliza wanakuambia hawana mtaji! Leo lazima tukubaliane tupeleke mtaji katika Shirika letu ili liweze kuagiza mafuta mengi na tuweze kupata faida Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma taarifa ya fedha utaona kwamba tayari wameshapleka gawio Serikalini zaidi ya Bilioni Tisa katika miaka mitatu, sasa kama hatuwezi kuwapelekea mtaji watapata wapi gawio la kuleta Serikalini ni lazima sasa tuone namna ya kuwapa fedha ili waweze kufanya biashara na tuweze kupata gawio Serikalini. Haya ni mambo ya msingi yatakayoenda kutupatia fedha katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo ukiangalia kuanzia 2004 Julai, mpaka Mei, 2022 *TPDC* wameokoa Trilioni 41 wa kutumia gesi asilia, lakini ukisoma taarifa inaonesha mpaka sasa hivi wanaotumia gesi asilia ni asilimia 10 bado asilimia ni ndogo sana. Kama tumeweza kuokoa Trilioni 41.3 sasa haya si ni mahesabu tu ya kawaida *comrade* Mwigulu, kwamba sasa tupeleke fedha nyingi *TPDC* ili tuweze kuokoa fedha nyingi na baadae tupeleke fedha kwenye mzunguko ndiyo *logic* ya hii Habari! Kwa hiyo tulione suala hili ni la msingi sana, kama tumeokoa Trilioni 41 na bado ni asilimia 10, Je, tutaokoa kiasi gani kama tutafikisha asilimia 60 hii ni hesabu ya kawaida twendeni tukaliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la Tatu ni kuangalia sekta za uzalishaji. Ninaipongeza sana Serikali kwa kuja na mkakati wa sekta ya kilimo kwa ajili ya uzalishaji. Niseme tu kwamba sababu mojawapo inayosababisha ongezeko la bei kwenye bidhaa mbalimbali ni kutokuwepo uzalishaji mkubwa wa mazao ya nchi husika. Tusipozalisha kwa wingi hapa nchini maana yake bei za mazao zitaendelea kuwa kubwa kwa sababu tunategemea kuingiza kutoka nje. Nini kifanyike, tunatakiwa tuzalishe kwa wingi hapa nchini ili tuweze nasi kuuza kwa wenzetu, tukienda mbali zaidi tuweze kutumia hapa nchini kwetu tuzalishe *final product* na hizi *final product* zikaweze kutumika katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano kule Simiyu tunalima sana pamba lakini tunalo andiko kubwa ambalo limekuja Wizara ya Fedha la kutengeneza kiwanda kikubwa Simiyu kitakachozalisha vifaa tiba vitokanavyo na pamba. Vifaa tiba hivi vinaenda kuokoa fedha zaidi ya Bilioni 147 ambayo

tunatumia sasa kuagiza vifaa tiba huko nje. Sasa kwa nini tusizalishe hapa tutengeneze kiwanda, tuzalishe sisi wenyewe na tutumie, hii itaokoa fedha nyingi ambazo tunapeleka kule nje. Pia zaidi ya wananchi 1,000 wanaenda kupata ajira, kule Busega watapata ajira, kule Bariadi watapata ajira, kule Iramba watapata ajira. Kinachotakiwa sasa kufanyika ni kuwekeza eneo hili ili wananchi wetu waweze kupata ajira na tuokoe fedha nyingi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo itakuwa sasa mantiki ya kuwepo kwa reli, huwa najiuliza swali moja huko nyuma kwamba kwa nini tunajenga reli wakati hatujaenda kuwekeza katika sekta za uzalishaji, hii reli inaenda kusafirisha nini? Lazima tuwe na mipango, reli siyo ya kusafirisha watu peke yake, reli ni ya kusafirisha pia mizigo ya kusafirisha mazao. Mantiki ya kutengeneza reli ni pamoja na usafirishaji kama tunatengeneza reli kwa ajili ya kusafirisha watu hatutarudisha huo mkopo. Ni lazima sasa twende mbali zaidi tunatengeneza reli na mwisho wa siku huko reli inakoenda kuna uzalishaji gani. Kama reli inaenda Mwanza kuna uzalishaji gani kule Mwanza, kama reli inaenda Kigoma kuna uzalishaji upi kule Kigoma ambao sasa tutatumia katika suala zima la usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Songe. Sasa Mheshimiwa Gambo, ujiandae Dkt. Chaya, jiandae Mheshimiwa Mtemvu na Mheshimiwa Manyinyi pia ajiandae.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru sana kupata nafasi ya kuweza kuchangia kwenye Bajeti Kuu ya Serikali na nitajielekeza kwenye maeneo matatu, kwenye upande wa maduka ya kubadilisha fedha, kubana matumizi ya Serikali na *Tanzanite*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, *BOT* ina *double standard,* tunafahamu kwamba kwa muda mrefu imekuwa inapuuza maelekezo ya Serikali. Tumemsikia Waziri wa Fedha kupitia Bajeti ya Wizara ya Fedha ameonyesha umuhimu wa maduka haya ya kubadilisha fedha hasa kutokana na kazi nzuri aliyoifanya Rais wetu kwenye sekta ya utalii. Kuna Kampuni inaitwa *Kadoo Bureau De Change* inafanya kazi zake Dar es Salaam na Arusha imepewa kibali na *BOT*, pia kampuni nyingine nyingi zenye sifa zilizoko Arusha zimenyimwa leseni na *BOT* kwa sababu ambazo hazieleweki na vigezo wameshakidhi, inaonekana kwamba huyu mwenye hii Kampuni wa maslahi naye ndiyo maana wamemuachi na kuzuia wengine ili aweze kufanya biashara peke yake. Tunadhani hili jambo siyo sawa na siyo jambo jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Rais ametoa malekezo akiwa Kagera, kwamba wenzetu wa *TRA* wanapofuatilia kodi wasiende miaka zaidi ya miwili, lakini kwenye hawa wetu *Bureau* bado wanakwenda kuwauliza taarifa za mwaka 2015 mpaka 2016 ili tu kuwatafutia sababu na mwisho wa siku wawanyime fursa hiyo ya kufanya biashara kama wenzao wanavyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi utalii umeongezeka hoteli zimejaa mpaka mwezi Desemba na kuendelea,

Ndege nyingi zinaingia usiku tunategemea watalii wanapofika wasipate changamoto ya kubadilisha fedha. Kwa sababu ukileta urasimu wa namna hii mnasababisha pia wakati mwingine kuwa na *black market* katika maeneo mbalimbali, badala ya ku-*change* fedha kwenye maeneo rasmi wana-*change* kwenye maeneo binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia changamoto nyingine kubwa katika jambo hili ambalo tunaomba *BOT* waliangalie ukiritimba nao ni mkubwa sana. Unapokwenda Benki kwenda kubadilisha fedha ni tofauti na kwenye *Bureau* wanataka wajue je unayo akaunti, je kama hauna akaunti umetoka wapi na maswali mengine mengi, lakini ukienda kwenye *Bureau* taratibu zinakuwa rahisi zaidi. Tunaomba *BOT* waache urasimu, kama wana watu wao wanawataka wawape lakini pia na Watanzania wengine wenye sifa wapewe kama watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kuhusu kubana matumizi ya Serikali. Kwanza naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na kwa usimamizi wako Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yako yote, kwenye kuhakikisha magari ya Serikali kwa kiwango kikubwa mnakwenda kuyadhibiti kwa sababu ni kweli gharama zimekuwa kubwa. Lakini kuna eneo jingine pia naomba tuliangalie, angalia kwenye Halmashauri zetu, ukienda Halmashauri za Dar es Salaam, Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam mapato yao ya jumla makisio yao ni bilioni 81, lakini mapato yasiyolindwa ni bilioni 62.2 ukichukua asilimia 70 ambayo inatakiwa iende kwenye maendeleo ni sawasawa na bilioni 43.587, lakini *other charges,* yale matumizi ya kawaida posho, kaweka mafuta kafanya hivi ni Bilioni 18 kwa Halmashauri moja kwa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Halmashauri kama ya Dodoma makisio yao ni Bilioni 55, mapato yasiyolindwa ni bilioni 44, ukichukua asilimia 60 ni bilioni 26, *other charges* matumizi yale ya kawaida ya kila siku ni kama bilioni 17. Ukichukua Halmashauri ya Kinondoni hivyo hivyo bilioni 57 ya asilimia 46, maendeleo 32, matumizi ya kawaida bilioni 14. Ukienda Jiji la Arusha mapato yetu ni bilioni 30 makisio, mapato yasiyolindwa bilioni 24, asilimia 70 kwenye maendeleo ni bilioni 17, matumizi ya kawaida ni bilioni saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona mfano mmoja Jiji la Arusha kwa mapato haya ya Bilioni Saba tu wameweza kuingiziana fedha kwenye akaunti binafsi, tumeona aliyekuwa Mkurugenzi wakati huo Ndugu John Pima kachukua milioni 103, kamuingizia Mchumi Innocent Maduhu milioni 103 kwenye akaunti yake binafsi. Mchumi kachukua milioni 25 kaenda kununua gari Subaru kwa matumizi yake binafsi na ushahidi upo. Mkurugenzi kachukua fedha kamuingizia kijana anaitwa Ndugu Alex milioni 65, mwingine milioni 65, unaona hizi fedha ambazo mnazijazia hizi Halmashauri na hizi asilimia zenu zinakwenda kunufaisha watu na siyo kunufaisha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba tunaomba Wizara ya Fedha wakae na TAMISEMI badala ya kusema waangalie asilimia waangalie matumizi halisi. Ukichukua hizi bilioni 18 za Halmashauri ya Dar es Salaam ni sawasawa na ukichukua Halmashauri ndogo 14, ukichukua Halmashauri ya Mbulu, Halmashauri ya Gairo, Halmashauri ya Butiama, Halmashauri ya Rorya, Kigoma, Kakonko, Buhigwe, Nsimbo, Bumbuli, Mbogwe, Mlele, Momba, Madaba na Halmashauri ya Ileje. Halmashauri 14 hizi

matumizi yao ya kawaida kwa mwaka mzima ni bilioni 9.9. Matumizi yao ya kawaida kwa miaka miwili ndiyo matumizi ya Jiji la Dar es Salaam ya kuweka mafuta, kulipana posho na masuala mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hapa kuna haja ya Serikali kwenda kuangalia kazi nzuri kwenye magari lakini turudi pia kwenye matumizi ya kwenye Halmashauri zetu. Rais anafanya kazi kubwa sana, anakwenda kutafuta hela Dunia nzima, anabana matumizi kila mahali, lakini Waziri wa TAMISEMI na Waziri wa Fedha msaidieni Rais kupitia matumizi haya ya Halmashauri zetu ili tuweze mwisho wa siku kupata fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasi Arusha hapa kwa nilivyoangalia wanavyo kulakula hawa wakipewa hata Bilioni Tatu, Nne zinawatosha, hii Bilioni Tatu nyingine au Nne zinazobaki tuende tukajenge barabara kwa sababu changamoto ya barabara ni kubwa sana, tukanunue vifaa kwenye Vituo vya Afya na tukapeleke huduma mbalimbali kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba pia kutoa mchango wa mawazo kwenye eneo hilo na ni imani yangu kwamba wenzetu wa TAMISEMI watatusaidia. Kwa sababu hizi hela zinaliwa sana nikitaka niseme mnyororo mzima hapa wa namna ambavyo hizi hela za Arusha zilivyoliwa na zilivyogawana hapa ndani kuna wengine tutapoteana kwa sababu changamoto ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la tatu ni kuhusiana na Madini ya *Tanzanite*. Hili jambo nimekuwa nalisema kila siku na kila nikilisema nadhani sieleweki. Watu wa Arusha hatukatai madini ya *Tanzanite* kuuzwa Mererani kwa sababu Mererani ndiyo yanakochimbwa.

Tunachokisema sisi yakishachimbwa yale madini kwa sababu lengo la kujenga ule ukuta ni kuzuia utoroshaji, yakishichimbwa na Serikali iko pale na vyombo vyote viko pale waangalie kodi zote za Serikali ambazo mwekezaji anatakiwa kuzilipa, kwa sababu akishalipa anaruhusiwa kusafirisha haya madini kupeleka kote Duniani. Akitaka kupeleka India anapeleka, akitaka kupeleka Marekani anapeleka na sehemu nyingine zote, lakini eti haruhusiwi akishalipa tozo zote kupeleka Arusha, kupeleka Dar es Salaam, kupeleka Mwanza, kupeleka na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanachokifanya wafanyabiashara anakwenda pale Mererani anachimba madini yake, anapata vibali vyote, anafungua Ofisi yake Dubai, anafungua Ofisi yake India, anafungua Ofisi yake Kenya, anasafirisha madini anakwenda kuyachakata kule halafu anakuja kwenye *border* zetu anayapitisha kuja kuyauza Arusha na maeneo mengine. Sasa tunayafanya haya kwa kumunufaisha nani? Sisi hatukatai mambo haya kupelekwa Mererani lakini tuangalie mtu akishalipa kodi kama anaruhusiwa kupeleka India kwa nini haruhusiwi kupeleka Arusha, kupeleka Dar es Salaam, kupeleka Mwanza, Zanzibar na maeneo mengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wakati huu wa utalii, watalii ni wengi sana mtu anakuja amekwenda kuangalia Pundamilia, kaangalia Simba na wanyama wengine, akitaka kurudi nyumbani anataka arudi na zawadi, anakwenda kununua Tanzanite kama zawadi anapeleka kwa ndugu zake kule nchi alikotoka. Leo haruhusiwi kufanya kitu cha namna hiyo! Kwa hiyo, naomba Wizara ya Madini waliangalie jambo hili kwa uzito unaostahili, kwa sababu

kwa kweli changamoto hii ni kubwa na mambo haya yanahitaji uzalendo wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa fursa hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Dkt. Chaya, jiandae Mheshimiwa Mtemvu, jiandae Mheshimiwa Mathayo, jiandae Mheshimiwa Tumaini Magessa, jiandae Dkt. Kimei.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nachukua fursa hii kushukuru sana kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia, kipekee sana nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya, katika Jimbo letu la Manyoni Mashariki ameweka *impact* kubwa sana. Nichukue nafasi hii nimshukuru sana Dkt. Mwigulu Nchemba na Naibu Waziri wako kwa kazi kubwa kwa kuja na bajeti ambayo ina ubunifu mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nina mambo takribani matatu ya kuchangia, eneo la kwanza nitachangia kuhusu tathmini ya vyanzo vya mapato ambavyo tulipitisha mwaka uliopita, nitachangia kuhusu namba ya mlipa kodi *(tax identification number)*, nitachangia vilevile kuhusu ile asilimia 10 ya mapato ya Halmashauri inatokana na asilimia 40 ya maendeleo na mwisho nitachangia kuhusu suala la mishahara binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba mwaka jana tulipitisha vyanzo vya mapato, mojawapo ya vyanzo vya mapato tulipitisha tozo kwenye miamala ya simu na wewe ulikuwa kinara uliita tozo ya uzalendo. Pia tulipitisha

mfumo wa kubadilisha ukusanyaji wa kodi za *property tax*, kutoka *TRA* lakini tukapeleka kwenye mfumo wa *LUKU*. Sasa sikusikia kwenye taarifa yako Daktari kwamba kwa kiwango gani tumeweza kufanikiwa na hivi vyanzo ambavyo tulivi-*propose* ili sisi itusaidie kuja na mfumo ambao tunaweza tukaboresha zaidi *whether* tunahitaji kuendelea na miamala ya simu na *efficacy* yake ilikuwaje, vilevile kodi ya majengo ni jinsi gani imekuwa *effective*, niliona hilo nimshauri Waziri anapokuja ku-*wind up* tujue kwamba *to what extent* hizo tozo na hizo kodi zimekuwa *effective* na unashauri nini tuendelee nazo au zibaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni suala la Namba ya Mlipakodi. Kumekuwa na sintofahamu kubwa na kumetokea taharuki kwa wananchi, lakini mimi naomba niwatoe mashaka, nimepitia nchi mbalimbali ambazo zinatumia *TIN Number* katika mazingira tofauti. Kwa mfano, *UK* wana kitu kinaitwa *National Insurance Number (NINO)* ile *NINO* ndiyo inatumika kama *substitute* ya *TIN Number*. Nchi ya *Hong Kong* wenye hawana *ID* zingine wanaita *Hong Kong Identity Card* ileile *Hong Kong Identity Card* ndiyo inatumika kama *TIN number, the same to Pakistan*, *the same* kwa *USA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema nini hapa? Kwanza niseme *idea* aliyokuja nayo Daktari Mwigulu Nchemba *is the valid idea* na tumechelewa sana. Tumechelewa kwa sababu gani, nilitegemea kwanza tuondoe utitiri wa vitambulisho tulivyonavyo, mimi nina vitambulisho zaidi ya vitano vyenye Namba nina cheti cha kuzaliwa, nina *employers ID number*, nina *Social Security Number*, nina Leseni ya Udereva na zingine huu ni utitiri mkubwa sana. Nchi zingine wanachofanya mtoto

anapozaliwa anapewa *TIN number* ile *TIN number* inakuwa *the same* kote huko, ukimwajiri atatumia *the same TIN number*, kwenye *social security* atatumia *the same TIN number*. Lakini kumekuwa na upotoshaji mkubwa kwenye mitandao, watu wanajua hii *idea* ya *TIN number* ni kwamba watu wanakuja kulipa *head tax*, kodi ya kichwa siyo kweli. Kwa hiyo, mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwamba tu-*harmonize* hii mifumo tusiwe na vitambulisho vingi, kama inawezekana cheti cha kuzaliwa, mtoto anapozaliwa apewe *TIN number* atakutana nayo akishakua mtu mzima huko atalipia kwenye mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nilipenda kuchangia suala la asilimia 10. Nimewasikia Wabunge wenzangu wakichangia asilimia 10, mimi namuunga mkono Daktari Mwigulu Nchemba. Kwanza ninaishukuru Serikali kutenga ile asilimia 40 ya maendeleo kwenye mapato ya ndani, ambapo asilimia 10 tunaenda kukopesha katika ile 4-4-2. Tukumbuke kwamba hizi fedha tunaenda kuzikopesha lakini hawa watu tunapowakopesha hizi fedha hawana miundombinu ya kufanyia kazi, hakuna masoko, hakuna vibanda vya Mama Ntilie kufanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu amekuja na *idea* kwamba badala ya kuchukua yote asilimia 10 uipeleke kwenye mikopo, ambayo nitailezea baadae, ame-*propose* asilimia Tano ya ile hela iende ikaweke miundombinu kwa ajili ya hawa ambao tunaenda kuwakopesha. Unakikopesha kikundi hakina soko, unawakopesha mama ntilie hawana sehemu ya kupika matokeo yake anaenda kutumia gharama nyingi kulipia pango la kile kibanda cha kufanyia biashara. Kwa hiyo, mimi naunga mkono wazo kwamba tuchukue asilimia tano

ya mapato yale ya asilimia 10, tukaweka zile *infrastructure*, lakini kuna *multiply effect* kubwa kwenye hili, watu wengi watanufaika na lile soko kuliko vikundi. Nitakutolea mfano, katika Jimbo langu la Manyoni Mashariki….

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa mchangiaji kwamba dhana kuu ya asilimia 10 ilikuwa ni kuwainua wananchi kiuchumi, lakini hizi asilimia tano anazosema kwamba zinakwenda kwenye miundombinu ya masoko kwamba watu waende kuuza pale, wengine wanakopa wanafuga nguruwe, wengine wanafuga kuku, *products* ambazo haziendi kwenye hayo majengo ambayo anaelekeza. Kwa hiyo, nimependa kumpa tu hiyo taarifa kwamba sio wote wanaokopeshwa wanakwenda kwenye umachinga. *(Makofi)*

**SPIKA:** Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, *partially* naunga mkono hoja ya dada yangu, lakini naomba nimweleze kitu kimoja wale watu wanakopeshwa kwa kutumia *revolving system,* zile fedha zinarudishwa. Nitatolea mfano, kule Manyoni, tumeshakusanya fedha kutoka kwa wale ambao waliokopa, zile fedha zikirudi wanakwenda kukopeshwa wale tena. Hoja yangu ni nini, hatuna miundombinu ya hawa watu katika kufanya biashara. Kwa hiyo, bado naunga mkono kwamba tutenge asilimia tano kwa ajili ya kuwasaidia kujenga masoko, kujenga vibanda ile fedha ambayo inarudishwa itatumika

kwa ajili ya kukopesha na tutaongeza *capacity* ya kukopesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ni la mwisho ni kuhusu hii mishahara binafsi, wenzangu wamechangia kuhusu mishahara binafsi na naunga mkono hoja. Kuna matatizo mawili katika mishahara binafsi hususani kwa wale ambao walitolewa kwenye utumishi wa umma, hususani wale ambao walishushwa vyeo vyao. Kwanza kuna hoja kubwa tatu hoja ya kwanza, huyu mtu wakati anateuliwa je, alikuwa ameajiriwa? Hoja ya pili ni kwamba, je, kama alikuwa ameajiriwa? Tatu, je, alikuwa ameajiriwa wapi ni Serikalini au kwenye *private sector*? Nne, wakati tunamteua nini tofauti ya mshahara wakati anateuliwa na kule alikokwenda? Hizo ndio hoja kubwa nne ambazo tunahitaji kuangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine watu wakishateuliwa anakuwa na mshahara mkubwa, anaamua kwenda kukopa, kwa hiyo, kuna *burden* ya mikopo ambayo mtu huyu anakuwa nayo. Tatizo ni kwamba na nakubaliana nalo kwamba tumekuwa na watu wengi ambao wapo mtaani, wametolewa kwenye mfumo wanapokea mishahara mikubwa ambayo ni *burden* kwa nchi. Kwa mfano, katika halmashauri moja wakati fulani kulikuwa kuna Wakurugenzi wanne wote wanapokea mshahara sawa, hiyo ni *burden* kubwa kwa nchi. Ushauri wangu ya kwanza, tuandae mwongozo mpya ambao sasa utakuja kusaidia *idea* ambayo Mheshimiwa Dkt. Mwigulu anayo kwamba kama mtu ametenguliwa, je… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Dkt. Chaya kwa mchango mzuri.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Mtemvu, wajiandae Mheshimiwa Mathayo, Mheshimiwa Magessa na Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. JUMANNE I. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie katika bajeti hii ya Serikali. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye nchi yetu. Pamoja na kumshukuru Mheshimiwa Rais, lakini ni lazima tuendelee kuwapongeza juzi tu tumetoka kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwenye sekta ya Wizara yake ya Fedha kazi ambayo wanaendelea kufanya kama Wizara pamoja na watendaji wao. Kwa hivyo, leo nitajielekeza katika maeneo kama mawili, matatu kwa haraka jambo la kwanza ni lile ambalo limesemwa na wengi la asilimia 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo hapo kwenye asilimia 10. Wengine wanajaribu kutofautisha kati ya Miji yenye mapato makubwa na halmashauri nyingine. Mimi natoka Dar es Salaam unakotoka wewe, kwenye Wilaya yetu ya Ubungo tunasema asilimia 10 bado tunaweza tukasema ina asilimia 50 kwenye mafanikio na nimewahi kusema humu ndani. Tunatamani kujua uhakiki na tathmini ya ujumla katika kipindi chote ambacho asilimia 10 imefanya kazi, hiyo itatupa matokeo. Niliomba hapa TAMISEMI wakafanye hili jambo, leo tungekuwa tunajua

kwa nini tano, ingekuwa wanatuambia vizuri kwa nini wanazipunguza, tumefanikiwa kwa kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu humu ndani bado zipo taarifa nyingi zimeshapotea fedha nyingi katika hizo asilimia 10. Sasa tunakuwa katika mazingira ya kwamba hatuwezi kufanya maamuzi, je, ni kweli tukubali zipungue au tubaki hapo hapo au tuongeze kama wengine ambavyo wanaona? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia liko jambo tumezungumza juzi na nilikuwa na swali la nyongeza juu ya vijana wengi zaidi ya miaka 35, akinamama wameingizwa katika umri ambao hauna mpaka. Vijana kundi la akinadada wapo katika umri wao katika ujana na pia na wanawake, lakini vijana mwisho miaka 35. Tunajua wajasiriamali hapa ambao tunawazungumza wengi ni zaidi ya miaka 35 mpaka 40 ndio wengi na huo ndio ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiona azma hii ya kuhamisha asilimia tano ni kama vile, wanakwenda kuwatafuta wajasiriamali ambao wengi wamezidi miaka 35. Kwa hiyo, kama huo ndio muono ni jambo jema, lakini inaweza kubaki 10. Katika halmashauri zenye uwezo, ninayotokea mimi nikikubali kwamba 10 zibaki, lakini jambo hili lenye nia njema na wajasiriamali wa zaidi ya miaka 35 waongezewe hiyo tano. Kwa hiyo, ningefurahi kabisa ingeenda hata asilimia 15, kumi zingebaki na tano zingeongezwa, lakini kwa nani wakafanye tathmini. Wale wenye mapato madogo waachwe vile walivyo, wenye mapato makubwa waende kwenye 10 wajumlishiwe na tano ziweze zikawasaidie au hiyo miundombinu ya hao wengine. Ziada kwenye hili niwaombe sana hebu

tukaongeze/tukafungue ule umri pale kwenye hii mikopo, tukaufungue ufike miaka 40 inaweza ikatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye asilimia 10 kuna shida moja ambayo hatuizungumzi. Wananchi wengi wanalia, wapiga kura wetu wengi wanalia. Tunazungumzia asilimia 10 (4:4:2) au hiyo (2:2:1) kwa wajasiriamali wenye biashara, lakini wale ambao wanataka kuanza biashara hatuwataki kabisa na ambao ndio wengi. Sasa hao wanataka kuanza biashara, wanataka mtaji mdogo na sisi hatuwezi kuwapa, tunasema lazima uanze na biashara, ndio maana kuna udanganyifu sasa. Wanatafuta duka la mtu wanakwenda watano, 10 wanasema tukae humu kwako, ili iweze kuja kwa mtu mmoja wakagawane vipande vipande, hii haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Maafisa Biashara, tunao wengi tu katika kila halmashauri yupo, ana kazi gani kama hawezi kutoa elimu juu ya kuanza biashara na akaweza kuisimamia biashara iliyoanza? Uoga wetu ni nini kama nchi? Uoga wetu ni nini katika hili? Ione hii, tushauri Wizara katika bajeti yetu hii, hebu tuone jambo hili, tufungue pale miaka 40, lakini tukaone mitaji hii inayotolewa iende kwa kuanza biashara na sio kwa mwenye biashara. Inasababisha kuwa na manung'uniko makubwa makubwa sana na fedha zinakwenda kwa watu wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye jambo la asilimia 10 hapa naweza nikachomeka jambo ambalo limezungumzwa sana na watu. Kuna jambo la mapato dhidi ya matumizi kwenye halmashauri zetu. Mdogo wangu Mheshimiwa Gambo hapo kaisema katika njia fulani

kaifananisha Dar es Salaam na mimi ndio maana naamua nirudi hapo. Ni kweli tunayo hayo mapato, lakini nasema hata hayo mapato ambayo tunayapata ya ndani bado ni madogo kwa sababu, ipo kauli ya Serikali ambayo huwa inatolewa au mpaka sasa imeshawahi kutolewa kwamba matumizi ya Waheshimiwa Madiwani kwenye *allowances* au hizo *capacity building* ili waweze kwenda kutoa hamasa ya kukusanya mapato inatolewa kauli moja tu halmashauri zote posho zitafanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo hapo Wazii ametamka mwenyewe kuna halmashauri zaidi ya 19, kukusanya tu wanakusanya shilingi 500,000,000, huyu mwingine anakusanya shilingi 8,000,000,000, unasema wote wakatumie shilingi 200,000 tunawezaje hivyo? Hatuwezi kufanana, kama tunatofautiana kwenye kuzitafuta, tutofautiane pia kwenye kuzitumia. Hili ni jambo muhimu sana, inakatisha tamaa. Leo Waheshimiwa Madiwani wanalia kwa sababu wanafananishwa na kule kwa ndugu yangu Tunduru, hakusanyi, hana uwezo wa kukusanya, lakini Ubungo nakusanya. Hivyo, kama nakusanya waacheni Madiwani waendelee kutafuta mianya mingine iliyopotea ili waongeze mapato zaidi lakini na wenyewe waone au wapewe hizi *capacity building* tofauti kutokana na wanavyokusanya na sio kufananishwa kwa sababu tunatofautiana jinsi ya kutafuta. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. JUMANNE I. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la *TARURA,* ukurasa 25 wa taarifa unasema vizuri na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, zipo tozo nyingi ambazo zimeingia na kutoka. Tumeingiza mwaka jana ya

simu, lakini tumeitoa haraka, kwa hiyo tuliingiza ili ikapunguze gharama za *smartphone* ili tuweze kupata fedha kupitia bando na vitu kama hivyo na *data*, lakini ujanja ujanja wa wafanyabiashara wamekataa kupunguza. Mwaka huu nimfurahie sana Mheshimiwa Waziri ameirudisha tena, tunakwenda sawa, tukikupa ili twende sawa unakataa tunarudi tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo la tozo ya mafuta *fuel levy,* jambo hili limebaki hivyo hivyo na limetusaidia, kwenye bajeti ya barabara unaweza ukaangalia kabla ya tozo Mfuko wa barabara peke yake kwenda *TARURA* zile asilimia 30 ulikuwa unapeleka shilingi bilioni 243.15, lakini baada ya Mheshimiwa Rais kuona umuhimu wa kuweka tozo, imekwenda kuongeza shilingi 322.16. Unaweza ukaiona imekwenda *ku-double* ukiondoa vyanzo vingine vya barabara ambavyo vinatupeleka kama Shilingi Bilioni 781, lakini tayari shilingi bilioni 600.66 kama asilimia 66 zaidi ya shilingi trilioni 1.1 zimeshatoka. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE. JUMANNE I. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kwa leo nimeyasema hayo machache, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Namwita Mheshimiwa Mathayo, wajiandae Mheshimiwa Tumaini Magessa na Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hii hotuba ya Waziri wa Fedha. Ndugu yangu, mjukuu wangu Dkt. Mwigulu namshukuru sana, kwa namna jinsi ambavyo hotuba yake imejielekeza na inaonesha kwamba ni hotuba ambayo inaweza ikasaidia katika kuwakomboa Watanzania hasa kiuchumi. Maana kati ya shida kubwa ambayo tuliyonayo kwa Watanzania kwa sasa tuna tatizo kubwa sana la ajira katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kila mwaka nchi yetu inazalisha watoto zaidi ya milioni mbili ambao wanaingia katika soko la ajira. Sasa shida inakuja kwamba ajira inatupa taabu sana. Sasa umesema vizuri na ukaonesha kwamba kwa mwaka huu peke yake zaidi ya Shilingi Bilioni 900 zimeongezeka kwenye upande wa kilimo, lakini vile vile na kwenye mifugo, kwenye uvuvi na katika maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninachokifahamu katika hii Serikali yetu, wakati mwingine tunazungumza kitu kingine, lakini kwenye utekelezaji vinakuja vitu viwili tofauti. Tusipoangalia mwaka kesho hii hotuba tunaisifia tutakaporudi hapa bado itakuwa haionekani katika macho ya watu, kwa maana kwamba ni kwa namna gani imeweza kuwasaidia Watanzania. Nitoe mifano michache ambayo inaonekana dhahiri. Leo tukizungumza upande wa mifugo, Tanzania ni nchi ya tatu katika Afrika kwa kuwa na mifugo mingi, lakini cha ajabu ni kwamba pamoja na kwamba ni nchi ya tatu kuwa na mifugo mingi ni nchi ambayo mifugo haioneshi kuchangia katika kuondoa umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba, wale wafugaji wenyewe ni maskini na mifugo yao yote bado ina hali duni. Sasa ukija kutafuta kwamba sababu ni nini Watanzania ng'ombe wengi tulionao tuna ng'ombe aina ya *Zebu*. Ng'ombe aina ya *Zebu* mchungaji au mfugaji anamfuga zaidi ya miaka mitano, akija kumuuza anauza shilingi 300,000. Sasa nini kifanyike, tunahitaji kuhakikisha kwamba *tuna-improve* ile mifugo yetu na katika ku-*improve* ile mifugo yetu ni pamoja na kuleta mbegu za kisasa. Leo ukienda katika mashamba ya Serikali tuna mifugo mfano aina ya *Borani,* hawa ni ng'ombe ambao wanakuwa haraka wana nyama nyingi ambao wanaweza wakatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nimekwenda kwenye shamba mojawapo la la mifugo kwenye haya mashamba ya Serikali, unamkuta leo anauza dume mmoja wa miaka miwili shilingi 3,500,000. Mimi ni mfugaji, leo ukiangalia ng'ombe wangu mimi ambaye ni mfugaji, ng'ombe wangu ni bora kuliko wale walioko kwenye mashamba ya Serikali. Nilikuwa nauza ng'ombe dume wa miaka miwili kwa shilingi 2,000,000 lakini nimekuja nimegundua kumbe huku Serikalini wanauza shilingi 3,500,000. Sasa matokeo yake na mimi naye nimepanda badala ya kuuza shilingi 2,000,000 nauza shilingi 3,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa shida iliyopo ili yule mfugaji aweze *ku-improve* mifugo yake, tafsiri yake, lazima auze ng'ombe 10 apate shilingi 3,500,000 ili aweze kununua dume moja. Hivi katika utaratibu huo ni dhahiri kwamba mifugo haiwezi kusaidia katika kunyanyua kipato cha wafugaji, lakini na kunyanyua kipato cha Watanzania. Hata ungeenda kwenye upande wa uvuvi maana unajua ni

rahisi sana tukapeleka fedha kwenye kilimo, lakini tusipeleke fedha kwenye ukulima na hilo tunahitaji tuliangalie sana kwamba tunahitaji hizi fedha ambazo tumezipeleka ziweze kuwafikia wale ambao ni walengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hata kule kwenye uvuvi kuna vizingiti vingi yaani leo mtu akitaka kufungua kizimba chake kule cha ufugaji bora wa samaki, bado utakuta mambo ya *NEMC* yanamsumbua, upatikanaji wa vibali unakuwa na mlolongo mrefu kwa hiyo matokeo yake mtu anakata tamaa. Kwa hiyo, hayo yote ni mambo ambayo tunahitaji tuyaangalie ili tuweze kufikia malengo. Sasa niseme sisi ndio viongozi tuliopo na kazi ya viongozi ni kufanya mambo yatokee wala tusisubiri mambo yatokee. Sasa nizungumzie kwenye suala la kilimo na kwa kuwa tuna tatizo kubwa la ajira katika nchi yetu na hasa kwangu kule Musoma, vijana wetu wengi hawana ajira na tumesema kilimo kinaweza kikaleta *impact* kubwa, nini kifanyike? Pale kwenye Wilaya yetu ya Musoma tuna eneo kule linaitwa Bugema, zipo hekari zaidi ya 20,000, nasema tuanze mwaka huu na hekari 5,000 peke yake, ili mwaka kesho tukisimama hapa tuwe na vitu vya kuzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tukilima zile hekari 5,000 peke yake katika hekari 20,000 tutaleta ajira zaidi ya 10,000, nini kifanyike? Mheshimiwa Waziri wa Fedha atupatie fedha, nitashirikiana na Mbunge mwenzangu wa Musoma Vijijini Profesa Muhongo, pamoja na *DC* wetu pamoja na halmashauri zetu, twende tukalime zile hekari 5,000 tu kuanzia mwaka huu na ukulima wenyewe ni *very simple*. Tutatangaza nani anataka atulimie zile hekari 5,000, atakwenda atalima tutamlipa fedha, nani anataka ku-

*irrigate* zile hekari 5,000, ni rahisi kupatikana, atafanya kazi ya ku-*irrigate* na tutaanza kulima alizeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukilima zile hekari 5,000, bahati nzuri kutokea pale kwenye shamba kilometa 80 tunacho kiwanda cha kuweza kusindika mafuta. Tafsiri yake ni nini? Piga hekari 5,000 zote ulime alizeti na umwagilie, matokeo yake ni kwamba, tutapata mafuta mengi sana katika nchi yetu, hilo ni la kwanza. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba kuanzia mwezi wa Septemba mwaka huu mpaka mwezi Januari tayari tutakuwa tumepata mafuta mengi kwa ajili ya Watanzania, lakini hiyo haitoshi vijana wetu zaidi ya 10,000 watakuwa wamepata fedha na watakuwa wamepata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi mwaka kesho tunavyoanza katika kile kipindi cha miezi sita kuanzia mwezi Januari mpaka mwezi Juni, utaratibu ule ule tunatangaza nani anataka kutulimia hekari 5,000 atalima, nani anataka ku-*irrigate* hekari 5,000 ata-*irrigate*. Wale vijana wetu watafanya hiyo nguvu kazi ya kazi zote zinazofanywa kwa mikono. Tunahangaika masuala ya mbolea, kule kwetu wafugaji wako wengi wana makundi makubwa ya ng'ombe, maana yake ni kwamba ile mbolea yao tutapeleka ma-*tipper,* vijana watapakia watapeleka kule mashambani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kazi zote za mikono wale vijana watafanya na kwa kufanya hivyo tukilima mpunga hekari 5,000, ni eneo kubwa ambalo litasaidia vijana wetu kuwa na ajira na maisha yao yakawa mazuri. Kwa hiyo tunadhani kwa kufanya hivyo itatusaidia sana…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mathayo.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tumaini Magessa, jiandae Mheshimiwa Kimei.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii uliyonipatia ya kuchangia mapendekezo ya bajeti kuu, lakini namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii ambayo ameruhusu leo tuweze kuzungumza juu ya bajeti kuu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa bajeti nzuri ambayo tumeiona, tumeisikiliza. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hiki ambacho kimeandaliwa na kuletwa kwetu kwa ajili ya kutoa maoni yetu. Naamini kwamba tumeletwa duniani kufanya mambo tunayoyafanya yawe endelevu kwa ajili yetu sisi na vizazi vijavyo. Kwa hiyo, naamini kila tunachokizungumza leo lazima kiwe endelevu kwamba tutakitumia sisi na watu wanaokuja wataendelea kukitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, yale tuliyoyakuta tuliyonayo leo na tutakayoyafanya baadaye. Kwa hiyo, naamini kabisa kwa bajeti hii ambayo naiona nilikuwa najaribu kuangalia dhima yake, inatuonesha wazi kwamba, dhima ya bajeti hii ni kuongeza kiasi cha kufufua uchumi na kuimarisha sekta za uzalishaji kwa ajili ya kuboresha maisha.

Sasa tunazo sekta za uzalishaji kadhaa ambazo mimi nimekuwa naziangalia kuona kama kuna mabadiliko yamefanyika ili tujue kwamba tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwenye madini, ukuaji wa sekta ulitoka asilimia 6.7 kwenda 9.6, lakini kwenye mchango wa Taifa inaonekana inatoka 6.7 kwenda kwenye 7.2, inaoonekana kuna kitu kimefanyika. Sasa tunatakiwa tuhakikishe kwamba utekelezaji wa bajeti hii unakwenda kutupeleka mahali ambapo madini yatakwenda kuchangia pato la Taifa kwa kiwango kikubwa kuliko hiki tulichonacho leo na vilevile ukuaji wa sekta uweze kuongezeka. Ukuaji wa sekta utaongezeka vipi? Utaongezeka kwa sababu tutaongeza wigo wa wale wanaoshughulika na shughuli hizi za madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mahali nimesikia watu wanazungumzia habari ya makaa ya mawe, inaonekana hayajafanyiwa kazi, yafanyiwe kazi, lakini kuna mahali kwenye maeneo ambayo mimi natoka, jana nilikuwa napigiwa simu na mwanamke mmoja ananiambia, nina *plant* yangu, nataka umeme nitaupataje? Kwa hiyo, kuna mahali fulani ambapo watu wa umeme sasa wanatakiwa wapeleke umeme kwenye *plant* hizo ili uzalishaji uongezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa haya ni mambo mtambuka, basi Wizara zote ambazo zinahusika kwa mfano watu wa umeme wakaweke umeme kwenye hizo *plants* ambazo ninazisema ili uzalishaji ule uongezeke. Kwa sababu, tunajua kabisa bajeti ya umeme imeongezeka, haya mambo yatakwenda kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wale wanaoshughulika na kutoa leseni, *Special Mining License,* tuongeze wigo huu sasa. Tusichukue muda mrefu sana kuwapatia watu leseni kwa ajili ya kuongeza watu wanaochimba madini. Inawezekana pato letu linaonekana sasa hivi limekua, ni kwa sababu kumetokea mahali fulani mazingira yetu ya vita yale na nini bei yetu ya dhahabu ikapanda au bei ya madini fulani ikapanda, tukaonekana tuna mapato makubwa. Itakapokwenda ku-*stabilize* mapato yatashuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha pili ambacho nilitaka nikizungumzie ni katika hilo hilo ambalo tumesema, shabaha halisi ya bajeti hii ambayo tunaizungumzia leo imeongezeka. Tunatakiwa kutoka kwenye ukuaji wa 4.7 kwenda *at least* kwenye 5.3. Kuna mambo fulani ambayo yanatakiwa yafanyike na dhima imeyaonesha wazi. Mfano kilimo, tumepongeza kwa sababu kilimo kimeongezewa zaidi ya Shilingi bilioni mia sita kama na sitini hivi, lakini hoja yangu kubwa hapo ni kwamba, je, *machinery* yetu iliyozoea kupata Shilingi bilioni 100 tumeiandaa kwa ajili ya kubeba zaidi ya Shilingi bilioni 954? Tusije tukafika mahali tukamtengenezea sifa *CAG* mwaka kesho akija hapa atuoneshe tu kuna mahali kuna shimo hapa lilitokea, hapa shimo lilitokea. *Machinery* yetu ya kilimo iko tayari kubeba mzigo huu ambao tumeipatia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nilitaka kusema ni sekta ya mifugo na uvuvi ambayo nilitaka niizungumzie. Kilimo wamepata pesa, uvuvi wameongezewa na mifugo ukomo wao kwa Shilingi bilioni 100. Changamoto ninayoiona, sasa nimeona wameandika ukurasa wa 34, wanasema wanakwenda kuchukua *Ranch*

ya Kongwa, *hectares* 38,000. Sielewi sasa, wakati huo huo kwenye *page* hiyo wanaonesha wazi kwamba kuna shida, bado mchango wa uvuvi na mifugo haujatosha kwenye Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilitegemea hii Shilingi bilioni 100 iliyoongezeka ikaboreshe *NARCO* Kongwa, lakini bahati mbaya ni kwamba haiendi kuboresha, wanakwenda kunyang'anywa Kongwa. Sasa sielewi tunakwenda kuboresha mifugo au tuna maana gani? Kwa sababu mapori bado tunayo mengi? Kwa nini wasiende sehemu nyingine tukaiacha Kongwa iboreshwe kwa sababu *geographically ranch* ilipokuwa *located* Kongwa pale ni mahali pa kimkakati zaidi. Tukiwaondoa maana yake tumeonesha kwamba, tunawapatia sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa inaonekana tunaondoa mifugo michache iliyo mle ndani, tunaweka mashamba ya alizeti, tunaweka kiwanda cha alizeti kikubwa. Mimi sifikirii kwa sababu tumeongezewa Shilingi bilioni 100, maana yake Shiingi bilioni 40 kwenye mifugo, Shilingi bilioni 60 kwenye uvuvi. Basi twende tukaboreshe maeneo yetu, badala ya kuanza kuyaua sasa, tukiyaua maana yake tutakuwa hatuwezi kwenda. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sekta ya kilimo ambayo nilikuwa naizungumza, tuna maeneo mengi. Maeneo ninayotoka yanapitiwa na Ziwa Viktoria, kwa hiyo, nilitegemea sana hizi *irrigation schemes,* (hii mifumo ya umwagiliaji) tuione mingi kwenye

maeneo hayo ili maji ya Ziwa Viktoria yatumike tujenge uchumi wetu. Sina uhakika sana kama alivyosema mchangiaji aliyepita, tusije tukaja mwaka kesho tunapokuja kuzungumza hapa, tukazungumza kitu kingine tofauti na kile ambacho tumekipanga leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, kwa sababu nimesikia kengele imelia, nizungumzie wigo huu mpana uluoongezeka wa *TIN Number*. Tunapigiwa simu nyingi sana sasa kwamba tumerudisha kodi ya kichwa. Kwa hiyo, naona tu kwamba kuna nia njema ya Serikali kama wachangiaji walivyosema huko nyuma kwamba, *TIN Number* hizi ni muhimu kila mmoja apate *Tax Identification Number*. Kwa namna yoyote tutakavyofanya, kwa sababu tunataka kuhakikisha kwamba kila mmoja ana *TIN Number,* elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi wetu ili isionekane kitu kipya kimekuja wananchi wanalalamika wanahisi kama kuna tatizo mbele ya safari, na sisi tukanyamaza kwamba tumeingiza kwenye utaratibu wetu na wananchi wakaona kama wanakwenda kufanyiwa habari ya kodi ya kichwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kabisa Mheshimiwa Waziri kwamba, kitengo kile cha elimu ambacho kipo kwa ndugu zangu wa *TRA,* kinaweza kwenda kule vijijini kikakaa siku mbili kikarudi Dar es Salaam halafu wanawaambia tumetoa elimu mahali fulani. Ukienda kuuliza elimu yenyewe iliyosemwa huko ndani inaonekena haitoshi. Kwa hiyo, tutumie vyombo vya habari, tutumie majukwaa yote ambayo yanawezekana ili wananchi wapate elimu kwamba *TIN Number* hii ina maana gani kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maneno haya machache kwa kengele iliyolia naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tuna mgeni kwenye Jukwaa la Spika, anaitwa Mheshimiwa Olivia Tingea Moa. Yeye ni Mkurugenzi wa Masuala ya Kimataifa kutoka Bunge la Cameroon. *(Makofi)*

*Welcome Mr. Moa. Welcome to the Parliament of Tanzania, you are most welcome. Thank you very much. (Makofi)*

Sasa mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunivumilia. Nimeomba sana nichangie mapema, na umenivumilia ukanipa fursa hii. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Sasa vipi, umekasirika uondoke au?

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, niko vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Aah, *okay*. Ahsante.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kutuletea bajeti ambayo ni nzuri sana kusema kweli. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri wetu mchumi msomi

Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Mchemba, Naibu wake, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu na timu nzima ya Wizara kwa kazi nzuri. Niseme kwamba wamefikiria sana nje ya *box* wakati huu, ndiyo sababu unaona kwamba sera wanazotuletea ya matumizi na mapato ni sera ambayo ina vitu vipya, vitu ambavyo hatukuviona huko nyuma. Nasema kwamba, kweli ninyi mmechapa kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwamba, nitaendelea kuwapongeza endapo watakumbuka kwamba tuna wananchi kule Kahe Mashariki ambao wanadai shilingi bilioni 5.2 kwa thamani ya mwaka 2013 ambao wametoa maeneo ya kujenga *One Stop Inspection Center* pale Njiapanda Himo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye bajeti yenyewe. Niseme kwamba, hii bajeti ni bajeti ambayo kweli imetengenezwa kwenye mazingira ambayo mimi nasema ni magumu kwa sababu kuna vihatarishi vingi ambavyo havitabiriki kutokana na uchumi wa dunia na uchumi hata huu uchumi wetu. Kwa hiyo, naamini kwamba tutapitisha hii bajeti, lakini mimi naamini ni vizuri utekelezaji wake ukawa unafanywa *continuous risk assessment* ili kujua kwamba, je, ni kweli kwamba, zile *assumptions* zitakuwa *fulfilled*?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba bajeti imebana, inaonesha kuwa na *fiscal measures* ambazo ni nzuri na ndiyo sababu unaona kwamba *financing* ukiondoa ile *rollover, financing* inayokuwa *required* na angalau *3%* ya *GDP* ambapo kusema kweli kwa hivyo naona kwamba tumeji-*tighten.*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba, kwa viashiria hivi tunavyoona kule Ulaya sasa hivi, *UK* wanatangaza *inflation* ya *11%,* Marekani *inflation* iko juu *7%* na viashiria hivi vya *interest rate* kupanda kuendana na *inflation;* na kule Marekani sasa hivi riba kwenye hizo *third reserve rate* ni *3.5%.* Kwa hiyo, inaonekana kwenye masoko ya kukopa, masoko ya *International Re-capital Market* riba zitapanda sana. Zitapanda sana kwa maana kwamba sio wakati wa kukopa nje kwenye masharti ya biashara kwa sababu ni lazima tujiangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo sababu nikasema kwamba, cha kwanza ni kuona kwamba kweli kuna mambo ambayo tumeweka. Kwa mfano, ukopaji wa *about three trillion* kutoka kwenye masoko ya nje, inawezekana baadaye tukaona kwamba pengine tusitishe au tupunguze miradi ile ya maendeleo, hususan ununuzi wa ndege nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri ndege tunazozitaka sasa hivi ni lazima tumwombe Mheshimiwa Rais atuletee ndege ya mizigo kwa sababu inahitajika, ndio *big constraint* ya ku-*export* bidhaa za bustani *(hot culture products)*. Ni hazina, ni kwamba hatupati kutoka nje *flights* za kutosha kwa sababu pia uzalishaji wetu hautoshelezi kwa ndege za nje ziweze kuja na zitue mahali pamoja, lakini tukiwa na ya kwetu itatua Mbeya, ije Dar es Salaam, iende Arusha, itajaa itapeleka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ubunifu nilioona hapa ni kwamba Serikali na timu ya *finance* wamegundua kwamba, sasa hivi nadharia ya kuongeza tu kodi siyo njia pekee ya kuongeza mapato ya Taifa. Pia unaweza

ukahamasisha matumizi kwa mfano, kama ni wanywa bia wanywe kwa wingi zaidi, kama ni watumia simu, watumie kwa wingi. Kwa hiyo, *this time* tunaona wamejaribu kuangalia ni namna gani waongeze *volume*. *I think* tutapata mapato makubwa zaidi kwa kupunguza au kwa kutokuongeza kodi za vinywaji; bia na vinywaji vingine pamoja na vinywaji vya baridi, hawakuongeza. Nawapongeza kwa sababu watu watatumia na *volumes* zitaongezeka, kwa hiyo, naamini mapato yatakayotokana na ile *volume* itakuwa ni vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona ile ya tozo tuliyozungumza mwaka 2021, wamepunguza, lakini pamoja na kupunguza kidogo baada ya mkutano wa mwaka 2021, na mwaka huu 2022 wamepunguza ile tozo ya miamala. Ninaamini kwamba, hiyo imetokana na ukweli kwamba, matarajio ya makusanyo kutoka kwenye tozo hayakufikiwa *by more than 70% I think* kutokana na takwimu. Kwa hiyo, hiyo kupunguza huko kutasababisha watu waendelee kutumia hiyo *financial improvement* iendelee kupatikana kupitia hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hatua nyingi zilizochukuliwa kwenye bajeti hii zinalenga zaidi kuwapunguzia wananchi makali ya mfumuko wa bei ambao tunaona unatoka nje. Nataka niseme hivi, nitoe angalizo kwamba tusipeleke matarajio ambayo hatutaweza kuyafikia. Matarajio kwamba tunaweza tukadhibiti mfumuko wa bei kwa sasa hivi, naomba tujaribu kuwaelimisha watu kwamba kwa nini huu mfumuko ni mgumu?

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mfumuko siyo ule wa kawaida ambao Benki Kuu wanaweza wakaenda tu wakasema tunapunguza ujazo wa fedha kwenye mzunguko wa uchumi wetu. Hawawezi, kwa sababu wakifanya vile siyo *source* yake. *Source* ya huu mfumuko ni ugavi; ni upungufu au uhaba wa bidhaa duniani, na uhaba wa bidhaa unachukua muda. Kwanza kuongeza uzalishaji kunachukua muda, kwa hiyo, hata ufanyaje ni kitu kinachukua muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ili kuongeza uzalishaji ni lazima tuweze kutoa mikopo. Hiyo mikopo ni ya kuwasaidia wale watu waweze kuanzisha miradi ile na kama kilimo wafanye. Ila ukweli ni kwamba, ukiongeza hiyo mikopo maana yake unaongeza fedha kwenye mzunguko, na unachochea *demand*. Kwa hiyo, hiyo inasababisha mfumuko wa bei uwe mgumu sana kuudhibiti kwa sababu, ukiingiza hela ili watu wazalishe, lazima itasababisha mfumuko. Ila ukweli hatuwezi kuepuka hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ina maana kwamba, tukubali, hata kama mfumuko utaongezeka kidogo, lakini itakuwa ni *temporary transitory,* baada ya muda kidogo uzalishaji utakuja, tutapata mawese, na kadhalika halafu tutaanza sasa kushusha tena ule mfumuko. Kwa sasa hivi tusing'ang'anie sana hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, kuna suala zima la *stabilization fund* ya bei za *commodities.* Nafikiri badala ya kufanya vile, mimi niende haraka niseme kwamba, nashauri Wizara iangalie mfumo wa *commodity pricing insurance.* Sisi tulifanya kwa kushirikiana na *IFC* pamoja na Rabobank pale

wateja wetu wakafaidi sana. Tutumie huo mfumo badala ya kuanza *funds* na kadhalika. Hilo linawezekana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine kuna *issue* hii ya kutengeneza Dar es Salaam kama *hub,* na jana au juzi uliizungumza, naamini kitu cha msingi, hizi *measure* zilizochukuliwa sasa hivi ni za kupunguza ushuru ili watu waweze ku-*trade* kutoka Dar es Salaam zaidi badala ya kwenda jirani halafu mizigo inarudi kwetu, naamini kwamba hiyo itasaidia. Ila kwenye *issue* ya changamoto…

*(Hapa, kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, aah, *time keeper* naona, huyu *time keeper* huyu!

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tum-*audit* huyu *time keeper. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tunapochangia au tuki-*refer* Ripoti ya *CAG,* tuseme ya mwaka gani. Maana ripoti iliyokuwepo ni ya 2020/2021, na sasa ni takribani mwaka mzima, na kipindi hiki Serikali inakuwa mambo mengi yenye changamoto imeshaanza kuyashughulikia.

Kwa hiyo, naomba tu mkichangia mseme ni ya mwaka gani ili tuweke *records* zetu vizuri.

Waheshimiwa jioni tutaanza na Dkt. Ishengoma, Mheshimiwa Aloyce Kamamba, Mheshimiwa Jophet Hasunga, Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mheshimiwa Kanyasu na Kiti kitaelekeza wengine.

Nasitisha Shughuli za Bunge mpaka Saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu!

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, nilimuita Mheshimiwa Dkt. Ishengoma lakini ana dharura kwa hiyo tunaanza na Mheshimiwa Aloyce Kamamba

jiandae Mheshimiwa Hasunga, Mheshimiwa Mwambe na Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia na kuwa mtu wa kwanza kwa muda huu wa jioni. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa, nzuri sana ambayo ameifanya hasa katika kupeleka fedha nyingi katika ujenzi wa madarasa, hospitali na barabara. Yapo maeneo mengine ambayo tangu dunia inaumbwa hayajawahi kupata barabara lakini kupitia Mheshimiwa Rais maeneo hayo sasa yamepata barabara, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kugusa eneo la kilimo na nianze kupongeza Serikali kwamba kupitia bajeti yake ya mwaka huu, Serikali imeweza kuongeza fedha nyingi kutoka Bilioni 200 kwenda Bilioni 900 tunapongeza sana Serikali kwa fedha hizo ambazo zimepelekwa. Lengo la Serikali nafahamu kwamba ni kuongeza chakula lakini vilevile kujibu changamoto inayokabili Serikali hasa ya mafuta ya kula.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao mojawapo ambalo Serikali imeweza kuliona na kuliweka ni zao la Chikichi. Kwetu Kigoma zao hili linakubali. Kwa hiyo niombe sana Serikali iongeze nguvu ya kutosha kwa kupeleka wataalamu wa kutosha wa mbegu ikiwa ni pamoja na mbegu ya chikichi katika eneo hili. Hii iende sambamba na kupeleka mbegu za kutosheleza kuweza kukidhi mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi Kigoma ipo, ardhi siyo changamoto, lakini vile vile Kigoma mvua si tatizo, kwa hiyo eneo hilo linaruhusu moja kwa moja zao hilo kuweza kukubali, kwa hiyo naomba sana Serikali iangalie eneo hilo. Vilevile nasisitiza zao la chikichi kwa sababu zao la chikichi kupitia chikichi tunapata mafuta, kupitia chikichi tunapata sabuni, kupitia chikichi tunapata chakula cha mifugo na mazao mengine yote. Kwa hiyo, ili tuweze kufanikiwa naomba sana Serikali iongeze nguvu zaidi katika zao hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kukidhi zao hilo ambalo linaongeza mafuta lipo zao la alizeti. Kakonko tunalima zao hili vizuri sana, lakini changamoto ni upatikanaji wa mbegu, upatikanaji wa mbolea, niombe sana Serikali iandae mbegu mapema, iandae mbolea mapema, iweze kupeleka katika maeneo haya ili Kakonko na Mkoa mzima wa Kigoma tuweze kupata mafuta ya kutosha kupitia alizeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo miundombinu hasa ya barabara, barabara ni uchumi, lakini barabara ndiyo mishipa ya kuongeza uchumi katika nchi. Mkoa wetu wa Kigoma ikiwa sambamba na Mikoa mingine ipo mikoa ambayo haijaweza kuunganishwa kwa njia ya barabara hasa barabara ya lami. Kigoma haijaunganishwa na Tabora, Kigoma haijaunganishwa na Katavi, Kigoma haijaunganishwa na Mikoa ya Mwanza na Kagera. Niombe sana fedha zipelekwe haraka ili ujenzi uweze kukamilika na hatimae Kigoma kama Mkoa nao uwe umeweza kuunganishwa katika maeneo hayo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ipo reli ya kisasa ya *Standard Gauge*. Nashukuru sana kwamba Serikali imeweza

kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kutoka Uvinza kwenda mpaka Burudi katika Mji wa Itega na kwenda sambamba mpaka Congo. Najua kwamba Serikali imeweka katika mpango niombe sana Serikali iweze kuongeza fedha za haraka na ujenzi uweze kuanza mara moja kwa sababu barabara hiyo reli hiyo inahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu bila malipo. Serikali imeweza kupeleka fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba elimu kuanzia Msingi hadi Kidato cha Sita inatolewa bure kwa maana gharama zote zinakwenda upande wa Serikali. Vipo vyuo vya elimu ya kati wapo wanamaliza Kidato cha Nne wanakwenda kusomea ualimu, wapo wamemaliza kidato cha nne wanakwenda kusomea ufundi, wapo wamemaliza kidato cha nne wanakwenda kusomea udaktari na kadhalika. Hawa Serikali inawaangalia kwa kiasi gani? Maana tunaona kwamba Serikali imechukua eneo la huku chini shule ya Msingi na Sekondari Kidato cha Tano na Sita, imekwenda mpaka Chuo Kikuu lakini hapa katikati ambapo pana watoto wa Watanzania wengi Serikali haijaweza kupaona. Naomba Serikali iangalie eneo hilo wapo Watanzania wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto hawa ambao wanakwenda kwenye vyuo elimu ya kati hawana tofauti na hawa ambao wanakwenda Kidato cha Tano na Sita na kwa taarifa vijana wengi sasa badala ya kwenda hata kwenda kwenye vyuo na kadhalika wanatamani sasa kwenda Kidato cha Tano na Sita kwa kuwa Serikali imeamua kwamba iwe elimu bure. Kwa hiyo, niombe kwa kuwa hawa vijana wanakwenda kusomea taaluma wanasomea ufundi, wanasomea u-*nurse*, wanasomea udaktari ambao wanatoka moja kwa moja na kuweza

kujiajiri, naomba Serikali iweze kupeleka fedha katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira ya watumishi. Ni ukweli kwamba Serikali imejenga madarasa mengi safi, lakini imejenga vituo vya afya safi, imejenga hospitali nyingi safi, imejenga zahanati safi, lakini ni sawa na chakula kizuri ambacho hakina chumvi. Watumishi wanahitajika, Waalimu wanahitajika, Madaktari wanahitajika, sasa sijaona vizuri ni kwa kiasi gani Serikali inapeleka nguvu kubwa zaidi katika kuajiri hawa watumishi ili waweze kufanyakazi kwenye shule zetu za msingi, kwenye hospitali zetu, kwenye zahanati zetu na kadhalika.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala la barabara ambayo inatuunganisha Tanzania na Burundi. Taarifa zilizopo ni kwamba nchi ya Burundi imehamisha Makao Makuu kutoka Bujumbura kuja Mji wa Kitega na Mji wa Kitega uko kilomita kama 150 kutoka mpaka wa Muhange, lakini hatuna barabara sasa ambayo inatuunganisha Tanzania kwa barabara ya lami kutuunga na nchi ya Burundi hasa kwa kwenda Makao Makuu ya nchi ambayo ni Kitega. Barabara ambayo inastahili kutuunganisha ni barabara ya kutoka Kakonko kwenda mpaka kwenye mpaka wa Muhange. Niiombe Serikali ilifanyie kazi hili kwa kupeleka fedha za kutosha, barabara hiyo ijengwe na niombe sana Waziri wa Fedha upeleke wataalam kwenye mpaka huo wa Muhange ambao wanajua kwamba barabara ikishajengwa na wataalam hao wakipatikana watakusanya fedha, kwa hiyo hiyo fedha ambayo utakuwa umeitumia kujenga barabara nina hakika fedha hizo zitarudi bila kuchelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo barabara za Mji wa Dodoma. Dodoma ni Makao Makuu ya nchi, ni Jiji sasa, hatutegemei kwamba Dodoma itarudi iwe Manispaa au iwe Mji Mdogo lakini barabara zake ni tatizo. Ukiangalia sasa hivi Kiongozi yeyote wa Kitaifa awe Spika, awe Naibu Spika awe Waziri Mkuu awe Rais anapita Mji wa Dodoma unakuwa ni tatizo sehemu ya kupita. Sasa ni juu ya Serikali kuamua kulidhibiti tatizo hili mapema, isije ikawa kwamba baada ya muda ni mrefu sasa ndiyo tunaanza kufikiri kujenga barabara za kupitisha labda upande mmoja barabara tatu au nne upande mwingine barabara tatu au nne ni vema zikaanza kujengwa sasa ili kudhibiti tatizo la *jam* kwa maana ya wingi wa magari katika Mji wetu wa Dodoma. Kwa hiyo, napendekeza ijengwe barabara mapema ya kuweza kupitisha malori, badala ya malori kupita katika Mji wa Dodoma katikati basi malori hayo yaweze kupita pembeni kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa niendelee kupongeza Wizara ya Fedha kwa bajeti nzuri sana, ambayo imeiweka ina vipaumbele vyote muhimu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Serikali yetu inafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja nashukuru sana ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Hasunga ajiandae Mheshimiwa Mwambe, jiandae Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa hii nafasi ili niweze kuchangia katika hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake kwa kazi kubwa ambayo wameifanya na namna walivyokuja na bajeti nzuri yenye matumaini makubwa kama yeye mwenyewe alivyosema, kwa kweli tunawapongeza sana. Pia ninampongeza kwa kusimamia uchumi wa nchi yetu ambao ndiyo uhai wa maisha yetu, kwa kweli tunakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimpongeze sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan alipokutana na Wabunge mara ya mwisho alituambia kwamba atapeleka mkazo zaidi kwenye sekta za uzalishaji na bajeti hii imeonesha yale aliyoyasema anaenda kuyatekeleza kwa vitendo tunampongeza sana kwa namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta za uzalishaji ziko kama tano, lakini sekta ya kilimo ikijumuishwa kwa mtazamo mpana inajumuisha kilimo cha mazao, mifugo na uvuvi pamoja na misitu. Sekta hii ndiyo imebeba uhai wa Taifa letu, tukifanya vizuri katika hili eneo tunao uwezo wa kupata mapato makubwa tuna uwezo wa kuondokana na umaskini, tuna uwezo wa Pato la Taifa likaongezeka kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kilimo ndiyo tunapata chakula chote na bila chakula chote na bila chakula hakuna kazi inayoweza kufanyika, sote tunategemea chakula lakini kwenye kilimo ndiko tunapata malighafi zote za viwanda, kwenye kilimo ndiyo kwenye ajira nyingi, kwenye kilimo ndiyo tunapata fedha nyingi za kigeni. Kwa hiyo, ina maana madeni yote tuliyonayo ya nje yatalipwa na fedha zinazotokana na sekta hii ya kilimo na

sekta zingine za uzalishaji. Kwa hiyo, lazima tuongeze mkazo kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo pia ndiyo biashara kwa hiyo katika hayo maeneo matano ndiyo yamebeba nchi yetu, Watanzania walio wengi wanaishi huko, wanaishi vijijini wanategemea kilimo, wanategemea uvuvi, wanategemea ufugaji wanategemea misitu. Uwekezaji wa Taifa letu lazima ujikite kwenye eneo hilo na Rais wetu amejibu. Kwa mara ya kwanza nafikiri itakuwa ni mara ya kwanza kama sikosei, sasa bajeti ya kilimo yaani kwa tafsiri pana kwa maana ya kilimo cha mazao ya misitu, kilimo cha ufugaji na uvuvi tunazo zaidi ya Trilioni moja, kwa hiyo hili tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uwekezaji huu mkubwa alioufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuamua kuongoza na kuisimamia sekta ya utalii. Utalii wa nchi yetu unaweza ukaleta mchango mkubwa sana, tukiungana na sekta zingine za uzalishaji utalii utaleta manufaa makubwa sana. Ukiangalia sasa hivi utalii kwa mwaka uliopita mwaka 2021 duniani, pamoja na kuwepo kwa ugonjwa wa UVIKO-19 zipo nchi zimefanya vizuri kwenye utalii sana. Lakini ukichukua kwa takwimu za namna ya vivutio vya utalii vizuri Tanzania tulikuwa tunashika nafasi ya pili duniani sasa hivi imeshuka mpaka nafasi ya nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa na nafasi nzuri na kuwa na vivutio vingi bado uwekezaji wetu hautoshi na bado hatujaweza kupata watalii wa kutosha hatujapata mapato ya kutosha. Kwa mfano, ukiangalia nchi inayoongoza sasa hivi kwa mwaka 2021 Ufaransa ndiyo

iliyoongoza ilipata watalii milioni 89.4 ikifuatiwa na Spain ilipata milioni 83.7, Marekani ilipata milioni 79.3, China ilipata milioni 65.7, Italy milioni 64, Turkey milioni 51, Mexico milioni 45, Thailand milioni 39, German milioni 39, United Kingdom milioni 39, Tanzania hatujafika hata milioni moja kwa watalii wa nje, kwa hiyo ina maana eneo hili lazima tuwekeze vya kutosha, ndiyo maana Rais wetu ameamua kuja kuhakikisha anaisimamia hii sekta vizuri ndiyo maana akaja na huu utaratibu wa hii filamu ya *Royal Tour*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hii filamu inatutangaza sana kama nchi na mimi nafikiri tujipange katika kuhakikisha kwa kweli utalii ulete mchango mkubwa, hii ndiyo nchi pekee yenye vivutio vingi, tuna milima ya kutosha, tuna mito, tuna mabonde, tuna mbuga za Wanyama, tuna bahari, tuna maziwa, tuna kila kitu, tuna utamaduni! Sasa eneo la kuliangalia tusifurahie tu kwamba hoteli zimejaa tuseme kwamba bado tuwekeze zaidi kwenye hoteli ili tupate watalii wengi wa kuja kwenye mahoteli yetu, watalii wa kuja kwenye mikutano mbalimbali ambao hao ndiyo watakaotuletea fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunataka utalii wa ndani uongezeke na ndiyo maana mwaka 2018 nilisema kwa mara ya kwanza kwamba Watanzania wajifunze kula Maisha, twende tukale maisha kwenye mbuga zetu. Watanzania wengi hawakunielewa walifikiri labda ni utani, hiyo ni *theory* ya uchumi! Ili uchumi wetu uchangamke Watanzania tukale maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nafurahi sana kuona Rais wetu ameunga mkono na ameonesha sasa yeye ameshika mstari wa mbele nasi sasa tumuunge

mkono. nawapongeza sana umoja wa vijana wa Chama cha Mapinduzi juzi walipokuja kwenye Mkutano wao wote waliongozana mpaka Ngorongoro kwenda kufanya utalii wakiunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais, nasi tuendelee kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais. Tutangaze vivutio vyote vilivyopo katika maeneo yote, Rais ametangaza sehemu sasa ni wajibu wetu sasa kutangaza vivutio vingine vyote vilivyobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Mbozi kuna Kimondo cha aina yake cha kihistoria, kuna maji moto, kuna Ruaha kule kwa mwenzangu kule na maeneo mengine utalii wote Nyanda za juu Kusini nchi yetu hii tuviangalie tutangaze, naamini itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuangalie utalii wa elimu, tunavyo vyuo vingi tuhakikishe tunabadilisha taratibu za udahili ili watu wengi kutoka nchi za nje waje kusoma hapa, watatuletea fedha nyingi za kigeni, huo ni utalii ambao tunauhitaji. Tuna utalii wa matibabu, kufuatana na jitihada ambazo Serikali ya Awamu ya Tano na ya Sita zimechukua kuimarisha huduma za afya kwenye mahospitali yetu, tunapata wagonjwa wengi tunapata watalii wa matibabu. Hili ni eneo ambalo lazima tuwekeze vya kutosha na tuendelee, kuna utalii wa maliasili, kuna utalii wa mali kale na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ambalo nafikiri ni muhimu kwenye uzalishaji ni eneo la viwanda. Viwanda ndiyo uti wa mgongo kwa kilimo chetu tunatakiwa kuwekeza zaidi kwenye viwanda, sasa viwanda hivi bila kuwa na mfuko wa kuchochea maendeleo ya viwanda hatutaweza kufika, nashauri tuangalie namna ya kuweka

mfuko wa kuongeza kuchochea viwanda itatusadia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne nilizungumzia kuhusu ujenzi wa bandari kavu kule Tunduma na Pemba kwamba ni muhimu sana ile bandari ikajengwa, kwa sababu itatusaidia nchi mbalimbali za kusini mwa Afrika zitakuwa zinachukua mizigo yao maeneo yale. Kwa hiyo, tuijenge ile ili kusudi watu kutoka Zambia, Malawi, Zimbabwe, Congo wachukulie mizigo maeneo yale itatusadia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hapo suala la mafuta tuongeze uwekezaji. Mheshimiwa Waziri tuangalie sehemu zote ambazo reli inapita reli ya kati, sehemu kule *TAZARA* inapita kwenye Mikoa mikubwa kama Dodoma tuweke matenki makubwa ya mafuta, mafuta yasafirishwe na treni, yaje hapa yawekwe kwenye hayo matenki, maeneo mengine kama Kigoma au Tunduma tuweke matenki ili kusudi nchi jirani waje kuchukulia mafuta hapa. Tutapata fedha nyingi, naamini zitachangia katika uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri kwa kuja na mifumo ya kusimamia matumizi ya fedha, kwa kweli nimefurahia sana kwa namna alivyokuja lakini amesema pia ameimarisha ukaguzi wa ndani, *CAG* tumemwongezea fedha na pongezi, lakini naomba niongezee sasa hawa Wakaguzi wa Ndani wana kazi kubwa ndio wanaosimamia fedha za umma, lakini wanahitaji kupatiwa mafunzo ili waelewe na waweze kwenda kufanya kazi vizuri. Sasa hivi utaratibu uliopo, fedha wanazitegemea kutoka kwa Maafisa Masuuli bado kama

hatutarekebisha hawataweza kwenda kwenye miradi na kukagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nafikiri tuliangalie hilo. Tuwatengenezee bajeti yao ili iwatosheleze kama ilivyo kwenye *M&E*. *M&E* wana bajeti yao na hawa Wakaguzi wa Ndani wawekewe mafungu kule katika kila mradi wa kwenda kufanya hiyo kazi na kufuatilia, itatusaidia sana. Pia tuwape vyombo vya usafiri, tuwape mafunzo, wataenda kufanya kazi nzuri sana na *CAG* atakapokwenda itasaidia sana katika kufikia ile hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi sana kuona bajeti imekuja na majibu mazuri na matumaini makubwa, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, nawapongeza wote, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kusikia kilio cha Watanzania cha kuja na bajeti inayoenda kutoa majibu. Nina uhakika ruzuku na mambo mengine yatasimamiwa vizuri ili nchi hii iweze kupiga hatua kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwambe, wajiandae Mheshimiwa Kanyasu na Mheshimiwa Msongozi.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ili niweze kuchangia na kutoa maoni yangu hasa zaidi kuhusu bajeti iliyopo mbele yetu na kuifanyia maboresho kwa manufaa ya nchi yetu. Kwa namna ya pekee kabisa niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake Mheshimiwa Chande

tumefanya kazi wote pamoja kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara, ni mtu makini na hawa wote ni watu makini sana na wasikivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti iliyopo mbele yetu ni nzuri sana na kwa vyovyote vile imeonesha nia njema kabisa ya Mheshimiwa Rais kutaka kulisongeza Taifa hili mbele. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara, kwa hiyo nitaongea kidogo kwenye upande wa biashara mambo ya kodi, tozo na mengine kwa maana ya kutaka kuboresha bajeti hii. Kwa namna ya pekee kabisa nimpongeze Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara yetu ya Utalii kwa sababu hivi karibuni tumeona Mheshimiwa Rais amesafiri nchi nyingi hapa duniani kwenda kufanya kazi ya kutangaza vivutio vyetu vya utalii kwenye ile sinema maarufu kabisa inayoitwa *Royal Tour*. Hata hivyo, jambo ambalo nataka niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba kwenye Bunge lililopita kila mara tulikuwa tunaongea suala la vita ya kibiashara na tulikuwa tunajaribu ku-*site* namna ambavyo majirani zetu wanajaribu kutumia vivutio vyetu na kuvitangaza kama vivutio hivi ni vya kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vyovyote vile namna mama alivyofanya kazi nzuri kwenye hii sinema ya *Royal* isingekuwa rahisi majirani zetu kukaa kimya na kuona kwamba sisi sasa tunataka kwenda kuwa sehemu kubwa ya utalii katika Afrika ya Mashariki. Kwa hiyo lazima tutapigwa madongo kwa kila kona na sisi kama Watanzania lazima tuwe na uwezo wa kuwajibu lakini na kuongeza zaidi vivutio kwa maana ya biashara yetu ya utalii iwe kubwa zaidi kuliko nchi za jirani, kwa sababu sasa hivi tumeamua kueleza sisi wenyewe kwamba sisi kama

Watanzania ndio wamiliki wa Mlima wa Kilimanjaro, sisi kama Watanzania ndio wamiliki wa Ngorongoro, sisi kama Watanzania ndio wamiliki wa Loliondo. Kwa hiyo ukishuka Uwanja wa Kimataifa wa Dar es Salaam, ukishuka Uwanja wa Kimataifa wa KIA uliopo Kilimanjaro kwa vyovyote vile utafika Kilimanjaro, utafika Loliondo, lakini pia utafika na Ngorongoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani walikuwa wanasema ili ufike Mlima Kilimanjaro unatakiwa ukashuke kwenye uwanja wa nchi za jirani ili iweze kuwa rahisi kutoka kule kurudi hapa. Ninachoomba sasa ni kuboresha miundombinu ili tuweze kwenda sambamba na hizi kelele zinazopigwa na majirani zetu tusizichukulie poa poa kidogo, Mheshimiwa Waziri wa Utalii aongeze juhudi kwenye kuhakikisha sasa vivutio vyetu vya utalii vinatangazwa zaidi duniani kwa ajili ya manufaa ya Watanzania ili tuweze kukuza uchumi wetu tuweze kupelekwa kwenye nchi ya daraja la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kuna *NGOs* nyingine na wanaharakati hata Watanzania na wenyewe wamekuwa sehemu ya hujuma zinazofanyika kwa maana ya Ngorongoro lakini pamoja na Loliondo. Kwa hiyo tuwe makini sana tusichanganye mambo haya. Harakati pamoja na haki za binadamuh lakini harakati pamoja na biashara na lazima tutambue kwamba sasa hivi tupo kwenye vita ya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine tumeona sasa hivi nchi yetu kumekuwa na *inflation* na hii *inflation* imesababishwa na kupanda kwa bei ya bidhaa. Ukiangalia vizuri imegawanyika katika namna mbili kuna

sababu zetu wenyewe za ndani na kuna sababu za nje. Sababu za nje kila mara tulikuwa tunasema vita lakini pia na upatikanaji wa malighafi za kuzalishia, vitu vingi sisi tulikuwa tuna *import*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sasa na sisi tuwe *exports* kwa maana tufanye kazi kwa nguvu kabisa tuhakikishe Mradi wetu wa Liganga na Mchuchuma unaanza mara moja ili tuweze ku-*export* chuma, tuweze kupata fedha za kutosha kufanyia miradi yetu ya ndani. Pia tuangalie, kuna tozo mbalimbali zinazotozwa kwenye bidhaa ambazo zinazalishwa hapa nchini lakini pamoja na bidhaa ambazo zinatoka nje ya nchi, tukiamua kurekebisha tozo hizi kwa vyovyote vile gharama za uzalishaji za ndani zitashuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, niwaombe Waziri amemaliza ku-*present* hii taarifa yake lakini kuna mambo tuyaangalie. Sasa hivi ni zaidi ya miaka minne, mitano, nafikiri toka *VAT* iliposhushwa kutoka asilimia 20 ikawa hadi 18 hawajagusa tena *VAT* lakini pia hawajagusa tena *corporate tax*. Tukiamua kushusha vizuri *VAT* labda kufikisha asilimia 16, tukashusha *corporate tax* hadi kufika asilimia 24, kutakuwa na *compliance* kubwa, watu wengi wataweza kulipa kodi na mauzo yataongezeka na hii itakwenda kuchangia kwenye kuongeza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze hapa wakati Waziri anatoa taarifa yake alikubali kabisa kwamba sasa hivi Sheria ya Korosho ambayo ilikuwa ina-*hold export levy* amekubali sasa kurudisha, lakini tuiboreshe zaidi. Ilipoondolewa wakati ule ilikuwa ni asillimia 65 ambazo asilimia 50 zilikuwa zinarudi Serikali Kuu, lakini 15 zilikuwa

zinakwenda kusaidia kwenye vituo vya utafiti na maeneo mengine. Sasa hivi imerudi ni *fifty fifty,* nimwombe sana Mheshimiwa Waziri tutengeneze kanuni bora kuona namna ya kutumia fedha hii. Sisi tunatamani sana fedha hii ingekwenda kupelekwa kama ruzuku kwenye pembejeo zinazosaidia kuzalisha korosho, lakini fedha imepelekwa Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizarani kuna mazao mengi sana, madhumuni ya fedha hii ilikuwa inakatwa ili ikasaidie wakulima wa korosho pamoja na kwamba sasa hivi wakulima wa korosho wamekuwa mtambuka nchi nzima watu wanahamasishwa kulima korosho, sio jambo baya, lakini ikasaidie tu kuendeleza zao la korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kuna suala la *blueprint*. Mheshimiwa Waziri wakati analeta taarifa yake ameongea sana kuhusu suala la *blueprint* na kwamba kuna kodi zile mbalimbali karibu 15, nafikiri wameamua kuziondoa ili kuweza kuona zinawafanya wawekezaji kuvutiwa kuja nchini kwetu kuwekeza kwa sababu ya kutengeneza mazingira rafiki ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe kwamba *speed* inayotumika sasa hivi kwenye kutekeleza mambo mbalimbali yaliyomo ndani ya *blueprint* ni ndogo sana. Niombe Wizara iongeze *speed* kwenda kuhakikisha na zile kero zinazotajwa na wafanyabiashara wanaokuja kuwekeza hapa Tanzania nazo zinaondoka, mojawapo ikiwepo hii ya *city levy*. *city levy* inapangwa na halmashauri zetu lakini *city levy* sheria inataka kuanzia asilimia 0.01 hadi 0.03. Kutokana na kuwa na vyanzo vichache vya mapato Halmashauri nyingi zinaamua kukamua wafanyabiashara.

Wengi wanang'ang'ania kutoza asilimia 0.03 wakati ruksa ni kuanzia asilimia 0.01 hadi 0.03.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa karibuni tulifanya ziara Bukoba, tulitembelea viwanda pale na tukaenda kwenye Kiwanda cha *AMIMZA* kwenda kujionea wenyewe wanaozalisha kahawa lakini pia tulifika kiwanda cha sukari, hii mitaji imekuwa ni kero kubwa sana. Nimwombe Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* basi atuambie kwamba ni nini, kodi hii lazima iwe ya pamoja,haiwezekani ukienda Mtwara ukute asilimia mbili, ukienda Bukoba ukute asilimia tatu, ukienda maeneo mengine, inakuwa inatofautiana. Kwa hiyo lazima nchi nzima iwe *uniform,* kama asilimia 0.01 kwa ajili ya *city levy* iwe hivyo, kama ni asilimia tatu basi iwe hivyo, lakini utofauti unaoletwa kwa kila halmashauri sio mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la *capacity charge*. Kuna tozo ambayo ipo kwenye umeme inaitwa *capacity charge,* kwa kawaida wazalishaji ukienda kwenye kahawa tuseme labda tutumie mfano, lakini ukienda kwenye viwanda vya korosho huwezi kuzalisha kwa mwaka mmoja, kuna kipindi fulani ambacho wanafunga uzalishaji. Sasa unapofunga uzalishaji bado Serikali au kwa maana ya *TANESCO* wanaendelea kukutoza gharama za umeme kwa asilimia 75 katika mwezi wa kwanza kutokana na *previously* bili yako. Bili uliyolipa mwezi uliopita tunazota asilimia 75 mwezi huu, halafu ukiacha tena kuzalisha au kutumia umeme, mwezi unaofuata unatozwa asilimia 50. Hii imekuwa kero kubwa sana kwa wafanyabiashara, kwa hiyo tunaomba sasa tuachane na hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine tumeona walifanya marekebisho hapa sasa hivi *crude oil,* nafikiri itaingia kwa asilimia sifuri, lakini tuangalie na viwanda vya ndani. Unapoamua kuruhusu wafanyabiashara wa nje kuingiza mafuta pasipo kutoza kodi, tafsiri yake unakwenda kusababisha upotevu wa ajira au uzalishaji, lakini tuangalie namna gani hili jambo tunakwenda kulifanya. Kwa vyovyote vile kama sisi Wajumbe wa Kamati ya viwanda na biashara tulikuwa tunajadili ili mara nyingi, utakapomruhusu mwekezaji wa nje aingize ndani mafuta ghafi kwa asilimia sifuri, ndio nia ni njema kutaka kupunguza gharama za mafuta hapa nchini, lakini tuone namna gani tunakwenda kuathiri viwanda vinavyozalisha mafuta hapa nchini kutokea *level* ya chini, maana yake kwamba wao wananunua alizeti, watakwenda kuzichuja mafuta, watafanya *refinery* baadaye wanaziingira sokoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoleta *crude oil* kwa asilimia sifuri, watu wataondoka. Tulikitembelea kiwanda kimoja Dar es Salaam, siwezi kutaja jina, lakini alikuwa analalamika kwamba wanaoleta mafuta toka nje wana-*declare* kwamba ni *crude oil,* wanafikia kwenye *process,* labda katikati ya *process* nzima ya uzalishaji. Kwa hiyo unaweza ukakuta gharama yake ni chini zaidi kuzalisha na kikubwa anachofanya ni kusafisha na kufanya *packaging,* lakini wale watu wana watu wanaonunua alizeti mitaani, wana watu wanaosafirisha alizeti kuleta viwandani, lakini pia kuna watu wanaofanya kazi ya kupepeta, kuchekecha hizo alizeti mpaka zinakuwa mafuta. Kwa hiyo tuone namna gani tutavisaidia viwanda vya ndani pamoja na nia njema ya Serikali kutaka kupunguza hizo gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la kodi kama ambavyo nimesema hapo, tunapoweka kodi nyingi kwenye viwanda, kwa vyovyote vile vitapunguza ajira, tunapoamua kusaidia viwanda kwa kupunguza kodi na sehemu kubwa ndio tunayosema *VAT,* tumeona hapa Serikali imeamua kufanya *VAT refund* hapa karibuni, lakini pia tumeiona Serikali inajaribu bado kutaka kuwasaidia wale wawekezaji wa ndani.  Mfano, nilioutoa kwenye mafuta unafanana pia mfano huo kwenye viwanda vya bati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona sasa hivi kuna viwanda vingi sana vya bati vimeingia Tanzania, lakini wenzetu nitataja kwa jina *ALAF,* wao *ALAF* wanachokifanya wananunua *rollers* zile *bar rollers,* mara nyingi ukiangalia ukiwa unatoka bandarini unaziona na wao wanaanza *process* kuanzia ya kwanza kuchukua zile chuma, kuzibonda, kuzi-size, kuzipiga rangi na baadaye kuziweka migongo na kuzikata, lakini kuna viwanda ambavyo wanaingiza hizo *material* zikiwa tayari karibu na kuwa *semi-finished,* wakifika hapa Tanzania kazi wanayoifanya ni kupiga rangi na kuweka migongo na kuzikata na kuziingiza sokoni. Kwa hiyo unaweza kuwa na kiwanda cha bati chenye watu 20…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi na mengine nitayaleta kama mchango wangu kwa maandishi.  Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kanyasu, wajiandae Mheshimiwa Msongozi na Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, lakini pia kwa namna ambavyo hotuba imejielekeza kwenda kujibu kero za msingi ambazo zilikuwa zinasumbua hasa katika maeneo ambayo nimeona kwenye eneo la uvuvi ambalo nina *interest* nalo na eneo la madini. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Rais hasa kwa kuondoa kwa kweli utaratibu uliokuwa unatumiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania, pamoja na kazi yao nzuri ya kupitia mahesabu ya nyuma, hii watu wengi sana sio tu walikuwa wanapata tabu, lakini ukweli ni kwamba ukiniambia nitoe hesabu ya miaka kumi, miaka sita iliyopita lazima litaishia kwenye mazungumzo na ninayefanya naye hesabu. Kwa hiyo namshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuliona hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali mwezi huu ilitoa bilioni mia moja kwa ajili ya ku-*control* bei ya mafuta na kusaidia kupunguza mfumuko wa bei. Naipongeza sana Serikali kwa hatua hiyo, lakini kama ambavyo watu wengi wanataka kujua bado tuna hamu ya kufahamu ufanisi wa jambo hili. Mimi ambaye ninatoka katika Kanda ya Ziwa, pamoja na jambo kubwa hili ambalo Serikali imefanya bado hatukuona kimsingi ile *impact* kubwa ya hii fedha ambayo imewekwa na nadhani kuna haja ya kuwa na *transport equalization fund* ili kumfanya Mtanzania anayeishi Dar es Salaam, ugumu ya maisha na urahisi wa maisha yake usitofautiane kwa kiwango kikubwa sana na mtu anayeishi Kagera, Kigoma na Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kutoa mfano, kwamba pamoja na fedha hizi zote kuingia, lakini kule hazijasaidia sana kupunguza gharama za usafiri, zimebaki pale pale, bado mfuko wa sementi Geita Mjini ni Sh.24,000, lakini utaona Dodoma hapa ni Sh.15,500 kwa hiyo inaona katika nchi moja kuna tofauti ya Sh.9,000, lakini ukiuliza sababu ni gharama za usafiri. Kwa hiyo kuna haja ya kulitazama jambo hili vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri kwa kufuta ada ya kidato cha tano. Hili ni jambo kubwa sana na laiti Serikali ingejua namna ambavyo Wabunge inapofika muda wa kufungua shule tunavyohangaika kuwalipia watu, basi jambo hili limetusaidia sana. Hata hivyo, niombe ombi moja, bado tuna shida kwenye vyuo vikuu, bado tunatoa fedha kwenye vyuo vikuu kwa kutumia zile *lettings* na vigezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushauri kwa sababu mkopo wa chuo kikuu ni mkopo, madam nataka mkopo na nimejaza fomu ya kuomba mkopo habari ya kuangalia nani anastahili na mwingine hastahili kukopa hili jambo lingeangaliwa vizuri sana ili iwe ni haki ya Watanzania wote waliopata sifa ya kwenda kusoma wapate mkopo. Sasa hivi hiyo *mean testing* yao inamwacha mtoto yatima, ninao watoto wawili ambao ni yatima, lakini kwa bahati mbaya walipata wafadhili kusoma na wafadhili waliowafadhili walishakufa, kwa hiyo hawawezi tena kwenda kusoma na wameshindwa kusoma kwa sababu wamekosa mkopo. Nimejaribu sana kwenda kwa Mkurugenzi wa Bodi lakini ilishindikana, kwa hiyo jambo hili liangaliwe vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nimeliona kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri, amezungumzia sehemu ambapo anaomba Bunge limpe ridhaa ya kusamehe baadhi ya kodi, niipongeze sana Serikali hasa Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo anazunguka huko nje na kutengeneza picha ambayo inavutia wawekezaji kuja Tanzania na hili ni jambo zuri sana. Hata hivyo, ni lazima twende na tahadhari kubwa, tumekuwepo na *harmful tax incentives* ambazo kimsingi hazijawahi kuisaidia nchi. Ukiangalia huko nyuma kote ambako tulikuwa tunalalamikiwa kwamba Serikali inapoteza *trillions of moneys* ni kwa sababu ya misamaha mikubwa ya kodi ambayo tulidhani inavutia wawezekaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji wanakuja kwa mambo makubwa, yapo machache. La kwanza, wanakuja kwa sababu ya hali ya usalama. Pili, wanakuja kwa sababu ya kutabirika kwa nchi ile *(predictability)* yaani kama nchi inakuwa na sera zisizotabirika tabirika mwekezaji hawezi kuja. Tatu, anakuja kama *infrastructure* na *energy supply* ni kubwa. Nne, anakuja kama kuna masoko na *human resource*. Sasa unaweza ukaweka *incentive* ya fedha haijawahi kusaidia kumfanya mwekezaji aje, kwa sababu mwekezaji anakuja kwenye eneo hata ambalo wewe hujampa *incentive* kama anapata *profit* anakuja. Kwa hiyo hili ni angalizo ambalo inatakiwa kuliona. Kwa sababu juhudi kubwa hizi zinafanywa na Serikali, lazima pia tuangalie kwenye mianya ambayo tunaweza tukajikuta tunapoteza fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye eneo ambalo sasa hivi linatupatia fedha nyingi za kigeni la madini. Tunafanya vizuri sana kwenye madini, lakini bado tuna

shida moja kwenye madini. Niliwahi kusema hapa kwamba, haya madini tunayoona kwa wachimbaji wadogo wanayauza mpaka anapata labda gramu moja ameshakula hasara yenye thamani ya gramu 10. Sasa hapo niombe mambo mawili; moja tuimarishe sana *GST* na watu wa *STAMICO* ambao wanafanya mambo ya utafiti, lakini tubadilishe mfumo wa kutoa leseni kwa gharama ile ile. Unakuta mtu amepewa leseni anachukua leseni ya *PML, SML, MML* anaitunza kwa miaka 20 kwa kulipa *fee* tu kumiliki leseni. Wenye leseni walazimishwe kufanya utafiti halafu tuweke *rates* za leseni kulingana na *deposit* au *value* ya kitu kilichopo pale chini, ili huyu mtu kama akichelewa kulipa kwa miaka mitano aone gharama ya kutunza ile leseni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, niende kwenye utalii, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Rais hasa kwa filamu hii ya kuitangaza Tanzania. Ukweli ni kwamba Watanzania wengi hatufahamu kwamba nchi yetu huko nje ilikuwa haijulikani. Tulipata bahati hapa, Mheshimiwa Spika alitupeleka nje tulikwenda China, tumefika kule mtu ukisema Tanzania lazima a-*google* kuitafuta ilipo, halafu akitazama pale mtu wa kwanza anayemjua ni Nyerere, basi anasema Oooh! Nyerere's *country* basi. Kwa hiyo, kuna watu duniani hawajui kama Tanzania ipo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuitangaza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa juhudi hizi za kutangaza Tanzania na kuvutia watalii zinakuja sambamba na maandalizi tuliyonayo. Jambo kubwa sana amesema hapa Mheshimiwa Sima asubuhi, duniani huko watalaii wanataka kwenda kwenye nchi ambayo usalama ni wa uhakika. Kwa

hiyo, jambo la usalama ni la msingi sana. Tetesi zozote zinazoashiria kutokuwepo kwa usalama zinamfanya anayefikiria kuja Tanzania asije na ukiona kama jirani yako au mwenzako yeyote anatangaza sana ubaya wa usalama kwenye nchi yako, maana yake hiyo tayari ni vita ya kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa ni lazima tuangalie vizuri. Naiomba Serikali jambo hili isilichukulie poa, kwenye biashara ya utalii hakuna mtu atakwenda kwenye nchi ambayo ana taarifa za kwamba wananchi wanapigana na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la pili ni ukarimu. Tanzania lazima tujue kwamba ili tuweze kuwapokea watalii wengi lazima tufanye maandalizi. Maandalizi haya ni pamoja na kulinda maeneo yetu ya asili, na pili kuandaa sehemu za kuwapokea. Sasa ipo shida kidogo ambayo niliiona juzi hapa na ninaomba niseme vizuri, inaweza kuwa ni *misconception* au ni *misleading* ambayo imetokea kwa wananchi wa Loliondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotakiwa kufanyika kwenye eneo lile siyo kuigeuza Loliondo nzima ile ya *square* kilometa 4,000 kuwa *game reserve*. Ni kiini cha *Lake Natron* na sehemu ndogo ya *square* kilometa 1,500 kwa sababu kubwa mbili. Moja, lile ziwa kuna ndege ambao wanakuja kuzalia pale na wanakwenda Ulaya, lakini limeendelea kupata *seriation* kutokana na uingiliaji wa watu. Kwa hiyo, lazima tulinde nusu ya lile eneo. Naipongeza sana Serikali kwa juhudi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, wanyama wote unaowaona, wana maeneo maalum ambapo huwa wanakwenda kufanya mazalia na maeneo ya mtawanyiko. Kwa hiyo, kale kaeneo lazima ukalinde. Sasa inawezekana kuna taarifa zisizo sahihi ambazo zinasambaa za kufikiri eneo lote lile zima wananyang'anywa wananchi na kupewa wawekezaji, jambo ambalo naamini siyo sahihi. Kwa sababu maandalizi ya andiko hilo yalifanywa na wizara na yakapelekwa kwa viongozi na yakafanyiwa kazi vizuri. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali, elimu ya kutosha ipelekwe eneo hili, watu wasipewe picha ambayo siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne, ambalo nataka kuzungumza ni eneo la uvuvi. Miaka ya nyuma tulikuwa na *TAFICO* na nimeona hapa Mheshimiwa Waziri umeweka *TAFICO* unataka kuwapa fedha. Mimi nilipata bahati ya kusoma uvuvi na nilipata bahati ya kufanya *field TAFICO,* sielewi mnakwenda kufanyaje *TAFICO* ili ije kutusaidia kutoka kwenye mchango wa kiuchumi. Maana yake sasa hivi uvuvi unachangia chini ya 3% kwenye *GDP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu sana. Miaka ya nyuma, mwanzoni mwa mwaka 2000 uvuvi ilikuwa ni kwenye *export;* kwenye *forex* ilikuwa ni zao la pili Tanzania kwa kuingiza fedha za kigeni. Tumekuja tukavuruga wenyewe. Nimeona hapa umetoa *exemption* ya nyavu, hakuna kodi, lakini tulivuruga wenyewe. Wawekezaji wenye viwanda ndiyo walikuwa wanaleta nyavu. Wakileta nyavu, wanawauzia wavuvi. Sasa zote zikakamatwa, zikachomwa moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ombi langu hapa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tutengeneze sera ambazo siyo kila atakayekuja kwenye Wizara hii atabadilisha ili wavuvi waweze kuvua vizuri.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kanyasu. Ni kengele ya pili, ahsante sana.

**MHE. COSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club* anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa kesho tarehe 18 kutakuwa na mechi ya kirafiki kati ya *Bunge Sports Club* na Waandishi wa Habari wa Michezo *Taswa Sports Club* kuanzia saa 10.00 alasiri kama ifuatavyo; Mpira wa Miguu Uwanja wa Jamhuri, Mpira wa Pete Uwanja wa Chinangali.

Waheshimiwa Wabunge na wakazi wote wa Dodoma mnaombwa kuhudhuria.

Mheshimiwa Msongozi, halafu Mheshimiwa Neema jiandae.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia katika bajeti hii kuu. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa utendaji wake mzuri sana uliotukuka. Kimsingi Mheshimiwa Rais anafanya

vizuri sana katika sekta mbalimbali. Amejipambanua hivyo kama mwanamke mahiri ambaye kimsingi sisi kama Watanzania tunajivunia yeye kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nimpongeze sana Waziri wa Fedha kwa namna ambavyo amekuwa akifanya kazi nzuri ya kumsaidia Mheshimiwa Rais pamoja na viongozi wengine waandamizi; Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na pia nampongeza sana Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha pamoja na *delegation* yote. Mnafanyakazi nzuri sana, Mungu awatangulie katika utekelezaji wa majukumu yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kazi zote zinazofanywa na Mheshimiwa Rais za kuhakikisha kwamba maendeleo ya nchi yetu ya Tanzania yanaendelea kukua, lakini pia ipo haja ya kuangalia vizuri zaidi masuala mazima ya usalama katika nchi yetu. Ninavyosema hivyo ninamaanisha. Zipo barabara za pembezoni ambazo zinaunganisha nchi ya Tanzania na nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii nitaizungumzia barabara ya Chiwindi mpaka Lumesule yenye kilometa 535. Barabara hii ni barabara ambayo inapita pembezoni mwa Mkoa wa Ruvuma kwenye Mto Ruvuma ambapo sasa Mkoa wa Ruvuma ndio kiunganishi cha nchi ya *Mozambique*. Kwa misingi hiyo, ninaizungumzia hii barabara kwa sababu ni barabara ya kiulinzi na kule Mkoani Ruvuma Mkuu wetu wa Mkoa ni Mwanajeshi. Kwa hiyo, mara zote amekuwa akiomba sana hii barabara iweze kutengenezwa kwa ajili ya kusaidia masuala ya ulinzi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni kwa sababu barabara hii inaungana na Mkoa wa Niassa, siyo Nyasa; Mkoa wa Niassa wa Nchi ya *Mozambique,* katika Jimbo la Niassa nchini *Mozambique* ambako sasa hivi kumekuwa na tishio kubwa sana la vikundi mbalimbali vya ugaidi. Kwa hiyo, ndugu zangu naomba sana hii barabara iende ikaanze kutengenezwa kwa kiwango cha lami ili kuweka mazingira mazuri ya masuala ya ulinzi katika maeneo hayo. Tusisubiri mambo yakaanza kujitokeza halafu ndiyo tunagundua shuka wakati kumekucha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie suala la pili ambalo linahusu Ngorongoro na Loliondo. Ngorongoro ilianzishwa mwaka 1959 na Ngorongoro hii kimsingi ndiyo maeneo ambayo yana mfumo wa ikolojia ambapo maeneo mahsusi katika yanatambulika kwa majina haya yafutayo: Natron, Longido, *Enduimet* na mfumo huu wa ikolojia unakwenda mpaka Manyara na Tarangile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa eneo hili la Ngorongoro ulitambulika mwaka 2010 eneo hili sasa limetambuliwa kama ni eneo la urithi wa dunia. Kwa misingi hiyo, na kwa umuhimu wake, kuna mambo ya urithi wa kidunia lakini pia kuna mambo ya kitamaduni. Kipekee kabisa, naomba nitaje baadhi ya vitu ambavyo vinapatikana hapo Ngorongoro pamoja na kwamba baadhi ya Wabunge wamezungumza vitu vingi vinavyopatikana, nami nitataja vichache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *creator* tatu kubwa ambazo zipo pale Ngorongoro, lakini pia kuna wanyamapori wa kila aina pale Ngorongoro wakiwemo ndege wa aina mbalimbali. Pia kuna mchanga mweusi

pale Ngorongoro na huo mchanga una tabia ya kuhamahama. Mchanga wa aina hii huwezi kuupata mahali pengine popote pale duniani, unapatikana Ngorongoro tu. Kwa hiyo, ni vitu muhimu sana vya kuvilinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie kuhusu Mheshimiwa Rais namna ambavyo amejikita kwenye suala la *Royal Tour* na amefanya vizuri sana katika eneo hili na wengine wamesema katika kutangaza nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitaje faida kubwa ambazo zimepatikana mpaka sasa hivi baada ya Mheshimiwa Rais kujitoa na kuhakikisha kwamba anatangaza kupitia hii video ya *Royal Tour*. Mambo ambayo tumefanikiwa kwa sasa hivi nataka niseme, watalii wameongezeka na wamekuwa wengi sana sasa hivi na viashiria vya kuongezeka kwa watalii vinapatikana hapa ambapo tunaona kabisa kumekuwa na ongezeko la watalii ambao wameshafanya *booking* kwenye zile hoteli ambazo zipo huko Mbugani. Mwaka mzima huu hakuna nafasi, kupo *full booked*. Kwa hiyo, hii ni moja ya viashiria kwamba utalii unakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kumekuwa na wawekezaji wa mitaji mbalimbali. Wawekezaji wa masuala ya hoteli wamejitokeza wengi ambao wanahitaji kuwekeza katika eneo la Ngorongoro. Kuna kampuni ya Mariot na kiwanda kikubwa sana cha Wachina ambapo wanakuja kwa ajili ya kutengeneza magari, wana-*reassemble* magari ambayo yatakuwa ni *special* kwa ajili ya watalii. Kwa hiyo, hivi ni viashiria vikubwa sana kwamba uchumi wetu unakua.

Pia kupikia suala la Ngorongoro, napo pia tunanufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kwa mashirika mbalimbali ya ndege; kwa mfano, kuna *Air Qatar* ambapo kwa kipindi cha wiki moja wanaweza wakafanya *trip* mpaka 15. Pia tumeona Mheshimiwa Mbarawa, amekubaliana na nchi ya Marekani ya kwamba ndege zipelekwe Marekani zitoe watalii Marekani moja kwa moja wanaenda kutua maeneo husika; na maeneo ya Ngorongoro kwa ajili ya kuboresha masuala ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niseme hivi ndugu zangu, tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri hii ambayo ameifanya. Pia wamekuwa wakijitokeza watu ambao hawaitakii mema nchi yetu na kwamba suala la utalii sasa hivi kwa kuwa ajenda kubwa ni kukuza utalii katika nchi yetu ya Tanzania kutoka watalii 1,500,000 hadi kufikia 5,000,000 ifikapo mwaka 2025, kwa hiyo, ajenda hii iliyofanyika ya *Royal Tour* kwa vyovyote vile imewastua hata majirani zetu kwamba eneo hili linaendelea kukua kwa kasi, na ushindani huu umekuwa ni mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana wale watu wote wenye nia mbaya ya kutaka kudhoofisha ajenda hii ya utalii ambayo imefanywa na Mheshimiwa Rais, kwa kweli tuwapige vita vibaya sana wasiweze kupata nafasi yoyote ya kuweza kuchukua huu uhalisia uliopo wa kupambana dhidi ya masuala ya uchumi kupitia utalii na baadaye wakaenda kujinufaisha wao kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninawalaani wapotoshaji wote katika mitandao ya kijamii, na hao wote wanaopotosha kwa namna moja au nyingine hawana tofauti na maharamia. Kwa hiyo, tusichukulie poa kama ambavyo wengine wamesema.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nataka kuzungumzia suala la *EPZ*. Kumekuwa na suala la *EPZ,* kuchukua maeneo mbalimbali katika nchi yetu. Maeneo haya wanayahodhi kwa muda mrefu likiwepo eneo la Kata ya Mwengemshindo katika Mkoa wa Ruvuma, Wilaya ya Songea Mjini wamechukua eneo la *EPZ*. Mpaka sasa hivi ni takribani miaka 14 wananchi wale wamekaa hawajui hatma yao, hawaelewi wafanye nini na wamezingirwa na vichaka, hawawezi kufanya maendeleo ya jambo lolote lile.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Ni kengele ya pili.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri. Ukiyazingua mazingira na mazingira yatakuzingua na wewe vilevile. Kwa hiyo, tulinde mazingira kama anavyosema Mheshimiwa Msongozi.

Waheshimiwa wageni waliopo Bungeni muda huu ni wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, Timu ya

Waandishi wa Habari wa Michezo Tanzania *(Taswa Sports Club)* wakiongozwa Ndugu Majuto Mali na mfadhili wao Ndugu Allen Mushi ambaye ni Mkurugenzi wa Masoko wa Kampuni ya *M-BET* Tanzania. Karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Tarimba ameahidi kesho atakuja na kitezo kile. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Neema, halafu wajiandae Mheshimiwa Matiko na Mheshimiwa Condester.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika bajeti hii iliyoletwa mbele yetu na Waziri wa Fedha. Kipekee napenda kuwashukuru viongozi wa Wizara hii, Waziri, Mheshimiwa Mwigulu pamoja na Mheshimiwa Hamad Chande kwa namna ambavyo wamekuwa wakiendelea kufanya kazi vizuri. Pia nawapongeza Katibu Mkuu wa Wizara hii na Manaibu wote kwa namna ambavyo pia wamekuwa wakitekeleza majikumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee zaidi namshukuru Mheshimiwa Rais wetu kwa namna ambavyo amekuwa akifanya mambo mzuri, nami kama mwakilishi wa Mkoa wa Songwe, ninayo mengi mazuri ambayo najivunia ambao Mheshimiwa Rais ameweza kufanya kwa ajili yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitapenda kuongelea masuala machache ambapo suala moja kubwa ni kuhusu mkataba huu ambao umesainiwa wa uuzaji wa makaa ya mawe, ambapo nchi yetu ya Tanzania itaenda kuiuzia makaa ya mawe nchi ya *Switzerland,* na tumesaini

mkataba wa kuuza tani 60,000 za makaa ya mawe kwa hiyo nchi ya *Switzerland*. Kwa sisi watu wa Mkoa wa Songwe hususan Wilaya ya Ileje, ni fursa nzuri sana ambayo kwa kweli tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutusaidia kuweza kuipata hii fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu Wilaya ya Ileje ni moja ya wilaya ambazo zinamakaa ya mawe mengi sana katika nchi hii. Kwa taarifa ambazo zipo na zilizofanyiwa utafiti zinaonesha kuna *reserve* ya tani milioni 100 ya makaa ya mawe katika eneo hili kitu ambacho kwa kupitia huu mkataba uliosainiwa, tani 60,000 tutauza kwa *4.4 billion* inaonesha kwamba kama tutafanikiwa kuuza haya makaa yote ya mawe ambayo ni tani milioni 100, kwa nchi yetu tunaweza tukaingiza kiwango cha Shilingi bilioni 6,900. Nadhani ni pesa nyingi sana ambapo kama nchi tunaihitaji kwa ajili ya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huu uliosainiwa utekelezaji wake unaenda kuanza ndani ya mwezi huu. Kwa namna hiyo, kupitia huu mkataba ambao ni wa miaka mitano, ina maana ya kwamba tutaweza kuvuna tani milioni 3.6 tu, kitu ambacho tunaona kwamba bado tunayo fursa ya kutafuta mikataba mingine mingi zaidi ili haya makaa ya mawe yaweze kutumika na kuliletea Taifa letu kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema nini? Kweli tumepata mkataba, lakini tunafahamu kwamba haya makaa ya mawe yaliko bado miundombinu haijakaa vizuri hususan kwenye barabara. Nilitamani kuiomba Wizara hii iweze kuweka kipaumbele cha ujenzi wa barabara hii ya

kilometa saba ambayo fedha yake imetengwa kupita *TARURA,* badala utekelezaji uende kufanyika kupitia *TARURA,* tulitamani kwamba utekelezaji huu ufanywe na *TANROAD* ili iweze kufanyika kwa haraka sana kulingana na umuhimu wake ambao upo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kama barabara haitakaa vizuri ina maana uzalishaji na usafirishaji wa haya makaa ya mawe itakuwa ni changamoto kubwa. Kwa hiyo, kwa maana ya ujenzi wa kiwango cha lami kupitia *TANROAD* utafanyika kwa haraka kitu ambacho tutakuwa tumeisaidia nchi yetu kurahisisha uuzaji wa haya makaa ya mawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema nini? Mpaka sasa hivi hii barabara ya kilometa saba imekuwa haitumiki. Kwa hiyo, wanatumia barabara nyingine mbadala ambayo ina kilometa 36 ambapo kwenda na kurudi unakuta kilometa 72, kitu ambacho kinaongeza gharama za usafirishaji wa yale makaa mpaka ile *selling point* ya haya makaa ya mawe. Ukiacha hivyo, pia ule mzunguko wa usafirishaji wa makaa ya mawe unachukua muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, najaribu ku-*justify* kwamba ujenzi wa hii barabara kwa kilometa saba kwa Serikali itaweza kuipunguzia gharama zisizokuwa za lazima. Kwa hiyo, nawaomba kwamba ile fedha iliyotengwa *TARURA* ihamishiwe *TANROADS* ili zoezi liweze kufanyika kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha hilo suala la barabara, pia tunafahamu kabisa kwamba pale Kyela kuna Ziwa Nyasa ambapo tumekuwa na mkakati wa ujenzi wa meli na meli zilizojengwa mpaka sasa hivi kwa usafirishaji wa mizigo hii zinaonekana ni ndogo, kama kweli Serikali ikiamua kuwekeza kwenye ujenzi wa meli nyingine mpya kubwa ya mizigo, itarahisisha usafirishaji wa haya makaa ya mawe kuelekea Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kabisa kupita Ziwa Nyasa kwenda Mtwara ndiyo inakuwa njia nyepesi ya usafirishaji wa mizigo kuliko kusafirisha haya makaa ya mawe kupitia barabara ya kutoka Kyela, Mbeya, Makambako mpaka Songea kuelekea Mtwara. Kwa hiyo, naishauri Wizara ione umuhimu wa kuwekeza katika Ziwa Nyasa, kujenga meli nyingine mpya kubwa ya mizigo ili tuweze kusafirisha kwa urahisi na kwa namna hiyo tutakuwa tunazilinda barabara zetu ambazo tunazijenga kwa gharama kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuliongea hilo, natamani kuongelea katika kipengele cha *TAZARA*. Ninaongelea *TAZARA* kwa uchungu mkubwa kwa namna ambavyo imeharibika, imechakaa. Kitu ambacho tunajua, kama tuliweza kukaa awali, tukatengeneza hiyo sheria ambayo ipo na tukawa tunaitekeleza na sasa inaonekana kwamba hiyo sheria inakuwa kama haitupi fursa ya uwekezaji sisi kama Watanzania, tuone namna ya kuweza kupitia hii sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, natamani kuona Serikali inachukua hatua kwenye kufuatilia utekelezaji wa hiyo sheria ambayo inaifanya Tanzania ishindwe kuendelea

kuwekeza katika *TAZARA*. Kwa namna hiyo, kama sheria ikibadilishwa tunaamini tutanunua mabehewa lakini pia tutawekeza kwenye *repair* ya hii reli ya *TAZARA*. Hivyo, Serikali iione *TAZARA* kwa jicho la kipekee. Kwa sababu tunaamini kabisa lengo la ujenzi wa *TAZARA* ilikuwa ni kusafirisha mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam kuelekea nchi za *SADC*. Kwa namna hiyo na tunafahamu kabisa asilimia 70 ya mizigo inayoingia bandarini inaelekea nchi ya Malawi, Zambia na Congo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niiombe Serikali ilichukue hili kwa kipekee iweze kupitia hiyo sheria na kupitia kama tutaweza kuboresha utendaji kazi wa *TAZARA*. Tuweze kufikiria ni kwa namna gani tutengeneze bandari kavu katika eneo la Mpemba pale Tunduma. Tunajua kabisa bidhaa nyingi wanaonunua ni watu wa hizi nchi za *SADC,* kwa nini tusione umuhimu wa kujenga hii bandari kavu pale? Kwa sababu tutakuwa tumerahisisha mambo mengi, kwa sababu barabara zetu hazitaharibika lakini mizigo itafika kwa wakati. Uratibu wa mizigo utakuwa ni kwa haraka kwa sababu itakuwa ipo *specifically* kwa eneo la watu wa *SADC*. Kwa hiyo, ipo haja ya kuona Serikali inachukua hatua kwenye ujenzi wa *dry port* Tunduma pia kwenye utengenezaji wa hiyo meli, hii itachangiza uanzishwaji wa *free market* katika eneo la Tunduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Matiko na Mheshimiwa Conchesta ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami ninakushukuru kwa kuweza kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye hotuba ya mapendekezo ya Serikali ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kwa kweli kwa kushukuru na kutambua jinsi Serikali ambavyo imeona iweze kuhakikisha kwamba watoto wa kaya maskini na wenyewe wanapata elimu kama vile wanavyopata wenzao na kwa kuanzisha Mfuko Maalum ambao kwa mwaka huu wa fedha wametenga Shilingi Bilioni Nane na wameelekeza kwamba zitaenda *TASAF* ili kwa wale watoto wanaotoka kwenye kaya maskini wanaoshindwa kujiendeleza na shule ya sekondari waweze kwenda kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika hili napenda kushauri. Pamoja kwamba mna nia njema na imeelekeza kwamba *database* inapatikana *TASAF* na kutoka kwa Wabunge na Madiwani, napenda kushauri kwamba wale Maafisa Maendeleo ya Jamii ndiyo ambao wanajua na wako pale wanajua hizi kaya maskini wanaweza kuwa na *database* nzuri. Huko nyuma tuliwahi kushauri kama ingependeza *TASAF* ingeweza kutoka Utumishi ikaenda ikawa chini ya hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii maana yake ndiyo wanaozitambua hizi kaya maskini, ndiyo maana hata tunaweza kuona kunakuwa na changamoto nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi ili kuweza kuona hizo Shilingi Bilioni Nane zisiwe *misused* ziweze kwenda kwa walengwa ambao ni walengwa hasa ambao wanatakiwa waweze kupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia na hili suala la kuondoa ada kwa Kidato cha Tano na cha Sita ni jambo jema, lakini tuangalie sasa ni vipi tunafanya elimu inakuwa bure kuanzia shule ya msingi, sekondari na hata kidato cha tano na cha sita, siyo kuondoa ada tu wakati unaacha mlundikano mkubwa wa michango ambayo wazazi wanashindwa kumudu na watoto wanapelekea kutokwenda shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine sasa najielekeza kwenye mchango wangu ni kuhusu kuhusiana na hali ya umaskini kwa Taifa letu. Mpango wa maendeleo wa miaka mitano uliainisha kabisa kufikia mwaka 2025 tuwe walau tumefikia asilimia 22, tupunguze umaskini wetu kwa asilimia 22. Kwa *data* zilizopo mwaka 2018 kiwango cha umaskini kilikuwa ni asilimia 26.4, kwa uwiano wa kwamba vijijini 2018 ilikuwa ni asilimia 31.4, tunagemea kwamba ikifika 2025 basi tuwe tumeshuka kwa vijiji kufika asilimia 28.1. Kwa Mijini kutoka asilimia 15.8 mpaka asilimia 13.2 kwa mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sasa umaskini wa mahitaji maalum kwa Watanzania kwa kipindi cha miaka 10 umepungua kwa asilimia 1.8 tu. Kwa maana mwaka 2012 ilikuwa ni asilimia 28.2, mwaka 2021 ilikuwa ni asilimia 26. Ukiangalia hapo tumeweza kumudu kupunguza umaskini kwa asilimia 1.8 tu kwa miaka 10, tumepunguza kwa asilimia 1.8. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa nini nimesema hii? Ili tuweze kuondoa umaskini kwa Mtanzania lazima tuhakikishe kwamba tumemuinua kiuchumi. Sasa ukiangalia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameainisha kabisa

kwamba anaenda kupunguza kwenye zile asilimia 10 ambazo zilikuwa zinamuinua, makundi maalum yale ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, anaenda kupunguza asilimia tano anazipeleka kwenye miundombinu na masoko ya wamachinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inakuwa inazidi kurudisha nyuma katika kuhakikisha kwamba unamuinua Mtanzania mmoja mmoja aweze kujiinua kiuchumi. Ninashauri tu kwamba, lengo linaweza kuwa lipo vizuri, lakini mosi halitakuwa na uwiano katika Halmashauri zenye mapato makubwa na zile Halmashauri hazina mapato kabisa. Leo kwa mfano kule Tarime tukijikakamua sana Tarime Mjini ni kati ya shilingi milioni 900, shilingi bilioni 1.1, shilingi bilioni 1.3; ambapo asilimia 10 ni shilingi milioni 130, asilimia tano unazungumzia shilingi milioni 50 mpaka milioni 75. Kusema hawa watu wajenge masoko na miundombinu kwa shilingi milioni 50/50 hizo wadundulize kwa miaka takribani 20 wakati huo hata yale makundi maalum umewanyima hizo fedha, *then* miundombinu inakamilika hawajaweza kujiinua kiuchumi, sasa hayo majengo wanaenda sasa wanaingia popo, maana yake yanakuwa hayana watu ambao umewa-*empower* kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukilinganisha na Dodoma Jiji mapato yao labda shilingi bilioni 40, shilingi bilioni 50 asilimia 10 kwao *it makes sense* inakuwa ni shilingi bilioni tano. Ukichukua *plus* shilingi 500 hapo ni shilingi bilioni 2.5, hawa *at least is viable* kwao. Kwa hiyo, tuliangalie hili wazo, *it's not practical at all. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine Serikali lazima itafute fedha, ijenge miundombinu hii ya masoko ambayo

yatakuwa na *uniformity* Tanzania nzima. Kama unajenga Dodoma soko la machinga *complex* kama hili ambalo tumeona, basi na Mwanza lijengwe na Tarime lijengwe na kwingineko kote. Inaweza ikapungua tu ukubwa lakini uwe na *uniformity* ya muonekano ulivyo. Leo ukisema tudundulize shilingi milioni 20, shilingi milioni 30 ndiyo unakuta yaani visoko vya ajabu ajabu. Kwa hiyo, hili mimi napingana nalo na naishauri Serikali iende iwaze vema katika hili, kuleta usawa kama tulivyofanya kwenye *COVID-19* ile fedha tuliyopata shilingi 1.3, mkatoa fedha zinaelekezwa na zikaonesha miundombinu ilipo na kila mtu ana-*appreciate* sasa hivi anaona, *its tangible* unaweza ukaiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuhusu *capital goods.* Katika zana ile ya kumuinua Mtanzania kiuchumi mmoja mmoja ili mwisho wa siku tuone kabisa uchumi wa Tanzania unakua, amesema kwamba *capital goods* ya shilingi milioni 60 kuendelea ndiyo atapata msamaha wa kodi *VAT*. Mimi nashauri na nashauri hili hata tuweze kuiga kwenye nchi za *South East Asia* zenye *tight economy,* wenzetu wale waliwekeza kwenye viwanda vidogo na vya kati kwa kuviwezesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tupunguze hii fedha, irudi mpaka shilingi milioni 20 ambayo ndiyo *capital goods* iwe hivyo, waweze kupata msamaha wa *VAT*, tutaweza kuibua Watanzania wengi ambao hata hizi fedha ambazo tunazikopesha kwenye Halmashauri zetu, kuweza kuwapa hivi vikundi vya milioni 20 kuweza kuagiza hivyo vifaa, ila sasa wanavyoleta wapitishie, wahakikishe kwamba wanafanya *incubation SIDO* kwa mwaka mmoja kuweza kupata mafunzo. Wakati huo wa kufanya mafunzo unakuta

wameshaingia kwenye *operation* ili sasa kuweza hata ku-*avoid* hizi *charges* ambazo ni tozo, kodi mbalimbali kutoka kwenye mamlaka mbalimbali kwa mwaka mmoja wa mpito hao watu utakuwa umewainua sana. Baada ya mwaka mmoja wanakuwa wameshaji-e*stablish* na wanaweza kulipa na kodi ya Watanzania, kinyume na hapo hatutaweza kuona chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine pia wameweza kuainisha kodi ya mfuto kwa lori na mabasi. Mmesema shilingi milioni 3.5, tuwe na uhalisia. Haya malori kwanza hamjaya-*categorize,* yaani hauwezi kusema unaweka kodi ya mfuto ya shilingi milioni 3.5 kwa lori la tani nne kwa lori la tani 10 sijui tani ngapi ni kuwafanya hawa watu waondoke kwenye hii biashara, ukizingatia *operation cost* ziko juu. Mafuta yamepanda, vipuri vimepanda, mtapandisha kodi mwisho wa siku hizi shilingi bilioni 141 hamtaziona, zitakuwa kama kodi za simu tu. Tukiwa na matarajio zitafika Shilingi Trilioni 1.02, tunaishia kupata hata shilingi bilioni 300 hazifiki, kwa sababu kodi imekuwa kubwa, watu wame-*pull out*. Ndiyo kitakachotokea hapa Mheshimiwa Waziri! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wata-*pull out,* watu wa malori wataacha biashara ya malori, watu wa mabasi wataacha biashara ya mabasi, mwisho wa siku hata zile kidogo mlikuwa mnapata msizipate! Ninashauri, kwanza mzi-*categorize* labla kuanzia tani kadhaa mpaka kadhaa labda walipe shilingi milioni 1.5 na zile kubwa hebu walipe shilingi milioni 2.5 ili kuhakikisha kwamba wote mnawaweka *on board.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi, tumeona kwanza ilivyo sasa hivi bei za vifaa vya ujenzi zimepanda

ukilinganisha mwaka jana na mwaka huu. Kwa mfano, Tarime bei ya nondo kwa mwaka jana Machi, nondo milimita 12 ilikuwa shilingi 21,000, sasa hivi Machi - *training* za *TPSF* walikuja kutupa semina juzi ni shilingi 27,000 ongezeko la asilimia 28.5. Milimita 16 ilikuwa ni shilingi 34,000 sasa hivi ni shilingi 44,000 ongezeko la asilimia karibia ngapi huko. Ukija kwenye mabati ilikuwa 28-gauge ilikuwa ni shilingi 26,000 sasa hivi ni shilingi 40,000 ongezeko la asilimia 53 na mengine mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mmeweka kodi, kwamba mnaweka kodi kwa wanaoingiza *finished goods* ambayo ninakubali, kwamba mnataka mlinde viwanda, lakini hivi viwanda *raw material* zinatoka nje, zile *raw material* zenyewe zinakodi kubwa *at the end of the day* watakuwa hawana hiyo *importation,* achilia mbali hamjafanya *assessment* kujua kama *production capacity* na *surplus demand* ya Watanzania wanavyohitaji. Kwa hiyo, kwenye *raw material goods* zinazokuja zina kodi, mwisho wa siku *operation cost* ikiwa kubwa bado vifaa hivi vitakuwa vikubwa sana na ile dhana ya kuwa na maisha bora kwa Mtanzania haitakuwepo, hatutaweza kujenga makazi bora. Mtu hawezi ku-*afford* kununua nondo kwa shilingi 36,000 tena baada ya Julai itakuwa shilingi siyo 36,000 ni shilingi 40,000 huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *white cement* tulikuwa tunanunua kwa shilingi 33,000 sasa hivi hapa Dodoma ni shilingi 48,000 nani ambaye ata-*afford?* Watajengea fito, watatumia mbao badala ya kutumia chuma na kila kitu, na hayatakuwa makazi bora. Kwa hiyo, nashauri wakati tunaangalia hizi kodi Serikali iangalie kodi ambazo hazimkandamizi Mtanzania bali zinaenda kumsaidia

kumuinua, lakini hata viwanda vyetu kwenye hizo *imported raw materials* mpunguze kodi, muwape *incentives* ili waweze kuzalisha visiweze ku-*pull out of the market*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine nitayachangia kwa maandishi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Conchesta, Mheshimiwa Kakoso, Mheshimiwa Kapufi na Mheshimiwa Mpakate wajiandae.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi nami niweze kuchangia mawazo yangu kidogo kwenye hoja ya bajeti iliyowasilishwa na Waziri hapa kwenye Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuweka hapa muda wote ili tuweze kuweka mipango yetu katika tafsiri ya fedha na nina uhakika fedha tulizozitenga na bajeti ilivyosomwa na mambo yaliyoko ndani ya bajeti kama yakisimamiwa vizuri, utekelezaji ukaleta tija, basi Watanzania wanaweza kuguswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama bajeti hii wako watu watakaofurahi na kuna watu ambao wameguswa hawataweza kufurahi. Kwanza niongezee kwa Mheshimiwa Esther pale aliposema kuhusu watoto wetu wa kidato cha tano na kidato cha sita kuwa katika elimu bure. Niende kwenye ukurasa wako Mheshimiwa Waziri wa 159, pale ulipoweza kuweka fedha ya maendeleo. Umetoa Shilingi

Bilioni 346.5 na ukasema itagharamia elimu ya msingi bila ada.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa neno hilo elimu ya msingi sijajua unamaanisha *basic education* kwamba Tanzania tunapaswa kupeleka mpaka *form five* na *six* au vipi, labda uiangalie vizuri *statement* hii sijaielewa vizuri unaposema elimu ya msingi bila ada sidhani kama unaongeza na watu wa *form five* na *form six*. Basi kama ni aina fulani ya Kiswahili au Tanzania tuambiwe sasa *basic education* ni nini na je, hizi shilingi bilioni 346 zime-*include* na *form five* na *six?* Kwa sababu ni mpango mpya na watoto wengine wameshaenda shuleni. Tunachoomba ni kwamba, Serikali sasa iwe na mpango mzuri kuhakikisha kwamba jambo hili linatekelezeka vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nakwenda na kurasa zako, ukurasa 107 na bahati nzuri kifungu ni 107 ambacho kinasema, kubadili sheria Serikali za Mitaa ile 10 *percent*. Tunapaswa tuiseme wote na hasa sisi wanawake kusema ukweli. Napenda kuuliza ni kwa nini Serikali imegeuza Mfuko huu kama shamba la Bibi? Mfuko huu unatolewa na Halmashauri na umelenga kusaidia makundi maalum, ukitazama tangu sheria hii iwepo hatujapima hata tija na hasa kwa watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napendekeza Serikali itafute Mfuko mwingine, Halmashauri hizi kumbuka mmeshazinyang'anya mapato yote. Mmezinyang'anya mapato yote, majengo, mabango na kila kitu. Kwa hiyo, Halmashauri nyingine zinachechemea. Sasa kila kitu kinachokuja, kila Wizara Halmashauri, kila Wizara hata Bajeti Kuu inasukuma mzigo wa machinga kwa Halmashauri, kwa

kweli jambo hili siyo sahihi na kwa upande wangu mimi sikubali kabisa kwamba, hakikisheni huu Mfuko unabaki jinsi ulivyo. Kama mnaamua kutenga ile *percent* ya vijana kupeleka kwa machinga, mkumbuke wanawake walio wengi siyo wamachinga, basi wasikope Halmashauri muwape Mfuko wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema katika kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali. Umesema maneno mengi, umesema mengi kuhusu magari, mambo ya manunuzi. Napenda kukuongezea vitu kama viwili pale. Kwanza katika manunuzi na hasa katika tenda, Mheshimiwa Waziri uandike hapo, kuna kitu kinaitwa *correction of error,* pale kwenye *tender*, pale mtu anapo-*tender,* labda mmesema kwamba ya chini ni shilingi bilioni moja, lakini anapewa kwa sababu sheria inasema apewe mtu aliye-*tender* kidogo, hiyo sheria inatoa *mandate* kwa watoa *tender* kwenda kurudia zile hesabu za *BOQ*.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta mradi kama ulikuwa wa shilingi bilioni moja, ile *correction of error* inakwenda shilingi milioni 500. Sasa tunashangaa na tumeiona hii kwa sababu niko kwenye Kamati ya *LAAC* na tunakagua miradi, tunakumbana na vitu vya namna hiyo, ni upotevu mkubwa wa fedha, kwa hiyo, uiangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna majengo mapya ya Halmashauri. Kuna maeneo mapya ya utawala. Sasa maeneo haya yanapaswa kujenga ofisi, *is well and good.* Ofisi zenyewe zinajengwa lakini Serikali iweke *limit* ya fedha. Tumeenda katika ziara zetu, tumeenda kwa mfano katika Halmashauri ya Busokelo, tumekuta wamejenga jengo lina vyumba 203 *plus one*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unaweza kujiuliza, Halmashauri inajenga vyumba 203, unajenga na hoteli za kulaza watu mle ndani? Kwa hiyo, tunapenda ofisi zijengwe, ziwe na *standard* na kiwango fulani cha fedha na ramani ambayo itawezesha nyumba hizi kuwa nzuri. Pia tufikirie huduma zaidi inayotoka kwenye majengo hayo kuliko thamani yake na *show*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mtazame namna hiyo kuweza kupunguza kuwe na *standard* kwamba nyumba itajengwa kwa shilingi bilioni mbili basi iwe shilingi bilioni mbili na ramani ziangalie na mahitaji. Kwa hiyo, hakuna sababu ya kujenga yale *bungalows* makubwa ambayo hayana maana. Unaenda kuangalia ofisi ya Mkurugenzi unashangaa kwamba inawezekana hata wewe Waziri wa Fedha hiyo ofisi huna, kwa sababu…..! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nije sasa kwenye *force account*. Hii *force account* katika kutengeneza miradi siyo kitu kibaya. Kinachohitajika Halmashauri ziwe na Wahandisi ambao wanaweza kusimamia. Kipindi fulani nimeshachangia hapa nikasema, Serikali, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Elimu ishirikiane ili wapeleke vijana wetu *VETA*, wale *technicians* wajifunze mambo ya kujenga, mambo ya barabara. Hata ukienda kwenye Chuo cha *VETA* - Dodoma hapa, bahati nzuri mimi nimepeleka watoto wengi kusoma hapo. Wanavyo vitengo vya ujenzi *(mason),* wanavyo na vitengo kabisa vya kujenga barabara. Sasa tunakosa wasimamizi, huku chini Halmashauri zetu hazina *Engineers* lakini *force account* inasaidia kujenga miradi mingi kwa gharama ndogo pia tutazame sasa kile kiwango cha miradi, kama miradi inafikia bilioni sita na kuendelea

tunaweza kuweka Mkandarasi, lakini kama miradi ile ni ya kujenga madarasa, kuna wengine kwa kweli wamefanya vizuri, kwa mfano tulienda Mbeya Mjini wametengeneza hospitali nzuri kabisa kwa *force account,* ukifika pale unaridhika na maeneo mengine ambayo tumepita, kwa hiyo nina uhakika kwamba tunaweza kuendelea na *force account* lakini pawe na usimamizi, hakikisheni ndani ya Halmashauri kunakuwa na *Engineers*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *force account* inasaidia kujenga miradi mingi kwa gharama ndogo, lakini pia tutazame sasa kile kiwango cha miradi kama miradi inafika bilioni sita na kuendelea, tunaweza kuweka mkandarasi, lakini kama miradi ile ni ya kujenga madarasa, kuna wengine kwa kweli wamefanya, ukienda pale Mbeya Mjini wametengeneza hospitali nzuri kabisa kwa *force account,* ukifika pale unaridhika na maeneo mengine ambayo tumepita.

Kwa hiyo, nina uhakika kwamba tunaweza kuendelea na *force account* lakini pawe na usimamizi, Serikali ihakikishe ndani ya halmashauri tunakuwa na ma-*engineer*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba Serikali imeongeza mishahara ni kitu kizuri, lakini mishahara hii iwatazame hata askari. Yapo malalamiko mengi na askari hawawezi kusema, hawawezi kuja hapa, kwa mfano Maaskari Magereza, wanalalamika hawajalipwa posho za chakula, posho za maji, umeme, pango, *per diem* nauli za likizo uhamisho na kadhalika. Kwa sababu ukiwatazama askari magereza kazi zao ziko kule kule ndani, sio watu wanaosafiri sana, kwa hiyo Serikali iwatazame hata kwenye

mshahara yao, kwa sababu Serikali imeongeza mishahara iwaangalia kwamba ni watu ambao wanatunza watu wetu ambao, tuwaite wa kurekebisha tabia tusiwaite wafungwa, wanakwenda kurekebishwa tabia zao huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali iwaangalie, hawajalipwa hizi posho karibu kuanzia 2018/2019, 2019/2020, 2020/2021. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri awafikirie atakapopandisha mishahara, ahakikishe Askari Magereza kama siyo wote, lakini wafanye *assessment* waone ni wangapi ambao wamelipwa na ambao hawajalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimalizie kwa kusema kwamba bajeti hii itoe majibu kwa kutengeneza miundombinu imara na hasa barabara, madaraja, yasimamiwe vizuri na wawe na wataalam ambao wanafanya upembuzi yakinifu ili waweze kutengeneza barabara nzuri, nilikuwa nikiuliza maswali hapa na hasa Bukoba Vijijini katika Wilaya ya Bukoba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Bukoba ni miaka mingi tangu tupate uhuru hatuna barabara ya lami. Sasa tunasema uchumi wa Mkoa wa Kagera umekufa kwa stahili hiyo wameuua wao wenyewe kwa sababu kama hawawezi kutujengea barabara, madaraja, vivuko ambavyo watu wanaweza kusafirisha mazao yao, tutawezaje kupata maendeleo. Pamoja na mambo mengine lakini hata miundombinu katika Mkoa wa Kagera na hasa Bukoba Vijijini kwa kweli wametuweka mahali pabaya na tumelalamika sana hapa, tunapewa majibu mengine kwa kweli ambayo siyo ya kuridhisha. Tunaamua Kwenda tu, basi bora liende, lakini tunaomba watufikirie

zaidi katika kutujengea barabara Bukoba Vijijini, barabara ya lami, watufungulie Jimbo letu, watufungulie wilaya yetu, tunalima migomba, tunalima mbao sasa hivi tunalima miti sana, lakini hatuwezi kusafirisha kwa sababu hatuna hata daraja pale Kalele, nimesemasema sana hapo Waziri Kasekenya ananisikiliza, alikuwa akinijibujibu maneno. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Moshi Kakoso, jiandae Mheshimiwa Sebastian Kapufi.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuwa miongoni mwa wachangiaji. Awali ya yote nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jitihada kubwa sana anayoifanya kuwatumikia Watanzania na kupeleka huduma mbalimbali ambazo kila eneo zimewafikia Watanzania. Hata hivyo, yapo ya msingi ambayo kayafanya, amewaongezea mishahara watumishi wa Serikali, ni jambo kubwa sana na bado kwenye sekta ya elimu ametoa elimu bure mpaka kidato cha sita. Kwenye bajeti hii aliyoleta Mheshimiwa Waziri, hili ni jambo la faraja kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na ushauri kwa Serikali hasa kupitia Wizara ya Fedha kwenye maeneo ya mapendekezo waliyoyaleta juu ya kuhamisha vifungu vya kisheria ambavyo kwenye sekta ya mawasiliano wanainyang'anya Mamlaka ya Mawasiliano *TCRA* wanapeleka kwenye *TBS* ambayo hawatakuwa na uwezo wa kufanya kazi hiyo inayokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi na ni vizuri Serikalini wanapokuwa wanaleta mapendekezo wawashirikishe wadau wote kuliko wakijifungia tu wanaleta ya kwao ambayo hayatafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hilo tu kwenye eneo la sekta ya ujenzi na *LATRA* wameleta mapendekezo ya kuhamisha baadhi ya mambo ambayo wanapeleka *TBS,* jambo ambalo si zuri na ni vizuri wakawashirikisha. Hata kwenye Wizara ya Kilimo nako kuna mapendekezo ambayo wameyaleta, wanahamisha shughuli zilizokuwa zinafanywa na mamlaka ya pamba, wanapeleka kwenye *TBS*. *TBS* kazi yake ni kutunza ubora na kuhakiki ubora ule ambao umefanywa kwenye eneo la viwanda. Hili naomba Waziri mwenye dhamana aliangalie na a-*review* kabisa hivi haya mapendekezo ambayo ameyaleta ambayo ukweli kimsingi ukiyafuatilia hayawezi kufanya kazi kama walivyokusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo napenda kusisitiza kwenye eneo hilo hilo, ni kumkumbusha Mheshimiwa Waziri *TBS* kupitia Bunge hili hili tuliwapa mamlaka ya kuhakiki mitambo ya magari na Serikali ikagharamia mtambo karibu wa shilingi bilioni 10 ambao ululetwa na umeshindwa kufanya kazi kwa sababu ya kung'ang'ania shughuli ambazo hawajazifanyia uhakiki ule unaokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nijikite kwenye sekta ya kilimo, kwenye sekta ya kilimo ni sekta ambayo ndiyo inayoweza kukuza uchumi na tuangalie nyakati zinavyokwenda. Sasa hivi dunia nzima ina njaa na tutakuwa na njaa kubwa na sisi kama nchi yetu ni nchi

ambayo ina maeneo ambayo tungeyapanga vizuri Serikali ikajikita, tungetatua baadhi ya maeneo na kuwafanya Watanzania wenzetu wakawa na kipato kikubwa sana na nchi ikawa na fedha ambazo zingesaidia kufanya shughuli zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo la ukosefu wa ngano tunajua Ukraine, Rusia kuna vita, Wazungu hawatakuja kuwasaidia Waafrika, ngano yote itabaki kule kule iweze kufanya shughuli za kuwasaidia wenzao. Niombe sasa Serikali ijikite katika kipindi hiki cha mwaka huu wa fedha wahakikishe kwenye maeneo ambayo yana uzalishaji mkubwa na unaofanana na hali ya hewa kama Mkoa wa Njombe, Mkoa wa Mbeya, Mkoa wa Songwe na Mkoa wa Arusha na hata kwetu Katavi kwenye eneo la Tarafa ya Mwese ni maeneo ambayo yanaweza yakazalisha ngano. Sasa wafanye utafiti wahakikishe wanawawezesha Watanzania kwenye maeneo haya wazalishe ngano ambayo itauzwa hapa hapa nchini na kupunguza fedha zile ambazo tunatafuta za kigeni kwenda kununua ngano nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni la muhimu sambamba na kukuza mazao ya mafuta. Tunayo mikoa ambayo tunazalisha mafuta ya michikichi kwa upande wa Mkoa wa Kigoma na Mikoa ya jirani kama vile Katavi, Tabora hadi Kagera wana uwezo wa kuzalisha michikichi, Wizara ihakikishe inawawezesha hawa wakulima wazalishe ili kuwe na uwezekano wa kuweza kuzalisha mafuta ndani ya nchi yetu. Kwenye zao la alizeti karibu kila mkoa alizeti inastawi mahali pote, wahakikishe wanaandaa mbegu, wanawapa mbegu bora ili wazalishe mazao hayo ambayo

yatapunguza kupoteza fedha za kigeni ambazo tunazitumia kwa ajili ya matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo tunaishauri Serikali ni kwenye sekta ya maliasili. Kwenye eneo la maliasili hatujafanya vizuri pamoja na jitihada ambazo zinafanywa na Serikali kuhakikisha tunatangaza utalii kwa nguvu zote na Mheshimiwa Rais amefanya hili vizuri sana, lakini kuna eneo ambalo hawajalifanyia kazi kama Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Nchi za Magharibi au zilizoendelea kwa ujumla zina uchafuzi wa mazingira kupitia viwanda. Sasa maeneo haya sisi kama Taifa hatujatumia fursa aliyopo, viwanda vyote duniani ambavyo vinazalisha na kuchafua mazingira vinatakiwa kulipa gharama za kutunza mazingira. Wenzetu Nchi jirani ya Kenya wanapata fedha karibu dola bilioni mbili kwa mwaka kupitia uvunaji wa hewa ya ukaa ambayo wanaifanya na sisi ambao tupo kwenye maeneo mengi ya misitu hatujanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri amefanya kazi kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais inayoshughulikia mazingira, analijua ninalolizungumzia. Tanzania wilaya chache tu ndizo ambazo zinavuna hewa ya ukaa. Wilaya ya Tanganyika nilikotoka mimi nina ushuhuda, vijiji karibu 10 vinanufaika, wanapata karibu kila kijiji kwa kipato cha mwaka huu tu wamepata bilioni tatu vijiji na tunategemea wanaweza wakapata karibu bilioni 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama tukitoa sheria ambazo tumeziweka zinazoziba mazingira ya kuweza

kukusanya fedha hizi kwenye *National Park* kama Wakenya wanavyofanya, kwenye misitu ambayo ni tengefu, naomba hili walifanyie kazi. Naamini Mheshimiwa Naibu Waziri analifahamu, tukieleza nguvu kwenye hii sekta ya misitu, Tanzania tuna uwezo wa kupata fedha zaidi ya bilioni 400 kwenye misitu tunayoimiliki. Naomba hili walifanyie kazi sambamba na kuchungulia ni mahali gani ambako tunafanya nao biashara, kwa sasa tunafanya na watu wa kati, *middle man* ambao wapo katikati, hatujawafikia wale ambao wanatoa hizo fedha. Naomba hili Wizara ilifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie eneo la sekta ya miundombinu. Tunapojenga miundombinu hasa barabara nashukuru Wizara ya Ujenzi imekuja na mpango wa kushirikisha sekta binafsi ili waweze kujenga barabara ambazo wata-*design,* watajenga na watakuwa *financier* wao, ni jambo lililo zuri. Sasa tuangalie ni barabara zipi tunazoenda kuzijenga, tujenge barabara ambazo zitakuwa na uchumi na zitakazorudisha *return* ya fedha tulizowekeza. Mfano, tunayo barabara ya kutoka Ifakara kwenda Madete hadi Njombe – Ludewa ambako kuna machimbo ya mkaa na sasa hivi kupitia vurugu ya dunia, mkaa unahitajika karibu kila sehemu. Naomba hili walifanyie kazi, tujenge barabara ambazo zina faida. Barabara nyingine ni ile ambayo inatoka Wilaya ya Mpanda, Mkoa wa Katavi kwenda eneo la Karema ambako Serikali imejenga bandari. Hii barabara waijenge haraka ili washike soko la Kongo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Kapufi, wajiandae Mheshimiwa Mpakate na Mheshimiwa Kwagilwa Reuben.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na niwashukuru ndugu zangu wa Wizara hii, lakini kwa ujumla wake nilifarijika niliposikia kwamba hawataacha kupeleka fedha katika maeneo yetu hata kama tutakuwa tumepata hati chafu. Jambo hili ni jema na yule aliyehusika kupelekea hati chafu ndiyo aadhibiwe, wananchi waendelee kupelekewa maendeleo, hilo ni jambo zuri na ni jambo lenye afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya kwanza kama si 2015 nilisimama hapa nikaendelea kuongelea habari za utalii, lakini habari za Ngorongoro. Bahati nzuri kipindi hicho nilikuwa ni Mjumbe wa Kamati hiyo wa mambo ya Maliasili na Utalii. Nilitembelea Ngorongoro, nilitembelea Loliondo, moja kubwa ambalo niliwahi kulisema wakati ule na nitalisema leo, bila utashi wa kisiasa hatuna Ngorongoro, bila utashi wa kisiasa hatuna Loliondo. Niseme, leo tunaiona hiyo Ngorongoro nzuri, Loliondo nzuri ni kwa sababu imehifadhiwa, bila uhifadhi hatuna maeneo hayo. Leo utatamani ni kwa sababu tumehifadhi, lakini tusipohifadhi ni eneo kama eneo lingine lolote, lakini kwa kupitia uhifadhi ndiyo panapata heshima hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana na tusisahau hiyo kauli nimemsikia hata mwenzangu mwingine akiongea hapa, mazingira yaliyoharibiwa hayana huruma,

yatakuadhibu tu hata kama ni miaka hamsini ijayo. Kwa hiyo, hilo Mheshimiwa kwa unyenyekevu mkubwa sana naomba tusilisahau. Katika eneo la utalii bosi wetu kafarijika kwa masuala ya *Royal Tour* na vitu vingine, lakini bosi wetu na naomba hapa tuelewane vizuri, atafanya yote, lakini katika eneo la utalii, bosi wetu ni mtalii na usipotii kiu yake haji, usipotii kiu ya mtalii haji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anahangaika, anakusanya fedha zake kwa muda mrefu ili kuja kutembea Tanzania, kwa hiyo wewe usipotii kiu yake, usipotengeneza mazingira rafiki haji, ana uwezo wa kwenda sehemu nyingine yoyote. Hapa naomba tuendelee kuelewana vizuri, yawezekana sisi kama Tanzania, kama nchi, leo nafarijika, kuna baadhi ya maeneo huko duniani vyanzo vyao vya utalii labda ni jengo refu, kitu cha namna hiyo, sisi Mungu ametupa zawadi ya pekee, leo hii fanya ufanyavyo hata kama utaweza yasukume maji kama ambavyo wengine wamesukuma maji ya bahari ya hindi *but thus not* Ngorongoro, fanya ufanyavyo hata kama utatumia *grader* kupalilia viwanja kama 10 au *15 but that is not endless plains* kwa maana ya Serengeti. Serengeti ina namna ya pekee, Ngorongoro ina namna ya pekee, hao wenzetu wengine vitu vyao ni *artificial,* vya kwetu ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, zawadi hii isiwe laana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tabia ya Mtalii nimesema usipotii kiu yake haji na naomba hapa tuelewe vizuri, kuna matabaka ya watalii. Wakati tumejipanga vizuri kabisa kwenda kuimarisha utalii wetu, kutangaza utalii wetu, vipi kuhusu sekta nyingine, naomba sana, kuna eneo hili, je, tumejipanga vizuri kwa maana ya *trained personnel,* watu

ambao wapo *well trained,* kwa sababu kuna mtalii wa madaraja, achilia kuna mtalii wanamwita labda mtalii kishuka, mtalii ambaye tunabanana wote huku huku, mahindi ya kuchoma na vitu vingine vya namna hiyo, lakini kuna mtalii anakuja anauliza je, kama nime-*fall sick*, nimeugua napata wapi tiba? Je, kama nchi tumejiandaa kwa hilo? Nitatibiwa wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, isije kuwa tumetengeneza vizuri, tumeimarisha utalii wetu, lakini ikitokea amekuja mtalii wa kiwango hicho, unaanza kuzungumzia habari ya *flying doctors* labda tumsafirishe kumpeleka nchi ya Jirani, maana yake nini? Mmepambana kuinua utalii lakini inapokuja ni suala kama hilo kwamba *you are finding flying doctors* ili kumpeleka nchi za jirani. Kwa hiyo, maana yake tujipange kwenye maeneo mapana zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanashindwa kuelewa jambo dogo kwa maana ya *customer care*. Leo hii kuna baadhi ya nchi ukifika tu uwanja wa ndege hata jinsi *taxi drivers* wanavyokupokea, inakupa nafasi ya kujua kwamba hapa napokelewa. Katika maeneo hayo wenzetu wa Wizara watengeneze mazingira, waandae watu wetu hata kama ni kwa kupitia semina tuwaandae watu hawa. Nimezungumzia habari ya *well trained personnel*, *waiters and waitresses,* watu hawa wakiwa *well trained* hata kama ni kwa semina, najua ni chanzo cha mapato kwa sababu mtalii huyo ambaye atakuwa amehudumiwa vizuri hawezi akaikimbia nchi hii, lakini hawa watu ambao ni *well trained* wana uwezo wa kuiuza nchi hata katika sekta nyingine. Unakutana na mtu anakwambia Tanzania hii tuna madini haya, tuna haya, lakini sio mtu unakutana naye, ndiyo

kwanza anasema kama hutaki acha. Tunawaandaje watu wetu? Hili ni jambo la msingi sana hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo, naomba niende katika sekta nyingine ambao ni eneo la madini. Naomba ifahamike vizuri, madini ya Tanzania, utajiri tuliopewa na Mungu, hatuko peke yetu. Hata kama ni dhahabu, hatuko peke yetu. Kwa hiyo, unapokuja na tozo; kwa mfano, sasa hivi tuna asilimia mbili ya kodi ya zuio. Wachimbaji wadogo waliwahi kukaa na Mheshimiwa Marehemu Dkt. Magufuli, tukazungumzia habari ya kutoa tozo hizo, na hii ndiyo unaona sasa hizi makusanyao ya dhahabu ni makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri mkafahamu tunapozungumzia mchimbaji mdogo, tuelewe mchimbaji mdogo ni yupi? Tafsiri ya mchimbaji mdogo ni ipi? Kuna mchimbaji mdogo jamani, hata machinga ana nafuu. Sasa mtu huyu, kama ndio huyu kweli mnamlenga kwa maana ya kodi hiyo, maana yake katika maeneo hayo ya machimbo kuna mtu unakuta amekaa miezi sita hajapata hata gramu hata moja. Ni vizuri pia mkayasoma mazingira hayo. Kwa hiyo, katika mazingira hayo, kuna mtu huyu kama hujamtengenezea *incentives,* atatorosha madini yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba watu wa Wizara, Serikali imefanya kazi nzuri ya kutengeneza masoko, wachimbaji wanatoka katika maeneo yao, wanapeleka dhahabu sokoni. Bananeni na hawa wanunuzi wa pale; kama kuna utoroshaji hapo, mbanane hapo, lakini nje ya hapo nakuhakikishia… *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapufi!

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Naam Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Kaa chini kwanza.

Kanuni yetu ya 68 kutozungumza jambo ambalo lina maslahi binafsi ya kifedha. Wakati wa majadiliano Bungeni au kwenye Kamati yoyote ya Bunge, Mbunge hataruhusiwa kuzungumzia jambo lolote ambalo yeye mwenyewe ana maslahi nalo binafsi ya kifedha. Ina utaratibu mwingi sana. Kwa nini nakwambia hivyo? Kifungu kidogo cha (2) kinasema, "kwa madhumuni ya Kanuni hii, Mbunge au mwananchi yeyote anaweza kumwarifu Spika kwa maandishi akitoa na ushahidi kuwa Mbunge amezungumzia jambo ambalo ana maslahi nalo binafsi. Unatakaiwa u-*declare interest*.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, na-*declare interest,* pia mimi ni mchimbaji mdogo wa madini. Kwa msingi huo, hili ninaloliongea ni kwa uzoefu mpana na lengo langu ni jema la kuisaidia nchi hii ili eneo la uchimbaji liwe na msaada kwa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kusisitiza, nawaomba sana kwa sababu lengo ni kufanya nchi iendelee kupata kipato kikubwa. Kwa hiyo, kwa sura hiyo nawaombeni sana wenzetu wa Wizara, katika eneo hilo nina uhakika tuna uwezo wa kuitoa nchi. Nafahamu tulikuwa na asilimia 6.7 mwaka 2020, lakini tukaenda asilimia 7.2 mwaka 2021. Kwa hiyo, tuna uwezo wa kwenda mbali zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa utoaji mikopo kwa wachimbaji, ni jambo jema, ni jambo la afya. Siyo kwa maana ya mwisho, lakini *GST,* kwa maana hawa watu ni wenzetu wa utafiti. Nchi hii ni kubwa, ina maeneo mengi, lakini hawa wenzetu wa *GST* tusipowazesha; leo karibia nchi kila sehemu utasikia leo kuna mfumuko wa madini, sasa wenzetu wa *GST* mko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Bashe alipokuwa anazungumzia habari ya kuimarisha kilimo, lakini eneo la uchimbaji lina uwezo pia wa kuajiri Watanzania wengi *especially* vijana, lakini wenzetu watusaidie kitu kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema katika kilimo tutakuwa na *extension officers* waende kwa mkulima mmoja mmoja, vipi wenzetu wa madini? Mnasemaje Ma-*geologist* kwenda kwa wachimbaji huko kumsaidia mchimbaji? Kwa sababu hapa unaweza ukasema eneo hili labda akiba *(reserve)* ni kilo 20 za dhahabu. Maana yake kumbe tukifanya kitaalamu, tuna uwezo wa kuzipata kilo 20 za dhahabu, lakini watu wanachimba kwa *design* ile ile ya zamani ya kuganga njaa. Watusaidie kwenda mbali zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo, nimalizie na suala la kilimo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Nakushukuru, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mpakate, jiandae Mheshimiwa Reuben.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii nami nitoe mchango wangu kwenye hoja iliyoko mezani. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama jioni hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili naomba niwapongeze, nikianzia na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waziri wa Fedha na waandamizi wake wanaofuatana katika kazi hii, kwa kazi nzuri waliyoionesha kwa ajili ya Watanzania. Ama kweli Mama ameonesha kwamba yeye ni Mama, ana uwezo wa kushinda na njaa lakini akampa mtoto wake tonge la mwisho ili aweze kushiba, ili Watanzania waweze kufurahi wote. Hili ndilo alilolionesha katika Bajeti hii ya Mwaka wa Fedha 2022/2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza naomba niongelee suala la kilimo. Naishukuru sana Serikali, namshukuru Waziri wetu kwa kurekebisha na kurudisha *Export Levy* kwa zao la korosho. Naomba kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, uzalishaji wetu ulikuwa mkubwa, ulikuwa unaongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na mapato ya *Export Levy* kuhudumia zao la korosho, mpaka tulifika hatua tuyolifikia tani 323,000. Baada ya kuondoa *Export Levy* ambayo ilianzishwa na wadau, basi zao hili limeshuka mpaka leo hatujafika uzalishaji wa tani 250,000. Naamini kwa kurejesha huku, zao litaendelea kupaa kwenda juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo nina mashaka na nina ushauri katika hili, kutokana na uzoefu niliyokuwa nao. Kwenye jambo hili mmestiki sana kwenye *Sulphur,* lakini *Export Levy* ina mambo mengi ambayo yanayofanya korosho iweze kukua katika uzalishaji. Moja ya jambo ambalo likuwa linashughulikiwa na *Export Levy* ni pamoja na kuzalisha miche bora na kusambaza kwa wakulima. Hiyo ni pamoja na kutoa fedha kwa ajili ya usimamizi kwenye Halmashauri zetu. Sasa hivi Halmashauri zinahangaika kusimamia zao la korosho kwa sababu hawana fungu maalum linalofanya waweze kusimamia zao hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na suala la usimamizi, tulikuwa tunajenga maghala. Pale kwetu Tunduru tulianza kujenga ghala, ilitolewa Shilingi bilioni moja, lakini tangu 2015 mpaka leo ghala lile lipo tu kwenye *foundation*. Naomba fedha hizi zirejee kutengeneza ghala lile likamilke ili katika mfumo wa stakabadhi ghalani tutumie maghala yenye ubora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo Tunduru tu, Mkuranga pamoja na kule Tanga haya Maghala yalianzishwa na yalifikia hatua yaliyofikia. Tunaomba sana kwa kuwa *Export Levy* hii inarudi tena, basi itumike kuhakikisha yale maghala yanajengwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kujengwa vizuri, tunaomba sana Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo ihakikishe kalenda ya uzalishaji wa korosho inafuatwa, siyo unatoa fedha mwezi wa Sita ya kununulia *Sulphur* wakati *Sulphur* inatakiwa mpaka kufika mwezi wa Tatu na wa Nne iwe imeshafika ili wakulima waweze kuwahi. Kwa hiyo, tusianze tena kuizungusha hii fedha kwa sababu

tayari imeshapitishwa kisheria, basi naomba sana jambo hili lizingatiwe ili kuhakikisha kwamba hili zao linaenda mbali kwa sababu linawaleta faida kubwa wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda nichangie kwenye hilo, ni suala la kilimo cha umwagiliaji. Naishukuru Serikali kwa kuongeza na kutenga fedha kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Ni wazo langu kubwa na kwa kuishauri Serikali, basi tuweke *specific area* angalau tuangalie maeneo machache ambayo tutatia nguvu kubwa tuweze kuzalisha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimebahatika kwenda kuangalia shamba la miwa pale *Kagera Sugar*, tumeona namna ya mwekezaji yule amejitolea kwa nguvu zake na kuhakikisha kwamba anazalisha na anaweka msimamo wa kumwagilia ili aweze kuzalisha tani 300,000 za sukari. Naomba kwa mtindo ule, wenzetu wa Serikali wakajifunze, tuanzishe mashamba ya mpunga, mashamba ngano na mashamba ya mahindi, kwani yatatusaidia kuhakikishwa kuondokana na tatizo la chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kwa umwagiliaji ule kama tutaenda kwenye mazao yote, basi tunaweza ku-*export* mazao mengi nchi za nje kwa ajili ya kupata umwagiliaji wa aina tofauti. Kwa kweli, tabia nchi imetuathiri, uzalishaji wa kutegemea mvua imekuwa ni changamoto kubwa sana. Tuweke mkazo, tuweke nguvu kwenye uzalishaji wa kilimo cha umwagiliaji ili kuhakikisha kwamba tunaondokana na shida ya njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, wakulima wetu huko vijijini hasa Wilaya ya Tunduru hasa Jimbo la Tunduru Kusini wanaathirika sana na tembo. Kile kile walichokilima vyote vinaondoka. Sasa nadhani hawa tembo wana ramani, wana *time table* ya kilimo hiki cha kawaida. Kama tutaanzisha kilimo kidogo hiki cha umwagiliaji, kipindi cha kuanzia mwezi Julai, mpaka Oktoba mpaka kufika Desemba, hakuna tembo, humwoni kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi tusisitize suala la kulima kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima wetu wadogo wadogo hasa kule Misaje, maeneo ya Mkotamo, Madaba, kote huko kuna mito na mahali ambapo tunaweza kulima kwa umwagiliaji angalau tukakwepa hawa tembo wanaokuwa na tabia ya kuweza kwenda kuvamia mazao ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwenye suala hili la *Export Levy* naomba tujenge maghala kwenye vijiji vyetu. Tunapokwenda na Mfumo wa Stakabadhi Ghalani naomba mtembelee muone hali ya vijiji hivyo jinsi ilivyokuwa. Naomba fedha zitengwe kwa ajili ya kujenga maghala kwenye vijiji vyetu yasaidie kwenye Mfumo wa Stakabadhi Ghalani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kumshukuru Rais wetu, ni suala la kutoa elimu bure kwenye Kidato cha Tano na cha Sita. Pamoja na changamoto ambayo sisi Wabunge, hasa mimi katika Jimbo langu ilikuwa na kila mwaka nalipa takribani Shilingi milioni mbili mpaka tatu kwa ajili ya kulipia ada Kidato cha Tano na cha Sita. Kwa hili Serikali kweli wametusaidia, nami angalau nitapumua kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ila changamoto tuiangalie, kuna wazazi washalipa *full*, *Five* na *Six*, fedha iko benki kwenye shule za sekondari. Sasa tuweke utaratibu, kwa sababu mwaka wa fedha huo haujafika na mtu alilipa *advance,* basi mtoe maelekezo, wale ambao tayari walishakuwa wamelipa basi tuone namna ya kuweza kuwafidia, kwa sababu mwaka wa fedha wao ulikuwa bado haujafika, Kidato cha Tano ndiyo kwanza kimefunguliwa. Malalamiko hayo yapo kwenye maeneo mengi tuhakikishe wale wazazi wanarudishiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie kwenye hili tumeacha sehemu moja ambayo tulitakiwa tuiangalie. Kila Tarafa tuweke *High School*. Jambo la kujenga madarasa 12,000 ya sekondari limeongeza idadi ya wanafunzi kwenye shule za sekondari kuanzia Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne, lakini bado hatujaangalia wakimaliza Kidato cha Nne hawa wanaenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali iangalie uwezekano wa kila Tarafa kuweka *High School* ili kuwapunguzia wazazi mwendo mrefu wa kuwapeleka watoto kutoka Tunduru kwenda Tabora, mwingine kwenda Bukoba, ambapo nauli yao ni mara tatu au mara nne ya ile ada ambayo tumeiondoa. Naomba sana kwenye jambo hili tuliangalie kwa hali ya juu na kwa huruma kwa sababu walio wengi waliosoma kwenye shule hizi za Sekondari za Kata ni wakulima ambao uwezo wao ni mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tujitahidi sana miaka ijayo tuangalie namna ya kuweza kuweka *at least* kila Tarafa iwe na *High School* ili watoto wetu waendelee

kusoma mazingira yale yale yatakayosaidia wazazi wetu kwa ajili ya kuondoa gharama za maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Reuben.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita, Mama shupavu, Mama mchapakazi kwa kutuletea bajeti ya kizalendo na ambayo ina harufu ya mapinduzi. Bajeti hii imekuwa ya tofauti kwa sababu ya mambo mawili makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni bajeti inayoelekeza kubana matumizi; na jambo la pili ni bajeti ambayo inakwenda kuimulika Sheria ya Manunuzi na kuiwekea *control*. Mambo hayo mawili ni mambo makubwa ya msingi sana, naipongeza sana Serikali kwa jambo hili kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2021 bajeti yetu ilikuwa shilingi trilioni 37.99 na makusanyo ya ndani tulilenga tukusanye shilingi trilioni 21, lakini tukaishia kukusanya shilingi trilioni 17 mpaka Aprili. Mwaka huu bajeti yetu ni shilingi trilioni 41.48 na makusanyo ya ndani tunalenga tukusanye shilingi trilioni 28.02. Kwa maana hiyo, katika haya

makusanyo ya shilingi trilioni 28.2, *TRA* inatakiwa ikusanye shilingi trilioni 23.65. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pale *TRA* zipo *department* nne za kikodi. Ipo *Department* ya *Custom and Excise, Department* ya *Domestic Revenue*, *Department* ya *Large Tax Payers* na *Department* ya Kikodi ya *Tax Investigation*. Mimi nitaongelea *department* moja ya *Custom and Excise*, *Department* yetu ya Forodha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye makusanyo ya *TRA* mwaka 2021 ya shilingi trilioni 17.2 *department* hii ilikusanya asilimia 40. Vivyo hivyo hata makadirio ya mwaka huu wa fedha shilingi trilioni 23.68 makusanyo ya ndani, tunatarajia *Department* hii ikusanye asilimia 40, karibia shilingi trilioni 10. Sasa *department* hii inakusanya wapi? Maeneo yake makubwa ni wapi? Maeneo yake makubwa ya kwanza ni bandari zetu, kwenye *airports* zetu na kwenye mipaka yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaangazia eneo moja katika hayo niliyoyataja nalo ni la bandari. Natambua kwamba tunazo bandari nyingi, lakini nitazungumzia bandari zetu tatu kubwa; Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Tanga na Bandari ya Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Dar es Salaam peke yake kwa Tanzania ndiyo bandari pekee ambayo *International Trade* kwa ukubwa inafanyika kwa karibia asilimia 90. Asilimia 90 ya biashara yetu ya Kimataifa inafanyika Bandari ya Dar es Salaam. Sasa ni nini tunatakiwa tufanye kwenye maeneo haya ya hizi bandari

tatu ili tukakusanye zaidi? Maana kupanga matumizi siyo shida, shida ni namna ya kukusanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, tunatakiwa tukanunue vifaa vya kisasa kwa ajili ya ku-*deal* na *containers*. Kwenye biashara ya bandari, fedha nyingi ipo upande wa *containers.* Vifaa ninavyoviongelea hapa, siongelei hizi *cranes* ambazo tunazo kwa sasa, hizi *Gottwald Cranes,* tunatakiwa tuwe na vifaa vya kisasa *SSG*. Hii inaitwa *Ship-to-Shore Gantry Cranes.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya gati zetu zilivyo, kwa namna ambavyo Mheshimiwa Rais ameweka fedha pale Bandari ya Dar es Salaam, tumeiendeleza gati ya kwanza mpaka gati ya saba. Tumeweka pale mradi wa dola milioni 420 kwa ajili ya kuendeleza hizo gati. Sasa gati namba sita na namba saba ndizo gati ambazo zita-*deal* na *containers*. Tunatakiwa tukanunue hivi vifaa *SSG* (*Ship-to-Show Gantry Cranes)*. Kifaa kimoja katika hivi, kinagharimu kama Euro milioni 11 hivi au milioni 10 na kitu. Kwa ukubwa wa gati zilivyo pale, gati moja itahitaji angalau kwa uchache, tena hizi *SSG* angalau tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upanuzi tuliyoufanya pale, bandari yetu kwa sasa ina uwezo wa kupokea meli kubwa sana zile za *post-panamax,* na zile meli zikija pale zina urefu mkubwa na zinabeba *containers* nyingi. Kwa hiyo, kutumia vifaa hivi vidogo vidogo tulivyonavyo pale, tunapoteza biashara. Meli zinakaa muda mrefu kwenye kushusha na zinakaa muda mrefu kwenye kusubiri kuingia. Kwa hiyo, tunapoteza biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiweka *SSG* tatu tatu kwenye kila gati, tafsiri yake ni kwamba hizi *post-Panamax ships* huwa zinakuwa na *partition* tatu. Kwa hiyo, kila crane itashambulia *partition* moja. Tutashusha mizigo yetu ndani ya muda mfupi, meli zitaondoka na tutavutia watu kuja kufanya biashara na sisi kwenye eneo letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, tunatakiwa tufunge mifumo ya ku-*control containers* ambayo ni ya *N-generation*; mifumo ya kisasa ambayo inai-*trace container* kutoka *the pot of loading* mpaka hapa inapofika kwetu na mpaka inaporudi kwa wenye nayo. Biashara ya *container* duniani ndiyo biashara kubwa inayo-*control* biashara za meli. Kwa hiyo, tusipofanya hivi tutakuwa hatujawekeza vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni *skilled labour*. Watu wetu tuwaelimishe, tuwasomeshe wajifunze mambo haya. Sasa ukurasa wa 27 wa Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti inasema, "Kamati imebaini kwamba Mamlaka ya Bandari, badala ya kuendeleza kuwekeza ili kuwe na ufanisi katika uondoshaji wa shehena bandarini inafikiria kutumia makampuni ya nje kama vile *DP World* na *TICTS*. Hatua hii inaweza kuleta mafanikio ya ufanisi lakini itapunguza kwa kiasi kikubwa mapato ya Serikali." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kushauri ni nini? Ninashauri kwa uwekezaji huu ambao tumeufanya bandarini, tusiende kufikiria kuwapa watu kuendesha bandari yetu. Tumeweka hizo Dola milioni 420 Bandari ya Dar es Salaam, tumeweka Shilingi bilioni 256 za Kitanzania Bandari ya Tanga, na tumeweka Shilingi bilioni 157 Bandari ya Mtwara. Sasa uwekezaji huo mkubwa; vifaa hivi

kuvinunua hata Shilingi bilioni 500 haifiki. Sasa Shilingi bilioni 500 ndiyo itufanye tuigawe Bandari yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tusifanye hivyo. Twendeni tukafanye utafiti kama ili tuone kama kuna *genuine reasons* ya kumpa mtu kuendesha bandari yetu. Tunao uzoefu, tuliwapa *TICTS,* leo ni mwaka wa 22 tunao pale, wakipata Shilingi bilioni 230, sisi tunachoambulia ni Shilingi bilioni thelathi na kitu tu. Ukiweka na hela ya pango ni kama Shilingi bilioni tisini na kitu tu, *it is a loss*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tumeshakubaliana kama Watanzania, Bandari ya Bagamoyo tutawapa watu. Hakuna mwenye ubishi juu ya hilo. Sasa na hii ya Dar es Salaam nayo tuwape watu? Hata ukiwa na nyumba yako ya kupangisha, unapangisha vyumba vyote mpaka unakosa pakukaa? Haiwezekani! *(Makofi)*

Mhehimiwa Naibu Spika, nami naishauri Serikali, na huu ushauri ni kwa nia njema, twendeni tukawekeze vifaa ambavyo vinatakiwa ambavyo ni hizi *cranes*, tuwekeze hii mifumo ya kisasa ambayo ni *N-generation* na tuwaeleimishe watu wetu halafu tuendeshe bandari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uwekezaji huu mdogo hata bila hivyo vifaa, mwaka huu wa fedha, 2022/2023 mpaka kufikia mwezi wa Aprili, Bandari ilikuwa imekusanya Shilingi bilioni 888, ukilinganisha na mwaka 2021 kabla ya uwekezaji ambapo muda kama huu tulikuwa tumekusanya Shilingi bilioni 751. Hapa tuna-*handle container* 600,000 tu, tukiweka hivi vifaa ninavyovisema, tutaenda kwenye *full swing* ya ku-*handle container* 1,500,000. Tukifanya hivyo, hii

*department* ya *TRA* ambayo naisemea hapa ya *Customs* itakusanya zaidi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijajua ni kengele ya kwanza au ya pili.

**MJUMBE FULANI:** Ya pili.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana kwa fursa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa michango mizuri. Naahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.02 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 20 Juni, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*